# Nipashe

Alhamisi Desemba 12, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580099

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure




## Daktari ahusisha tezi dume kusababishwa na mchepuko

UK. 3

# Wengi watinga kwa Mkemia kujua uhalali baba wa mtoto

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**MFUNGWA ALIYESAMEHEWA NA MAGUFULI ADAIWA KUIBA TENA**

SIKIO la kufa halisikii dawa. Ndivyo inavyoweza kuelezwa baada ya mfungwa aliyeachiwa kwa msamaha wa Rais John Magufuli wakati wa maadhimisho ya Uhuru, kukamatwa kwa tuhuma za wizi zikiwa zimepita saa nane tangu alipotoka gerezani.

UKURASA WA 4

**BODI YAWATOA HOFU WANAFUNZI MIKOPO**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imesema ina fedha za kutosha na hadi jana imeshapokea Sh. bilioni 186...

## MTOTO ABAKWA MPAKA KUFARIKI

UK.3



Aliyekuwa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamali Malinzi, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, tayari kwa kusikiliza hukumu ya kesi iliyokuwa inamkabili. **HABARI UK. 2**. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# Lissu amkingia kifua Mbowe

**Ni** juu ya kauli yake kuhusu maridhiano, asema alikuwa sahihi kusema hivyo... *Uk. 2*

UK. 2

**MICHEZO** YANGA YAPUKUTISHA MAPRO, BALINYA NJE UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# Malinzi ahukumiwa kulipa faini mil.1.5/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imewahukumu aliyekuwa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamal Malinzi na katibu mkuu wake, Selastine Mwesigwa, kulipa faini ya Sh. milioni 1.5 au kwenda jela miaka minne.

Vigogo hao walitiwa hatiani kwa makosa ya kughushi muhtasari wa kubadilisha watiasaini wa akaunti za (TFF kwamba kamati ya utendaji imepitisha mabadiliko hayo.

Pia imemtia hatiani Mwesigwa kwa kosa la nne la kuwasilisha muhtasari wa kughushi benki kwa ajili ya kubadilisha watiasaini. Washtakiwa hao wanatakiwa kulipa kosa la kwanza Sh. 500,000 kila mmoja au jela miaka miwili.

Katika kosa la pili, Msigwa peke yake alitakiwa kulipa faini ya Sh. 500,000 au jela miaka miwili.

Kadhalika, Mahakama hiyo imewaona mshtakiwa wa tatu, Nsiande Mwanga, aliyekuwa mahabusu tangu Juni 2017 na Flora Rauya aliyekuwa nje kwa dhamana kuwa hawana hatia na imewaachia huru.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Maira Kasonde. Akisoma hukumu hiyo, Kasonde alisema baada ya kupitia ushahidi wa upande wa Jamhuri, Mahakama imewatia hatiani Malinzi na Mwesigwa kwa makosa hayo.

"Mahakama yangu imewatia hatiani kwa makosa mawili, kosa la tatu linawakabili wote wawili kila mshtakiwa atalipa faini Sh. 500,000 au jela miaka mwili na la nne linamkabili Mwesigwa peke yake, atalipa faini Sh. 500,000 au kwenda jela miaka miwili," alisema na kuongeza:

"Katika mashtaka ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha fedha, Mahakama yangu imeona hakuna ushahidi wa Jamhuri uliothibitisha makosa hayo dhidi ya washtakiwa."

Aidha, alisema mahakama hiyo imewaachia huru washtakiwa hao katika makosa 18 ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha fedha kati ya mashtaka 20 yaliyokuwa yanawakabili. Akiichambua hukumu hiyo, hakimu alisema kuhusu hoja za mshtakiwa kuikopesha fedha TFF ni kweli alitoa fedha hizo lakini anaungana na Jamhuri kwamba hakufuata taratibu za shirikisho hilo kuhusu mkopo kutoka kwa mtu binafsi. Kabla ya hukumu hiyo, Wakili wa Utetezi, Nehemia Nkoko, alidai kuwa washtakiwa ni wakosaji wa mara ya kwanza na kwamba wamekaa mahabusu miaka miwili na nusu.

"Malinzi ana miaka 60 kwa hiyo yuko kundi la wazee ana watoto wanaomtegemea na anasumbuliwa na maradhi ya shinikizo la damu," alidai.

Kwa upande wa Mwesigwa, alidai kuwa anategemewa na mama yake mzazi mwenye miaka 89 na ana watoto wadogo wanaomtegemea na kuiomba Mahakama kuwapunguzia washtakiwa hao adhabu.

Hata hivyo, kwa kuwa hukumu hiyo ilisomwa mpaka saa 11:30 jioni, vigogo hao hawakulipa faini kwa kuwa muda wa kazi ulishapita.

# Wengi watinga kwa mkemia kujua uhalali baba wa mtoto

**Na Augusta Njoji,**

DODOMA

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) Kanda ya Kati, imesema asilimia 90 ya sampuli za kupima vinasaba (DNA) ilizozipokea, zililenga kuangalia uhalali wa baba wa mtoto.

Meneja wa kanda hiyo, Musa Kuzumila, aliyasema hayo jana alipozungumzia mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka miwili na nusu tangu kuanzishwa kwa ofisi hiyo katika ziara ya timu ya maofisa habari wa wizara na taasisi zake mkoani Dodoma.

Alisema kati ya sampuli mbalimbali 5,106 zilizokusanywa kwa kipindi hicho, 36 zililenga kuangalia uhalali huo, akieleza kuwa majibu ya sampuli hizo husaidia kumaliza kesi au migogoro kwa wakati.

"Hapa sina takwimu sahihi za kina baba wangapi wamesingiziwa watoto ambao si wao, tumekusanya sampuli 36 za DNA, asilimia 90 kati ya hizo ni za kusaka uhalali wa baba wa mtoto.

"Huwa tunapeleka kuchunguza kwenye maabara zetu zilizopo Dar es Salaam na Mwanza, tumekusanya na kufanya uchunguzi sampuli 5,106 hadi Desemba hii.

"Tunapofanya uchunguzi wa namna hii, DNA inahusika moja kwa moja na kutoa ushahidi mahakamani na kusaidia kesi kutatuliwa kwa wakati," alisema.

Alibainisha kuwa asilimia kubwa ya sampuli zilizokusanywa, zilikuwa za dawa ya kulevya hususan bangi. Alisema sampuli za dawa hizo wamekuwa wakizipokea kwa kiasi kikubwa.

"Sampuli ambazo tunachukua ni pamoja na dawa za kulevya, mazingira kutoka kwenye viwanda kuangalia namna wanachakata maji taka kwenye viwanda kabla ya

INAENDELEA UK. 8




Mbunge wa Viti Maalum wa Jimbo la Tabora, Munde Tambwe (wenye gauni la kijani na njano), akipokea saruji tani 12.5 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa kike wa kata mbalimbali za Tabora iliyotolewa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA). **PICHA: TAA**

# Tundu Lissu amkingia kifua Mbowe

**Na Maulid Mmbaga**

MWANASHERIA Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, amezungumzia uamuzi wa mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, kutaka maridhiano ya kitaifa kuhusiana na demokrasia nchini.

Mbowe aliibua hoja hiyo alipofuatana na wajumbe wa Kamati Kuu ya Chadema kwenye Uwanja wa Kirumba jijini Mwanza Jumatatu ikiwa ni mara ya kwanza kwa chama hicho kushiriki maadhimisho ya Uhuru tangu uchaguzi mkuu wa 2015.

Mbowe alipopewa nafasi na Rais John Magufuli kutoa salamu kwa maelfu ya wananchi na viongozi waliohudhuria maadhimisho hayo, alisema ameshiriki kama uthibitisho wa ulazima kuwapo maridhiano, kuvumiliana, kukosoana na kuruhusu demokrasia.

Jana, Lissu alizungumzia kwa kina hoja hiyo, alisema kuwa Mbowe kuomba maridhiano na serikali hakuonyeshi udhaifu, bali ni katika jitihada za kutafuta usawa wa kidemokrasia.

"Maridhiano ni hali ya kuhitaji kuwa na makubaliano ya kupata na kukosa sehemu," Lissu aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter.

Alisema kutaka maridhiano siyo kuunga mkono juhudi, ila ni katika mchakato wa kuhitaji kuwapo kwa maelewano, akieleza kuwa baadhi ya wanasiasa walitafsiri kauli hiyo vibaya na kuona Mbowe ameelemewa na kukosa njia ya kupenya na akaamua kutumia fursa hiyo kuungama.

Alisema suala la maridhiano siyo jambo la siku moja, bali linahitaji muda kutegemea mambo mbalimbali yanayohusisha mjadala huo.

Mwanasheria huyo ambaye yuko Ubelgiji kwa takribani miaka mwili sasa akiendelea na matibabu yake baada ya kushambuliwa kwa risasi jijini Dodoma mwaka juzi, alitolea mfano wa aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Nelson Mandela aliyetiwa hatiani wakati akihitaji maridhiano na makaburu.

"Mandela hakuanza kuzungumza na makaburi baada ya kutoka gerezani mwaka 90, mazungumzo yalianza muda mrefu tangu akiwa kizuizini huku vita vya ukombozi vikiendelea," alisema.

Tangu Mbowe atoe hoja hiyo ya kutaka maridhiano, kumekuwa na mijadala mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii, baadhi ya wanasiasa wakipinga uamuzi huo na wengine wakiunga mkono.

**HABARI KITAIFA**

# Mwanafunzi abakwa hadi kufa Dar

**Na Juster Prudence**

JESHI la Polisi mkoa wa kipolisi Ilala, linawashikilia vijana wanne kwa tuhuma za kumbaka kwa zamu mwanafunzi wa darasa la sita mwenye umri wa miaka 14 na kumsababishia kifo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ilala, Zuberi Chembela, alisema tukio hilo lilitokea Desemba 8, mwaka huu, majira ya jioni maeneo ya Pugu Bombani.

Kamanda alisema watuhumiwa hao wako mahabusu huku jeshi la polisi likiendelea na uchunguzi ikiwamo kupata taarifa kutoka kwa daktari aliyehusika na vipimo vya mtoto huyo.

Kwa mujibu wa Kamanda huyo, uchunguzi ukikamilika watapeleka jarida kwa wakili wa serikali ili atengeneze hati ya mashtaka watakayoitumia kuwafikisha watuhumiwa mahakamani.

Naye Mwenyekiti wa mtaa huo, Amani Bungara, alisema kutokana na tukio hilo, ameamua kila mwenye nyumba katika eneo hilo kueleka majina ya wapangaji wake katika Ofisi za Serikali ya Mtaa ili wajulikane.

# Daktari afunguka uhusiano wa tezi dume na mchepuko

**Na Boniface Gideon,** TANGA

MSIMAMIZI wa upimaji wa tezi dume na virusi vya ukimwi wilayani Pangani, Dk. Paul Chabai, amefunguka na kueleza chanzo cha kupata tatizo hilo kwa wanaume.

Akizungumza na Nipashe jana, daktari huyo aliitaja sababu ya wanaume kupata tezi dume kuwa ni kuwa na msururu wa wanawake wengi ambao hujamiiana bila kinga huku sababu ya pili ikiwa ni uwapo wa saratani japo inahitaji kupata vipimo vikubwa.

Kutokana na maelezo hayo, Dk. Chabai alisema wanaume walio na wapenzi wengi, maarufu kama michepuko wako hatarini kupata tezi dume.

"Unajua tezi dume ni uvimbe ambao huwa unajitokeza pembeni karibu na sehemu za siri na haujitokezi haraka. Unachukua muda mrefu na mwanaume anapokutana na wanawake wengi, ndivyo anavyojiwekea hatari ya kupata ugonjwa huu," alisema Chabai.

Aliongeza kuwa tezi dume haiambukizwi kwa mbu kama ngiri maji (mabusha) bali ni uvimbe ambao hujitokeza na huchukua muda mrefu.

"Naomba wanaume tujiwekee utaratibu wa kwenda hospitalini kupima afya zetu kwani ukigundulika mapema ni rahisi kupata tiba lakini ukichelewa tatizo linazidi kuwa tiba," alisisitiza Chabai.

Aliongeza tezi dume ikiwa katika hatua za mwanzo, mgonjwa anaweza kupatiwa tiba ya vidonge na madaktari bingwa kwa kufuatilia utaratibu wa vipimo vya ugunduzi.

"Lakini kama imefikia katika hatua za juu zaidi, kwa maana ya kukomaa, mgonjwa hufanyiwa operesheni ambayo huondoa kabisa tezi dume," alisema.

Dk. Chabai alibainisha kuwa changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni elimu ndogo kwa wanaume juu ya ugonjwa huo hali inayosababisha kuwapo kwa idadi ndogo ya wanaume wanaojitokeza kupima na wengi wao hujitokeza baada ya ugonjwa kuwa mkubwa.

# Mfungwa aliyesamehewa adaiwa kuiba

**Na Romana Mallya**

SIKIO la kufa halisikii dawa. Ndivyo inavyoweza kuelezwa baada ya mfungwa aliyeachiwa kwa msamaha wa Rais John Magufuli wakati wa maadhimisho ya Uhuru, kukamatwa kwa tuhuma za wizi zikiwa zimepita saa nane tangu alipotoka gerezani.

Mfungwa huyo, Musa Msolwa, maarufu kama Hitler, ambaye aliachiwa juzi saa 11:00 jioni Gereza la Makambako mkoani Njombe, na ilipofika saa 9:00 usiku akiwa mtaani, aliamua kwenda kwenye nyumba ya kulala wageni ya Nang'ano na kuvunja ili kujipatia fedha.

Akisimulia tukio hilo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi (ACP) Khamis Issa, alisema Msolwa baada ya taratibu zote za kutoka gerezani kufanyika, alikuwa mfungwa wa kwanza kushukuru kitendo cha Rais kuwaachia kwa msamaha.

"Wakati akishukuru alisema walizoea kufanya wizi wakienda mtaani wasiende kuiba na aliomba serikali isaidie kujengwa Mahakama Kuu ya Njombe,"

INAENDELEA UK. 8


**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

**MNADA WA UUZAJI WA VIWANJA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote kuwa zoezi la uuzaji wa Viwanja kwa njia ya Mnada litafanyika tarehe **14 Disemba, 2019** siku ya Jumamosi. Mnada utafanyika katika eneo la wazi la Manispaa ya zamani (karibu na Sabasaba) kuanzia saa 4:00 Asubuhi. Zoezi la kutembelea viwanja hivyo litafanyika Ijumaa tarehe 13/12/2019 saa 4:00 asubuhi eneo la mnada. Usafiri utakuwepo.

Viwanja vinavyouzwa ni Maeneo ya:

| ENEO | MATUMIZI NA BEI TSHS KWA (SQM1) |
|---|---|
| IYUMBU (New Town Centre) | • Viwanja vya Nyumba za kupangisha (Apartments)<br>• Viwanja vya Biashara<br>• Viwanja vya Viwanda Vidogo |
| NALA (Industrial Area) | • Viwanja vya Viwanda vya aina mbalimbali |
| NJEDENGWA (Investment Centre) | • Viwanja vya Nyumba za kupangisha (Apartments)<br>• Viwanja vya Biashara |
| NZUGUNI (Jirani na Uwanja wa Mpira, Soko Kuu na Stendi kuu mpya ya mabasi) | • Viwanja vya Hoteli<br>• Viwanja vya Biashara<br>• Viwanja vya Maduka makubwa (Shopping Malls) |

**NB**:

- Asilimia 50 ya Malipo italipwa siku ya Mnada
- Asilimia 50 inayobaki italipwa ndani ya siku 14 baada ya Mnada.

Tangazo hili limetolewa na:

**Mkurugenzi wa Jiji,**
**DODOMA**

215551101



**TANZANIA NATIONAL BUSINESS COUNCIL**

**SALAMU ZA RAMBI RAMBI**



Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Balozi Mhandisi John W. H. Kijazi, Wajumbe na Watumishi wote wa Baraza la Taifa la Biashara, tunatoa pole sana kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki, CEOrt, na wote walioguswa kwa kuondokewa na mpendwa wetu Ndugu Ali Mufuruki.

Daima atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya Taifa kupitia ushauri wake na kuhamasisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta binafsi. Mpaka umauti unamkuta, Ndugu Ali Mufuruki alikuwa ni Mwenyekiti Mwenza wa Kikundi Kazi cha Viwanda cha Baraza la Taifa la Biashara, Pia amekuwa mjumbe wa Baraza la Taifa la Biashara kwa vipindi tofauti. Naomba tumuuenzi kwa vitendo yale yote aliyoyatenda na kushauri ili kuliletea maendeleo Taifa letu kupitia sekta binafsi.

Tunawaombea familia na wote waliohuswa na msiba huu, Mwenyezi Mungu awape faraja katika kipindi hiki kigumu cha kuomboleza msiba huu mkubwa wa mpendwa wetu.

**Pumzika kwa Amani Mpendwa wetu Ali Mufuruki**

# Bodi ya mikopo yawatoa hofu wanafunzi

**Na Romana Mallya**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imesema ina fedha za kutosha na hadi jana imeshapokea Sh. bilioni 186 kutoka serikalini kwa ajili ya malipo ya miezi mitatu iliyoanzia Oktoba.

Kauli hiyo imekuja ikiwa ni siku moja baada ya Mtandao wa Wanafunzi Tanzania (TSNP) kusema kama serikali haitaingilia kati kuhusu mikopo ya wanafunzi, mamia watashindwa kuendelea na masomo kutokana na kukosa haki hiyo.

Juzi, Katibu wa TSNP, Joseph Malekela, akizungumza na vyombo vya habari, alielezea kuhusu changamoto ambazo wanafunzi wanazipitia kwa sasa huku baadhi wakikosa mikopo na wengine kulipwa kwa kupunjwa.

Baada ya taarifa hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, jana katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, alisema bajeti ya mikopo ya mwaka mzima wa masomo 2019/20 ni Sh. bilioni 450.

"Malipo kwa wanafunzi wote wenye sifa yamepelekwa vyuoni na ndiyo sababu ya utulivu unaoshuhudiwa vyuoni," alisema. Badru alisema hadi jana wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliopata mikopo kwa mwaka wa masomo 2019/20 ni 49,485 ambao wamepata mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 171.8.

"Idadi hii ni sawa na asilimia 74.8 ya jumla ya wanafunzi 66,164 ambao waliomba mikopo kwa usahihi katika taasisi mbalimbali za elimu ya juu," alisema.

Badru alisema kati yao, wanafunzi 698 wamepata mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 2.46 kupitia dirisha la rufaa.

"Kati ya wanafunzi hao 49,485 wa mwaka wa kwanza, wapo jumla ya wanafunzi 9,564 ambao ni yatima, wenye ulemavu ni 397, waliotoka kaya zinazohudumiwa na mpango wa TASAF ni 1,116 na wahitaji wengine 38,408 ambao uhitaji wao tuliothibitika baada ya uchaguzi wa maombi yao ya mkopo," alisema.

Alisema wanafunzi wote waliopata mikopo hadi sasa ni wale waliotimiza vigezo ikiwamo kuambatanisha nyaraka muhimu katika maombi ya msingi na rufaa.

Nyaraka hizo, alisema ni nakala za vyeti vya vifo vya wazazi, barua za madaktari zinazothibitisha ulemavu na barua zinazothibitisha ufadhili.

"Vigezo vingine ni mwanafunzi kuwa na udahili unaotambulika na kwa wanaoendelea na masomo wawe wamefaulu mitihani ya mwisho wa mwaka kuwaruhusu kuendelea na masomo," alisema.

Alisema uthibitisho huo ni muhimu ili kuhakikisha mikopo hiyo inawafikia walengwa tu na ambao waliokamilisha maombi yao kwa kuweka nyaraka sahihi zinazothibitishika na ambazo zitaiwezesha serikali kuwabaini wanufaika wanapomaliza masomo na kuanza kurejesha.

"Lengo la bodi ni kuhakikisha wanafunzi wote wenye sifa na ambao wametimiza vigezo wanapata mikopo kwa kuwa HESLB.

"Bodi ya mikopo inawashauri wanafunzi wote wanaokutana na changamoto mbalimbali vyuoni kuziwasilisha kwa maofisa wanaosimamia madawati ya mikopo vyuoni au menejimenti za vyuo ambao wamekuwa wakiwasiliana na HESLB moja kwa moja na kutatua changamoto hizo," alisema.

Kuhusu waliowasilisha maombi ya rufaa alisema siyo kila aliyewasilisha ombi la rufaa alikuwa na sifa.

"Si kila aliyewasilisha maombi ya rufani alikuwa na sifa. Ni kama uombaji wa mikopo, walioomba katika maombi ya msingi walikuwa 87,636 wakati walioomba vyuo na kupata nafasi za masomo walikuwa 66,154. Wengine hawakuwa na sifa hata za kupata vyuo," alisema.



Washiriki wakimsikiliza aliyekuwa mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Tanzania, Lundovick Utouh, wakati wa ufunguzi wa mkutano wa kuadhimisha siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu Tanzania (LHRC), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Kigogo TRC ahukumiwa kulipa mil. 100/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imemuhukumu kigogo wa zamani wa Shirika la Reli nchini (TRC), Xavier Kundi, kulipa fidia ya Sh. milioni 108.4, baada ya kupatikana na hatia ya wizi akiwa mtumishi wa shirika hilo.

Kadhalika, mahakama hiyo imemhukumu mshtakiwa huyo kifungo cha nje cha miezi sita, kwa masharti ya kutokutenda na kujihusisha na makosa yoyote ya jinai wakati akitumikia adhabu hiyo.

Hukumu hiyo ilisomwa na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally.

Alisema baada ya mshtakiwa kukiri mwenyewe tuhuma zinazomkabili, mahakama yake inamtia hatiani kwa kosa la wizi.

"Mahakama hii inakuhukumu kulipa fidia ya Sh. milioni 108.450 pamoja na kifungo cha nje cha miezi kwa kosa hilo," alisema Hakimu Ally.

Awali upande wa mashtaka ukiongozwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Mashtaka, Maternus Marandu, ulidai kuwa mshtakiwa alimwandikia barua DPP, akiomba kukiri shtaka na kusamehewa.

Marandu alidai kuwa mshtakiwa alikuwa anakabiliwa na mashtaka zaidi ya 14 yakiwamo ya kughushi tiketi za treni, lakini ametiwa hatiani katika shtaka moja la wizi akiwa mtumishi wa shirika hilo.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa katika makubaliano waliyofanyikia kati Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) na mshtakiwa ni pamoja na kulipa fidia ya Sh. milioni 108.450.

Katika kesi hiyo ya jinai namba 338/2018, mshtakiwa huyo anadaiwa kutenda kosa hilo katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma.

Mshtakiwa anadaiwa kati ya mwaka 2018 na 2019, katika mikoa hiyo, alijipatia kiasi cha Sh. 108,450 kwa njia ya wizi wakati akiwa mtumishi.

# Afariki dunia baada ya kusamehewa na Rais

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MMOJA wa wafungwa mkoani Ruvuma, amefariki dunia muda mfupi baada ya Rais John Magufuli kutoa msamaha wa wafungwa wa makosa mbalimbali, akiwamo mfungwa huyo.

Akihutubia maelfu ya wananchi waliojitokeza kwenye Uwanja wa Kirumba jijini Mwanza Jumatatu kuadhimisha miaka 58 ya Uhuru wa Tanganyika, Rais Magufuli alitangaza msamaha kwa wafungwa 5,533 katika magereza mbalimbali nchini.

Akitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, Mkuu wa Jeshi la Magereza wa mkoani hapa, Alexsander Nyefwe, wafungwa 181 katika mkoa huo wamenufaika na msamaha huo wa Rais. Hata hivyo, Nyefwe alisema mmoja wao alifariki dunia siku ambayo msamaha huo ulitolewa na mwingine alishinda kesi kwa rufani kabla ya kupata msamaha huo.

Katika orodha ya wafungwa hao waliopata msahama wa Rais, Nyefwe alisema 39 ni kutoka Gereza la Songea, Kitai 55, Tunduru 26, Mbinga 10, Mkwaya 21 na Majimaji 28.

Kiongozi huyo wa magereza, alitumia nafasi hiyo kumshukuru Rais Magufuli kwa kulipatia jeshi hilo vifaa mbalimbali yakiwamo matrekta kwa ajili ya kilimo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Mndeme, aliwataka wafungwa waliobahatika kupata msamaha wa Rais Magufuli kutorudia kufanya uhalifu.

Aliwataka kutumia mafunzo waliyoyapata wakiwa gerezani, kuendesha shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Gallus Ndunguru, amemshukuru Rais Magufuli kwa kuwapa msamaha na kuahidi kuwa raia wema katika jamii.



# Waliofunguliwa kwa msamaha wapewa ardhi

**Na Neema Hussein,** KATAVI

JUMLA ya wafungwa 74 waliopata msamaha wa Rais wa John Magufuli (pichani), mkoani Katavi wamepatiwa hekari 370 za ardhi ili ziwasaidie kwa kilimo.

Wafungwa 43 ni kutoka Gereza la Mpanda na 31 ni kutoka Gereza la Kalilankulukulu.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera alitoa hekari 5 kwa kila mfungwa jana na kusema wanatakiwa kuzitumia katika shughuli za kilimo, hali itakayowasaidia kujipatia kipato na kuachana na vitendo vya ukiukaji wa sheria.

"Mnatakiwa kumshukru Rais aliyetoa msamaha huu, nami natoa hekari 5 kwa kila mfungwa ni moja ya kuwasaidia msirudie tena kufanya makosa, mkajikite kwenye shughuli za kilimo, najua mtakuta familia zenu zimesambaratika, nendeni mkaanze maisha upya," alisema Homera.

Mmoja wa wafungwa waliopata msamaha huo, Idrissa Ally mkazi wa Wilaya ya Tanganyika ambaye alifungwa kwa kosa la kuiba pikipiki na kukaa jela miezi saba, alishukuru kwa msamaha na eneo la kilimo.

"Nashukuru kwa msaada huo, ama kweli kura yangu lazima nimpe Magufuli, maisha ya gerezani yamenifundisha mambo mengi... nimepata nguvu za kulima, wakati nipo uraiani sikujua gerezani kuna changamoto gani, hakuna uhuru wa kama uraiani," alisema Idrissa.

Maeneo watakayogawiwa ni wilaya za Tanganyika na Nsimbo ambayo serikali ya mkoa wa Katavi inaendelea kuwagawia wananchi.




Dastani Mbam, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kutoa taarifa za watoto juu ya ukatili na utafiti walizofanya katika mkutano ulioandaliwa na Shirika la Save The Children. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri ainyooshea kidole Tarura ujenzi barabara

**Na Neema Hussein,** KATAVI

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Isack Kamwele, amesema barabara nyingi za mkoa wa Katavi zilizo chini ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), zinaharibika haraka kutokana na kujengwa chini ya kiwango.

Akizungumza wakati wa kikao cha 14 cha Bodi ya Barabara mkoani Katavi, alisema na ujenzi wa barabara nyingi unachelewa kukamilika na zinajengwa bila ubunifu, hali inayosababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi.

Kutokana na hali hiyo, ametoa mapendekezo serikalini kupitia wizara yake ili Tarura iwe chini ya Wakala wa Barabara (Tanroads) ndani ya miaka 10, kutokana na kusuasua kwa utekelezaji wa miradi.


"Tarura wamejisahau kutekeleza majukumu yao, kuna miradi ya barabara nyingi zimeanza kujenga muda mrefu, lakini hazikamiliki kwa wakati," alisema Kamwele.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Nsimbo, Rafael Kalinga, alisema ni vyema serikali ikapanga mikakati madhubuti ya kuwaongezea bajeti ya Tarura kuliko kuendelea kuwatupia lawama, kwa sababu tatizo hilo linasababishwa na ufinyu wa bajeti.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa matengenezo ya barabara kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Mratibu wa Tarura mkoa wa Katavi, Zuberi Kilenza, alisema changamoto zinazowakabili ni ufinyu wa bajeti inayotolewa ikilinganishwa na barabara zilizopo na jinsi zilivyoharibika.

"Tuna uhaba wa watumishi katika kada mbalimbali ambapo mahitaji ni watumishi 119 waliopo ni 40, pia kuna upungufu wa magari," alisema Kilenza.

Mkoa wa Katavi bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni Sh.1,800,000,000, huku idadi ya miradi iliyopangwa kutekelezwa na kukamilika ni 17, lakini iliyokamilika ni 11 pekee.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni lazima kujilinda sikukuu zinavyokaribia

**HUU** ni msimu wa sikukuu ambao kila mmoja anafikiria namna ya kujifurahisha, kuburudika na kuifanya familia yake ijisikie vizuri kwa wengine wakati wa Noeli na pia Mwaka Mpya.

Tunapenda kusisitiza kuwa jambo kubwa la kuzingatia wakati huu msimu wa sikukuu unavyokaribia ni usalama na ulinzi wa kila mmoja.

Ni muhimu wakati wote kuwalinda na kuwatunza watoto, wanyonge wakiwamo wahitaji, wazee na wagonjwa hasa wenye matatizo ya akili. Tunayakumbusha haya kwa kurejea taarifa za Jeshi la Polisi zilizotolewa hivi karibuni kuwa kila siku watu wawili wanabakwa jijini Dar es Salaam.

Takwimu hizo zinazoihusu Kanda Maalum ya Dar es Salaam, zinasema ubakaji katika kipindi cha miezi 10 mwaka huu ni visa 719 ni habari mbaya.

Ulawiti umeongeza kutoka visa 259 mwaka jana na kufikia 319 mwaka huu, habari njema ni kupungua wizi wa watoto kutoka matukio 12 hadi saba.

Hata hivyo ni lazima kujilinda na kujiepusha na madhara yanayotokana na matukio ya uhalifu kama hayo. Japo haya ni baadhi yanayozungumzia ukatili wa kijinsia zipo ripoti nyingine kuhusu mauaji, utekaji wa watu na vipigo, ambazo hatukuzitaja. Lengo letu ni kukumbushana kuhusu usalama wa watoto na pia ulinzi wetu na mali pia. Tukumbuke ni wakati ambao wazee na wengine wenye mahitaji maalumu wanapotea. Aidha, watoto nao wanapokwenda kwenye michezo wanaweza wasirejee.

Ni msimu huu wa sikukuu ndiko kwenye hatari hizo. Ni vyema kuwa makini na kuwajali watoto na ndugu wasiojiweza.

Lakini ni msimu wa kupata taarifa za kuokotwa miili ikiwa imetupwa sehemu mbalimbali kwa madai ya ama kuuawa na kuporwa au kuchukuliwa baadhi ya viungo, kudaiwa kulewa kupindukia, kunyweshwa sumu na pia kuuliwa kwenye ugomvi.

Ni vyema kujiepusha na ugomvi. Tunakumbushana kuwa baadhi ya waathirika wakubwa wa mauaji ni madereva wa bodaboda na bajaji pamoja na teksi.

Wasijisahau msimu huu usafiri huhitajika sana, lakini hatari ya kuuawa nayo ni kubwa. Ni vyema kujiepusha na ulevi wa kupindukia na kuwakwepa watu wasiowafahamu au kuwatilia shaka. Pamoja na kuwalinda watoto na wahitaji ni wakati pia wa wanawake kuwa makini na kujali usalama wao kwa vile nyakati za sikukuu ndiko yanakotokea mauaji ya wapenzi hasa kwa kisingizio cha wivu wa mapenzi.

Kwa upande wao tatizo la kuporwa huibuka kwa kasi kubwa, tena linawahusu wanawake na mabinti ambao mara nyingi ni waathirika wa kuibiwa pochi, mifuko na chochote wanachobeba hasa muda wa jioni na usiku.


Ni vyema kuwa makini na kujiepusha kupita maeneo yenye maficho kama vichaka, mapagare, mitaa yenye giza na kwenye sehemu zenye wahalifu hasa vijiwe vya wavuta bangi.

Tunashauri kuwa ulinzi wa mali za nyumbani pia ni jukumu la kila mmoja wakati huu. Ni vizuri kufanga milango na kutunza mifugo hasa kuku, ng'ombe, mbuzi na nguruwe kwa kuwa wengi huiba mali hizo nyakati za sikukuu ili kuuza kitoweo ambacho kinahitajika sana.

Ni vyema pia kukumbushana kuwa huu ndiyo msimu wa kuuziwa kitoweo cha wizi na pia kisicho salama kwani wakati mwingine nyama inaweza kuwa na sumu kutokana na wauzaji kuiba mifugo hasa nguruwe na kuwalisha sumu ili kuwakamata kwa urahisi.

Kwa hiyo ulinzi wa watoto, wasiojiweza, mali kuanzia mifugo na vyombo vya usafiri kama magari, pikipiki na bajaji ni muhimu kuzingatiwa muda wote ili kuepuka kumaliza na kuanza mwaka na majonzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Utafiti, ubunifu wa kidijitali unahitaji kutumia Kiingereza

Na Michael Eneza

**JITIHADA** zinaendelea maeneo mengi kuwajumuisha wanafunzi hasa katika shule za sekondari kutumia mbinu za kupeana habari kimtandao kutoa majawabu ya changamoto tofauti za kijamii na kimasomo.

Yamekuwapo mashindano kuhusiana na ubunifu wa kutumia mitandao na inaonekana wazi kuwa wako wanafunzi wengi wenye vipaji vya hali ya juu katika kufikiria mbinu za kiteknolojia kutatua masuala tofauti ya kiufundi, kuendesha biashara au kuwasiliana kijamii.

Ni eneo ambalo linazidi kupanuka, na fani tofauti tayari zinahusishwa.

Taarifa za hivi karibuni za Taasisi ya Fizikia (Institute of Physics) ya Uingereza inayoshirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kujenga uwezo wa kubuni majawabu ya changamoto tofauti, kuyaunda kibiashara ni moja ya matukio yanayofungua pazia ya nini kinahitajika.

Pale wanafunzi wanapotumia Kiingereza kwa shughuli zote hizo inakuwa rahisi kwa kampuni tofauti za nje zenye umuhimu kiteknolojia au biashara kuanzisha mahusiano katika eneo fulani. Ukiangalia taarifa za matukio tofauti shuleni yanayoendana na suala hilo, uwezo wa kujenga mpangilio wa fikra na kuielezea kwa lugha fasaha inayoendana kwa urahisi na vifaa vya teknolojia na hata mahitaji ya kuundwa hitaji hilo kiufundi, suala la Kiingereza ni muhimu.

Hakuna mahali ambapo matumizi ya Kiingereza yamezuia wanafunzi kuunda ubunifu na kuuweka hadharani au mbele ya majopo ya hapa na pale yanayosimamia shughuli kama hizo.

Cha msingi ni kuwa vijana wanapokuwa wanazungumza Kiingereza kwa ufasaha na kusoma kitabu au jarida kwa lugha hiyo mradi tu inalingana na umri wao na kiwango cha taaluma, wanasonga mbele.

Hali hiyo ina maana kuwa Kiswahili kiendelee kupewa kipaumbele kama njia ya mawasiliano ya jumla, kwa mfano katika mitano ya hadhara na majukwaa mengine yasiyo ya kitaaluma, hasa yale ya siasa, na hata biashara.

Tatizo linakuja pale unapojengwa mkakati wa kuteka eneo lote la mawasiliano, ya kijamii na hata ya kitaaluma iwe kwa lugha ya taifa, kwa kudhania kuwa ina uwezo wa kushindana na lugha za kigeni. Mifano inayotolewa kuhusu suala hilo haigusi lugha za Kiafrika, kama matumizi ya Amharic ya Ethiopia na maandishi yake tata yatasukuma mbele sayansi na teknologia au maandishi rahisi ya Kilatini ndiyo mwelekeo fasaha.

Taasisi hiyo ya Uingereza ilikuwa inapiga chapuo zaidi kuwa ubunifu mpya wa kisayansi unahitji kuelekezwa katika mchakato wa kibiashara ili utoe majawabu stahiki kwa matatizo ya dunia kwa jumla. Ilikuwa ni wakati wa kufunga mafunzo ya STEM, mkakati unaowakilisha dhana ya 'Science, Technology, Engineering and Mathematics'.

Dhana hiyo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati ambayo ikitafsiriwa inakuwa 'STUH', huenda haitaeleweka bila kurudi katika dhana ya msingi ya STEM.

Mara nyingi tafsiri tata za kulazimisha hazieleweki mpaka angalizo litolewe la neno la awali la Kiingereza au hata la Kiswahili, kwa mfano neno 'kongole,' au pongezi ambalo kwa Kiingereza ni 'congratulations,'

Dhana ya STEM iliundwa ili kuzileta pamoja taaluma hizo katika kujenga ubunifu miongoni mwa anafunzi ambao wakati katika ngazi za juu za elimu ya sekondari wanakuwa na masomo hayo kwa pamoja,kwa mfano wengi tu wako katika mchepuo wa PCB au 'physics', 'chemistry' na 'biology', na kwa mwelekeo huu, hakuna haja ya kutafsiri masomo hayo ili yawe 'fizikia, kemia na biolojia' kwani yakifundishwa kwa Kiswahili yataharibu mpangilio mzima wa kuyaelewa.

Jambo muhimu ni kujenga msingi wa Kiingereza katika shule za awali na za msingi, siyo kianze baadaye.

Kuhitaji wanafunzi watumie taaluma hizo katika ubunifu wa kisayansi halafu masomo yao yajikite katika Kiswahili ni kudhania kuwa wahusika wote katika mtiririko wa ufahamu na maongezi kuanzia taasisi kama Institute of Physics na UDSM hadi kufikia shule wajikite katika Kiswahili.

Jinsi maji yanavyotiririka ni kielelezo cha kanuni hiyo, na hata maisha ya kawaida yanaifanana, kuwa ni rahisi kushirikiana na wale ambao hupati taabu ya kuwasiliana au kuelewana nao, si wagomvi.

# Jafo awapa kibarua kizito wakuu wa shule

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amewataka wakuu wa shule nchini kusimamia nidhamu na maadili kwa walimu na wanafunzi kutokana na kukithiri kwa vitendo vya walimu kudaiwa kuwapa mimba wanafunzi wao. Kauli hiyo aliitoa jana wakati alipomwakilisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwenye ufunguzi wa mkutano mkuu wa 14 wa Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania Bara (TAHOSSA), uliofanyika jijini hapa jana.

Aliwataka wakuu wa shule za sekondari kwenda kusimamia nidhamu na maadili kwa walimu wanaowaongoza kwenye maeneo yao kutokana na tabia inayoendelea kujitokeza ya walimu kudaiwa kuwapa mimba wanafunzi wao.

"Nendeni mkadhibiti nidhamu zenu, leo hii kuna walimu wanatembea na wanafunzi wao hii sio sawa, nidhamu hii ianzie kwenu ninyi wakuu wa shule ndipo kwa wale mnaowasimamia," alionya.

"Kama wewe mkuu wa shule unakula vifaranga, walimu wengine si watakula vifaranga na mayai yake? Jambo hilo halipendezi hakikisheni mnasimamia nidhamu," alisema Jafo. Alisema jambo la wanafunzi kuendelea kupewa mimba limekuwa likiwaathiri pamoja na wazazi ambao walikuwa wanawasomesha kwa lengo la kutimiza ndoto za watoto hao.

Aliwataka wakuu hao wa shule nchini kudhibiti utoro wa walimu na wanafunzi kwenye shule zao ili kufikia malengo ya elimu yaliyokusudiwa. Alisema kuna baadhi ya walimu ni watoro hawakai kwenye maeneo yao ya shule na wakitoka nje ya vituo vyao vya kazi bila sababu maalumu.

"Kama mwalimu ni mtoro haingii kwanza atawakosesha watoto vipindi vya masomo na atakuwa anaibia serikali kwa kuchukua mshahara ambao hakustahili, hakikisheni mnasimamia hili pia," alisema.

Waziri Jafo aliongeza kuwa mwakani serikali itatoa ajira kwa walimu 16,000 ili kupunguza changamoto ya upungufu wa walimu katika shule mbalimbali nchini.

Hata hivyo, aliahidi Ofisi ya Rais Tamisemi kuandaa mkutano mkuu wa wakuu wa shule za msingi na sekondari mwakani kwa lengo la kupeana mikakati ya kazi na atamwomba Rais Dk. John Magufuli kuwa mgeni rasmi.

Mwenyekiti wa Tahossa, Vitalis Shija, alisema umoja huo ulianzishwa mwaka 2005 na sasa una wanachama 5,000 na ulianzishwa kwa malengo makuu ya jukwaa la pamoja la kitaaluma la kubadilishana uzoefu na kuendesha shule na kuishauri serikali kuhusu masuala ya elimu nchini.

# Aliyegoma athibitika matatizo afya ya akili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Magereza mkoani Mbeya, limethibitisha kuwa mfungwa Merard Abraham, ambaye aligoma kuondoka gerezani baada ya kutolewa kwa msamaha wa Rais John Magufuli wakati wa sherehe za Uhuru wa Tanzania, ana matatizo ya afya ya akili.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Mkuu wa Jeshi la Magereza wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Magereza, Mathias Mkama, alisema Abraham afya yake ilikuwa inabadilika mara kwa mara.

Alisema pamoja na kuonekana kugoma kuondoka gerezani hapo, lakini ndugu zake walienda kumchukua na kuondoka naye kwenda Mwakaleli, wilayani Rungwe na jeshi hilo liliwasaidia baadhi ya gharama za usafiri. Juzi wakati Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipotembelea Gereza la Ruanga kwa ajili ya kuongea na wafungwa waliopata msamaha wa rais na kuwapa wosia wa kuishi wanaporudi uraiani, mfungwa huyo aligoma kurudi nyumbani na kudai kuwa hana mahali pa kuishi.

Akizungumzia tukio hilo, Mkama alisema awali alienda ndugu yake mmoja kwa ajili ya kumchukua, lakini baada ya kubaini kuwa ni 'mtata' akaamua kuwasiliana na ndugu wengine na hivyo wakaja wengi na wakafanikiwa kumchukua.

"Kwa sababu alikuwa amejijeruhi kwa jiwe kwenye paji la uso, tulilazimika kumtibu kwanza kwenye zahanati yetu na baada ya kuchunguzwa matatizo mengine wataalamu wetu walithibitisha kuwa yuko vizuri na hivyo tukaruhusu aondoke," alisema Mkama.

Alisema wafungwa wote 259 wa walionufaika na msamaha wa rais walishachukuliwa na ndugu zao na kurejea nyumbani baada ya jeshi hilo kuwapatia nauli ya kuwarudisha kila mmoja nyumbani kwao.

Kamanda Mkama alisema Merard alikuwa anasema anataka kurudi katika Gereza la Ukonga jijini Dar es Salaam kwa sababu ndiko alikokuwa amehukumiwa kwenda kwa mara ya kwanza na kwamba alitumikia kifungo kwa mara ya kwanza katika gereza hilo kabla ya kuhamishiwa Mbeya.

Alisema kitendo cha kijana huyo kutamani kubaki gerezani ni haki yake ya kuzungumza ambayo kila Mtanzania anayo kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania na hivyo wasingeweza kumchukulia hatua yoyote kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, alimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, kwa kusimamia urejeshaji wa raia ambao waliachiwa kwa msamaha wa rais katika Magereza ya Ruanda pamoja na Gereza la kimkakati la Kilimo la Songwe.

Rais John Magufuli wakati wa sherehe za kuadhimisha Uhuru wa Tanganyika zilizofanyika katika Mkoa wa Mwanza, alitangaza msamaha kwa wafungwa 5,533 na katika Mkoa wa Mbeya, walinufaika wafungwa 259.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo ( wa tatu kushoto), akifuatiwa na Mwenyeki wa Baraza la Usimamizi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) Dk. Naomi Katunzi, Mkurugenzi wa TEWW, Dk. Michael Ng'umbi (wa tatu kulia) wakiwa katika mahafali ya 55 ya TEWW jijini Dar es Salaaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Kanyasu awaongoza ma-DC kutembelea hifadhi Burigi

**Na Lusungu Helela, CHATO**

WIZARA ya Maliasili na Utalii imeanza mkakati wa kuwatumia wakuu wa wilaya nchini kuhamasisha utalii wa ndani.

Kutokana na hali hiyo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, aliongozana na wakuu wa wilaya saba kwa ajili ya kutembelea Burigi Chato, mkoani Kagera ili kutambua fursa zinazopatikana ndani ya hifadhi hiyo mpya.

Mbali ya kutambua fursa hizo, wakuu wa wilaya hao watatumika pia kuhamasisha wananchi wanaowaongoza katika wilaya watokazo kuhamasisha utalii wa ndani.

Kanyasu alisema utalii ni sekta muhimu katika maendeleo ya nchi, hivyo wakuu wa wilaya wote nchini wapatao 139 ni kundi muhimu katika kuwahamasisha wananchi wanaowaongoza kuhusu umuhimu wa kutembelea hifadhi zilizopo nchini.

Akizungumzia sababu za kuwatumia wakuu wa wilaya hao, Kanyasu alisema mbali na kuwatumia waandishi wa habari, wasanii na watu maarufu, wakuu wa wilaya ni kundi muhimu kwa vile wao ni wenyeviti wa kamati za ulinzi na usalama katika wilaya zao.

"Watalii wanaokuja nchini kutembelea vivutio vya utalii huzingatia ukarimu na usalama wao na wakuu wa wilaya ndio wasimamizi wakuu wa usalama wa watalii na mali zao," alisema.

"Tulianza kuwatumia waandishi wa habari wakafuata wasanii na leo (jana) tumekuja na wakuu wa wilaya. Lengo letu ni kuona jamii inapata mwamko wa kutembelea vivutio vyao wenyewe," alisisitiza.

Naibu Waziri alisema wakuu hao wa wilaya ni viongozi wanaowahakikishia usalama watalii na ndio wenye jukumu la kuhakikisha kila mtalii anayekuja nchini kutembelea vivutio vya utalii analala na kuamka salama.

Kwa upande wake, Damiani Salu, Mkuu wa Hifadhi hiyo alisema ujio wa wakuu hao wa wilaya utasaidia kuchagiza utalii wa ndani kwa vile wao ni viongozi wanaowangoza watu, hivyo watatumia ushawishi wao katika kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kutembelea hifadhi nchini.

Pia aliwaambia wakuu hao kuwa hifadhi hiyo iko katika hatua za mwisho za kuongeza wanyamapori mbalimbali wakiwamo simba wa kutoka familia tano.

Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, aliipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kutumia makundi mbalimbali yenye ushawishi katika jamii katika kuhamasisha utalii wa ndani ambao umekuwa haufanyi vizuri.

Mbali na Kiswaga wakuu wa wilaya wengine waliotembelea hifadhi hiyo na wilaya zao kwenye mabano ni Asia Abdallah (Kilolo), Mwanahamisi Munkunda (Bahi), Jumaa Irando (Momba), Felix Lyaniva (Temeke), Siriel Mchembe (Gairo) na Deogratius Ndejembi (Kongwa).

# TBS yajizatiti kudhibiti bidhaa za kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limesema limejizatiti kuandaa viwango na kudhibiti bidhaa za kilimo na ufugaji, ikiwamo, mbegu, mbolea, viuatilifu, mashine za kulimia na vyakula vya mifugo.

Hayo yalisemwa na Ofisa Viwango wa Shirika hilo, Mwajuma Iddi, wakati wa maonyesho ya Kilimo na Mifugo yaliyofanyika Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) mkoani Morogoro.

Idd alisema shirika hilo ndiyo taasisi pekee ya kuandaa viwango na kudhibiti usalama na ubora wa bidhaa nchini, hivyo wamejizatiti kuandaa viwango na kudhibiti bidhaa za kilimo na ufugaji.

Alifafanua kwamba shirika hilo huandaa viwango kupitia kamati zake za kitaalamu zinazojumuisha wadau muhimu katika sekta husika, wakiwamo, wahadhiri wa vyuo vikuu, wazalishaji, wafanyabiashara, wadhibiti, watumiaji, wizara husika, wasindikaji na wengine.

Katika kutimiza majukumu hayo, Idd alisema TBS ina kamati tano katika sekta ya kilimo na ufugaji. Alitaja kamati hizo kuwa ni ya mbolea (AFDC 10), viuatilifu na vichafuzi katika vyakula na kilimo (AFDC 27) na Kamati ya mbegu (AFDC 30).

Nyingine kwa mujibu wa Idd ni ya mashine za kilimo (GDTC 5) na ya vyakula vya wanyama (AFDC 9).

"TBS pia ina kamati zingine za vyakula vitokanavyo na kilimo na mifugo (ufugaji) zenye lengo la kutengeneza viwango za bidhaa hizo," alisema na kuongeza:

"Katika mchakato wa kutengeneza viwango, wadau wote na jamii kwa ujumla hushirikishwa kupitia rasimu ya viwango "Draft Tanzania Standard for public comments", kiwango hutumwa kwa wadau na jamii kupitia tovuti ya shirika na barua pepe kwa wadau, wizara na tunapeleka na kuwataarifu Shirika la Biashara Duniani (WTO) ili waweze kuvitumа viwango vyetu katika nchi zingine zitoe maoni yao visije kuleta vikwazo katika biashara katika utekelezaji viwango hivyo.

Alisema TBS pia hushirikiana na taasisi zingine kudhibiti bidhaa katika kilimo na mifugo kama vile TPRI, TOSCI na nyingine lengo likiwa ni kuleta ufanisi katika kudhibiti ubora na usalama wa bidhaa katika kilimo na mifugo.

Kwa upande wake Ofisa Masoko wa TBS, Rhoda Mayugu, aliwataka wadau wa sekta ya kilimo na mifugo kujitokeza kushiriki katika uandaaji wa viwango vinavyohusiana na maeneo hayo.




Meneja wa Wakala wa Barabara (Tanroads) Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Marwa Ruirya, akitoa maelezo ya mradi wa ujenzi wa daraja la Kigongo - Busisi walipotembelewa na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa CCM wakiongozwa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi, Humphrey Polepole, mradi huo unajengwa na mkandarasi wa China Civil Engineering Construction Cooperation kwa fedha ya serikali Sh. bilioni 699.2. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

## Mfungwa aliyesamehewa adaiwa kuiba

**INATOKA UK. 3**

alisema.

Kamanda Issa alisema mfungwa huyo aliwaeleza kuwa baada ya kwenda mtaani na kukosa kwa kwenda kwa sababu hana maelewano mazuri na baba yake, aliendelea kurandaranda huko. "Ameeleza kuwa baada ya kurandaranda mtaani na kukosa kwa kwenda, ilipofika saa 9:00 usiku, aliingiwa na tamaa akaamua kwenda kwenye hiyo nyumba ya kulala wageni ili kuiba," alisema.

Kamanda Issa alisema baada ya kufika hapo, alichungulia na kuona watu wamelala ndipo alipovunja na alipoingia ndani, alimwona mmoja wa wanawake waliokuwamo akiwa na fedha.

"Alipoziona hizo fedha na akiwa katika harakati za kwenda kuziiba, ndipo waliolala waliposhtuka na yeye katika kujihami aliwataka wajifunike sura zao kwa nguo walizokuwa wamejifunikia.

"Ndani ya nyumba hiyo ya kulala wageni kulikuwa na wahudumu, walinzi na baadhi ya wageni ambao walipiga kelele na kupata msaada kutoka kwa majirani ambao walifika hapo na kumkamata kisha kumpiga," alisema.

Katika tukio hilo, alisema Msolwa alijeruhiwa kwa panga eneo la kichwani na jana alipelekwa hospitalini kwa matibabu.

Alisema katika msamaha huo wa Rais Magufuli aliachiwa akiwa na kosa la uvunjaji ambalo ndilo alilolirudia baada ya kuachiwa huru.

# Wengi watinga kwa mkemia kujua uhalali baba wa mtoto

**INATOKA UK. 2**

kutoka kwenye mazingira ya nje, zingine ni vinasaba ili kuangalia uhalali wa baba wa mtoto, pia kuangalia sumu," alisema.

Aliongeza kuwa kanda hiyo inahudumia mikoa mitano ya Dodoma, Iringa, Morogoro, Singida na Tabora, akieleza kuwa kumekuwapo mafanikio makubwa tangu kuanzishwa kwake.

"Tunashukuru serikali ya awamu ya tano kuanzisha hii kanda kwa kuwa tumejionea mafanikio mengi ikiwa ni pamoja na kukagua maeneo 360 ambayo yanajihusisha na masuala ya kemikali," alisema.

Meneja huyo alisema katika ukaguzi huo wamebaini upungufu mbalimbali na kutoa elimu kwenye mambo waliyoyakuta ikiwamo utunzaji na kuweka miundombinu sahihi ya kemikali.

Kuhusu utoaji vibali vya kusafirisha kemikali, Kuzumila alisema kwa kipindi hicho wametoa vibali 139 vya kuingiza na kusafirisha kemikali kwenye maeneo mbalimbali nchini. Kuzumila aliweka wazi kuwa ifikapo mwaka 2028, serikali itapiga marufuku matumizi ya zebaki nchini.

"Bunge limeshapitisha mkataba ambao unazuia matumizi ya kemikali ya zebaki, inayotumika sana kwa wachenjuaji wadogo wa madini, kuna madhara makubwa na mkakati uliopo ni kutoa elimu ili kujua madhara na namna ya kutumia kabla ya kipindi cha kupiga marufuku, na ifikapo 2028 tutapiga marufuku," alisema.

Alieleza kuwa kinachofanyika kwa sasa ni kutoa elimu ya kemikali mbadala na kuwa na miundombinu ambayo haitaruhusu kusambaa kwa kemikali kwenye mazingira.

# ACT-Wazalendo yaitega Tume Haki za Binadamu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimewataka watendaji wa Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuzifahamu haki za raia zilizoainishwa katika Katiba ya Zanzibar.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ya chama hicho, Omar Said Shaaban, wakati akielezea maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu nchini pamoja na hali ya haki za binaadamu ilivyo kwa upande wa Zanzibar.

Alisema wananchi wengi haki zao za msingi zinavunjwa kwa sababu mbalimbali ikiwamo wengine kutokuzifahamu haki hizo ambazo zimetajwa katika katiba za nchi.

Alisema kazi za tume ni kutoa elimu kwa umma kuhusu kazi zake na majukumu ili wananchi wawe na elimu pana kuhusu fursa wanazostahili kuzipata.

"Wakati tukiadhimisha Siku ya Haki za Binadamu nchini, tunaiomba Tume kutoa elimu zaidi kwa makundi mbalimbali ili kuzifahamu haki hizo ambazo kwa bahati mbaya jamii yetu haina uelewa mpana," alisema.

Alisema wakati serikali zote mbili zikifanya kazi kubwa ya kuimarisha utawala bora, bado zipo taasisi zinazoshughulikia na haki hizo zikirudisha nyuma juhudi hizo likiwamo Jeshi la Polisi.

Alisema ukienda katika mahakama na kuangalia mashauri yanayowakabili wananchi, bado lipo tatizo la ubambikizaji wa kesi unaofanywa na Jeshi la Polisi ambalo limepewa majukumu ya kufanya upelelezi na kukamata raia wanaotuhumiwa kufanya makosa.

"Tumefanikiwa katika kuimarisha utawala bora na haki za binadamu, lakini bado Jeshi la Polisi linatakiwa kuangaliwa zaidi majukumu yake makubwa liliyopewa kwa mujibu wa katiba... tatizo la ubambikizaji wa kesi kwa raia bado lipo," alisema.

Aidha, alisema hatua ya serikali ya Tanzania kujiondoa katika kifungu cha 34 (6) inachowawezesha raia na mashirika yasiyo kuwa ya kiserikali kuishtaki serikali katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binaadamu, ni kuwanyamazisha wanaharakati wa haki za binadamu.

Alisema hatua hiyo inarudisha taifa nyuma katika mapambano ya kulinda, kutetea, na kudumisha haki za binadamu.

Chama hicho kimetoa rai kwa wabunge wa Tanzania bila kujali itikadi zao za kisiasa kuihoji serikali juu ya hatua hiyo waliochukua bila kupata ridhaa ya bunge kama liliridhia itifaki.

Tanzania itakuwa ni nchi ya pili kujitoa katika kifungu hicho cha 34(6) ikitanguliwa na Rwanda.



Mkazi wa Tabata Dampo akipita karibu na takataka zilizotelekezwa barabarani na kusababisha usumbufu kwa wenye magari na watembea kwa miguu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Wadau wafagilia maboresho bandarini

**Na Elizabeth Zaya,** MWANZA

WADAU wanaotumia bandari kusafirisha mizigo wamesema maboresho yanayofanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), katika bandari mbalimbali nchini yamesaidia kurahisisha shughuli za usafirishaji na kupunguza gharama.

Wakizungumza na waandishi wa habari katika Bandari ya Mwanza jijini humo, walisema mbali na kupunguza gharama, lakini yamesaidia kupunguza mlolongo uliokuwa unachangia kutumia muda mwingi katika usafirishaji wa mizigo bandarini.

Mahsen Omar kutoka Kampuni ya GSM, alisema kipindi cha nyuma kabla ya kuanza maboresho katika bandari hizo, walikuwa wakitumia muda mrefu kusafirisha mizigo bandarini na hivyo kusababisha gharama kubwa za usafirishaji wa mizigo hiyo, lakini tatizo hilo kwa sasa halipo.

"Kutokana na shughuli mbalimbali za kibiashara ambazo tunafanya kila siku, huwa tunatumia bandari kupitisha mizigo, lakini kipindi cha nyuma tulikuwa tunapata tabu sana kwa sababu ya mlolongo mkubwa uliokuwapo, lakini kwa sasa kuna nafuu kubwa," alisema Omar.

Alisema kwa sasa watakuwa na fursa kubwa ya kuendeleza biashara zao bila vikwazo.

Alisema wanaamini kupitia maboresho hayo na jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali upo uwezekano mkubwa wa kufikia uchumi wa kati

Kaimu wa Usafirishaji kutoka Shirika la Reli Tanzania (TRC), Lawrence Semanini, alisema kama wadau muhimu katika sekta ya usafirishaji, maboresho hayo yanayofanywa na TPA katika bandari mbalimbali nchini, yamewaongezea nguvu na kasi ya kufanya biashara.

Semanini alitoa wito kwa wafanyabiashara ambao waliacha kutumia bandari katokana na changamoto zilizokuwapo kipindi cha nyuma kuanza kutumia.

## Kesi 20 za madai talaka kwa miezi 2

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JUMLA ya kesi 20 za madai ya talaka zimeripotiwa katika Mahakama ya Kadhi Wilaya ya Wete kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu.

Akitoa taarifa katika Kamati ya Kupinga Udhalilishaji ya Wilaya katika mkutano wa kuwasilisha ripoti ya miezi mitatu iliyoandaliwa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa-Zanzibar), Khamis Juma Mohamed kutoka Mahakama ya Kadhi Wete, alisema jumla ya kesi 28 zilifunguliwa katika Mahakama hiyo, zikiwamo 20 za talaka na kesi nane za matukio mengine.

Alisema kati ya kesi hizo 20 za talaka, 10 zimeshatolewa maamuzi ya talaka na mahakama na kesi nyengine 10 zinaendelea kusikilizwa.

"Kesi nyingine ni huduma za watoto tatu, mirathi tau, idhini moja na kudai mke moja," alisema.

Khamis alieleza kuwa jambo la kusikitisha wakati zinapofikishwa kesi hizo ni kwamba wanawake hudai talaka wenyewe, jambo ambalo linasababisha watoto kusumbuka na kusambaratika, hivyo kukosa elimu na malezi mazuri.

"Wanapokuja mahakamani kudai talaka huahidi kuwa watoto watawashughulikia wenyewe, lakini wakishaachika tu wanatuletea kesi nyingine ya kudai huduma kwa mtalaka wake, hili linatukwaza sana," alieleza. Akielezea chanzo cha kesi hizo, alisema ni jamii kukosa elimu ya ndoa, hivyo wanandoa wanahitaji taaluma kubwa kabla ya ndoa jambo ambalo litasaidia kudumu na kupunguza wimbi la talaka.

Seif Sharif Khamis, kutoka Jumuiya ya Maimamu Mkoa wa Kaskazini Pemba, alisema wazazi wanachangia talaka kwa watoto wao kwa kuwaweka karibu zaidi kabla ya ndoa, jambo ambalo ni kinyume cha dini ya Kiislamu. "Baada ya kutolewa posa tu, wazazi tunawaweka pamoja watoto wale wanaotarajia kufunga ndoa muda wote, hapa lazima heshima inapotea, hivyo kusababisha kuwapo kwa talaka za ovyo," alifahamisha.

Aliwaomba wazazi na walezi kuacha tabia ya kuwaweka karibu wanandoa watarajiwa, kwani hilo linachangia ongezeko la talaka, na baada yake wapewe elimu ya ndoa ili waishi kwa amani.

Kwa upande wake, Ofisa wa Wanawake na Watoto Wilaya ya Wete, Siti Suleiman Juma, alisema elimu inahitajika katika jamii ili kuhakikisha wanadhiditi vitendo vya udhalilishaji vilivyokithiri.

Mratibu wa TAMWA Pemba, Fathiya Mussa Said, alisema talaka ni chanzo kikuu cha udhalilishaji wa watoto, hivyo ipo haja ya kutafuta njia mbadala ya kuzuia talaka zisizokuwa na ulazima, ili kuwakinga watoto dhidi ya vitendo viovu.

"Wazazi wanapoachana watoto hukosa huduma na matunzo bora, hivyo huacha shule na madrasa na hatimaye kwenda kujitafutia huduma za chakula wenyewe, jambo ambalo huwasababishia kudhalilishwa," alisema.

## Tanroads Katavi yajipanga kwa ujenzi barabara

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

WAKALA wa Barabara (Tanroads) mkoani Katavi, umepokea Sh. bilioni 3.704 hadi Novemba 30, ambayo ni sawa na asilimia 28 ya bajeti ya mkoa huo kwa mwaka wa fedha 2019/ 2020 kwa ajili ya matengenezo ya barabara kutoka Mfuko wa Barabara.

Wakala huo Mkoa wa Katavi pia wamepokea Sh. milioni 3.704 fedha ambazo ni za maendeleo.

Kaimu Meneja wa Tanroads Mkoa wa Katavi, Mhandisi Martin Mwakabende, alisema hayo wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa matengenezo ya barabara kwa mwaka wa fedha 2019/ 2020 kwenye kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Katavi na kuongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera.

Alisema Tanroads Mkoa wa Katavi imetengewa jumla ya Sh. bilioni 15 kwa mwaka wa fedha 2019/ 2020 kwa ajili ya matengenezo ya barabara na ukarabati, huku Sh. bilioni 14 ni fedha kutoka Mfuko wa Barabara na Sh. bilioni 1.5 ni fedha za maendeleo ambapo Novemba 30, mwaka huu walikuwa wamepokea Sh. bilioni 3.704 sawa na asilimia 28.

Katika utekelezaji wa matengenezo ya barabara kwa msimu huu, Tanroads umesaini mikataba na makandarasi 28 ambao wapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na wamefikia asilimia 25, na hii imesababishwa na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha katika mkoa huo.

Kuhusu miradi inayotekelezwa kitaifa kwa kiwango cha lami katika mkoa wa Katavi ni barabara ya Mpanda -Vikonge yenye urefu wa kilomita 37.65, na mkataba wa ujenzi wa ulisainiwa mwaka 2017 kati ya ofisa mtendaji mkuu wa Tanroads na Kampuni ya M/s China Railway Seventh Group Corporation Ltd kwa gharama ya Sh. bilioni 57 na mradi huo utekelezaji wake upo katika asilimia 88.10 na kilomita 30 zimeshajengwa kwa kiwango cha lami.

Ujenzi mwingine ameutaja kuwa ni barabara ya Tabora - Mpanda mkoani Katavi ambayo imegawanywa kwa makandarasi watatu wa kampuni za China, ambapo kila kampuni itatengeneza kilomita 108 ambapo ujenzi wa barabara hiyo ulianza Aprili mwaka jana na utakamilika Aprili mwakani.

Mwakabende alitaja baadhi ya changamoto katika utekelezaji wa kazi ni utaratibu wa kupata msamaha wa kodi kwa vifaa vya ujenzi unachukua muda mrefu, hivyo kuchelewesha utekelezaji wa matengenezo ya barabara.

Nyingine ni watu kupitisha mifugo barabarani, hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa barabara, fedha zinazotolewa kwa ajili ya maendeleo kutokidhi mahitaji halisi ya ukarabati wa barabara.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isaack Kamwelwe, alisema alipenda Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (Tarura) kuwa chini ya usimamizi wa Tanroads walau kwa miaka kumi kwa kuwa hawana ubunifu.

# Wabadili jengo la watumishi kuwa wodi

**Na Neema Emmanuel,** MISUNGWI

WANANCHI wa Kijiji cha Nhundulu wilayani Misungwi mkoani Mwanza, wamebadili matumizi ya jengo la watumishi kuwa wodi ya kinamama na mtoto ili kunusuru vifo vitokanavyo na uzazi pamoja na kuondoa changamoto ya wazazi kujifungulia nyumbani kutokana na kituo hicho kutokuwa na mazingira rafiki.

Akitoa taarifa ya utekelezaji mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto Kata ya Nhundulu, Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Mwawile, Consolatha Simba, alisema zahanati hiyo inapokea na kuhudumia wagonjwa wasiopungua 50 hadi 60 kwa siku, huku ikihudumia vijiji vya jirani kama Ibinza, Isenengeja, Mhangu, Izizimba, Shinyanga Vijijini na Kwimba, hivyo kusababisha wagonjwa kuwa wengi.

Alisema wananchi waliamua kubadili matumizi ya nyumba ya watumishi kuwa wodi ya mama na watoto baada ya kupata elimu ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto pamoja na ujenzi wa nyumba bora kupitia kamati za Mtakuwwa ambapo jengo hilo linalikadiliwa kugharimu Sh. 51,700,000 mpaka sasa nguvu ya wananchi ni Sh. 13,387,000, na kwamba hadi kufikia ukamilishaji wa jengo hilo linahitaji Sh. 38,313,000 nje ya vifaa tiba.

Aliongeza kuwa kwa siku wanawake watatu hadi sita wanajifungua, idadi inayopelekea wengine kukosa sehemu ya kupumzika baada na kabla ya kujifungua na kufikia hatua ya kulala chini kutokana na upungufu wa vitanda.

Alisema jengo hilo itakamilika litaondoa changamoto ya vifo vya wajawazito na watoto wakati wa kujifungua, kufanikisha utolewaji wa huduma bora kwa watakaofika katika kituo hicho kupata huduma.

Naye Katibu Tawala Wilaya ya Misungwi, Peter Sabato, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya hiyo alitoa shukrani kwa Shirika la Kivulini ambalo limesaidia kupambana na ukatili, hivyo aliomba ushirikiano huu uendelee na endapo zahanati hiyo ikikamilika na vifaa tiba vikiwapo vitasaidia upatikanaji wa huduma nzuri itakayookoa maisha ya kinamama.

Naye Mkurugenzi wa Kivulini, Ali Yassin, alisema shirika linajikita katika kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto ili kuwe na taifa lenye amani, furaha na usawa.

Akifunga kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia kwa mwaka huu sambamba na kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa jengo hilo ikiwa ni ishara ya utekelezaji wa jitihada za kumkomboa mwanamke, Naibu Mkuu wa Shirika la Maendeleo la Ireland, Adrian Fitzgerald, alisema, mwanamke yoyote hatakiwi kufa wakati wa uzazi, hivyo ataungana na juhudi ya wananchi kukamilisha ujenzi huo ili kunusuru vifo vya kuboresha afya ya mama na mtoto.

Magreth Maganga na Aleti Revocutus, wananchi waliozungumzia adha waliokuwa wakipata walisema changamoto walizonazo ni nyingi hasa ya ukosefu wa vyumba vya kupumzika, vitanda na nyumba za watumishi kitu ambacho ni hatari kwani watumishi wote wanakaa mbali ya zahanati.



Mkaguzi wa Hesabu za Ndani wa Benki ya Biashara ya DCB, Samwel Stephano (kulia), akionyesha tuzo ya mshindi wa kwanza katika kitengo cha benki ndogo na za kati ya Mwasilishi Bora wa Hesabu zinazotolewa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu (NBAA) baada ya kukabidhiwa katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa DCB, Nelson Swai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Udumavu Mtwara bado tatizo kubwa

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

HALMASHAURI za Mkoa wa Mtwara na maeneo mengine kote nchini zimehimizwa kutenga bajeti kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ya ndani, ili kutekeleza afua za lishe kwa lengo la kupunguza kiwango cha matatizo ya udumavu na utapiamlo kwa watoto chini ya miaka mitano.

Mkoa wa Mtwara unakabiliwa na tatizo la kiwango cha juu cha tatizo la udumavu ambapo asilimia 29.6, kiwango ambacho bado ni kikubwa.

Hayo yalisemwa wilayani Masasi na ofisa lishe kutoka Ofisi ya Rais - Tamisemi, Festo Tilia, wakati wa kikao cha kuijengea uwezo kamati ya lishe Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Lengo la awali la mipango na bajeti katika mamlaka ya serikali za mitaa ni kuwajengea uwezo kamati za usimamizi wa masuala ya afua za lishe kwa wilaya na mikoa. Alisema kamati hizo zikishajengewa uwezo zitaweza kubaini changamoto za afua za lishe kwenye maeneo yao kisha kuziingiza kwenye mipango na vipaumbele vyao kwa ajili ya utekelezaji kupitia bajeti zao.

Alisema katika mkoa wa Mtwara kiwango cha udumavu kipo kwa asilimia 29.6, ambapo kiwango hicho ni kikubwa na lazima wadau wa afua za lishe zishirikiane na serikali katika kupunguza tatizo hilo.

Tilia alisema kwa ujumla hali ya udumavu nchini bado iko juu ambapo kiwango cha udumavu kwa sasa ni asilimia 31.8, na kwamba lazima halmashauri zitenge hiyo bajeti kwa ajili ya kupambana na tatizo hilo.

Alisema juhudi za kukabiliana na kutatua changamoto za afua za lishe zinahitajika ili kuboresha ustawi wa afya za watoto na jamii kwa ujumla.

"Halmashauri inatakiwa kutekeleza baadhi ya viasharia mbalimbali vya afua za lishe na moja kati ya viasharia ni pamoja na kutenga na kutoa bajeti ili kutekeleza afua hizi za lishe kwenye maeneo yao," alisema Tilia.

Naye ofisa lishe mkoa wa Mtwara, Helieth Kupuyo, alisema Mkoa wa Mtwara unaendelea kupambana na kutatua changamoto za afua za lishe katika mkoa huo.

Alisema kwa miaka ya 2015/ 2016 ilionyesha kuwa katika mkoa wa Mtwara kulikuwa na hali ya udumavu zaidi ya asilimia 30, lakini kwa sasa hali hiyo imeendelea kupungua siku hadi siku.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selena Mzee, alisema kamati hiyo ihakikishe inaendelea kutatua changamoto za afua za lishe.

# ‘Utafiti uguse matatizo yanayoisibu jamii’

**Na Allan Isack,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Willium ole Nasha, ametaka utafiti unaofanywa nchini uguse na matatizo halisi yanayoikabili jamii.

Alitoa rai hiyo wakati akifungua mkutano wa 10 wa watafiti 300, kutoka nchi 36 za mataifa mbalimbali duniani uliofanyika katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST), jijini hapa.

Alisema serikali ya awamu ya tano imejikita kwenye ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda na kwamba utafiti unaofanyika ujikite kwenye maeneo ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kutatua matatizo yaliyopo kwenye jamii kwa lengo la kutengeneza bidhaa na huduma zinazoendana na mahitaji ya watu ulimwenguni.

“Utafiti tuliofanya ujikite katika matatizo ya wananchi, pia tuandae agenda za utafiti huo kulingana na mahitaji,” alisema Ole Nasha.

Rais wa Jumuiya ya watafiti katika malighafi, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela, Prof. Hulda Swai, alisema mkutano huo, umeainisha na kujadili mambo mbalimbali kwa kuzingatia vipaumbele vya utafiti ambao utatumiwa na vyuo vikuu na taasisi za kitafiti.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, alitoa rai kwa wajumbe wa Jumuiya ya watafiti katika malighafi (AMRS), kuja na suluhisho la namna bora ya kutumia vizuri utajiri wa malighafi zilizopo kwa ajili ya maendeleo ya Afrika.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Emmanuel Luoga, alisema kufanyika kwa mkutano huo chuoni hapo ni moja ya mambo muhimu katika kukuza na kukijengea uwezo kufanya utafiti utakazokidhi mahitaji ya kitafifa.

“Wote mnafahamu kuwa chuo hiki kina hadhi ya kimataifa, hivyo wageni wanapokuja kwa ajili ya majadiliano yao wanatusaidia kuongeza ujuzi mpya katika masuala ya utafiti ikiwa ni pamoja na kukuza ushirikiano baina ya taasisi zetu,” alisema Luoga.

Mkutano huo ulioanza Desemba 10, unafanyika kwa siku nne ikiwa ni mara ya pili kufanyika nchini tangu ulipoanzishwa mwaka 2000.

# Viongozi wa vijiji waonywa uuzaji ardhi

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Mhandisi Zephania Chaula, amewataka wenyeviti wapya wa vijiji na vitongoji, kutouza ardhi kwa tamaa zao na watakaobainika atawachukulia hatua kali.

Chaula alitoa onyo hilo juzi wakati wa kuapishwa wenyeviti na wajumbe wa serikali za kata za Terrat, Oljoro namba 5 na Komolo zilizopo Tarafa ya Terrat.

Alisema baadhi ya wenyeviti hao, wapo mstari wa mbele kujali maslahi yao, ikiwamo kuuza ardhi ili kujinufaisha.

Mkuu huyo wa wilaya alisema migogoro mingi ya ardhi inasababishwa na baadhi ya wenyeviti wa vitongoji na vijiji kutokana na mazoea ya kuuza ardhi bila kufuata utaratibu wa kisheria.

“Mmeapishwa ili mkatimize wajibu wenu ipasavyo, na kiongozi yeyote atakayekiuka kiapo chake alichokiapa mwisho wake ni kwenda jela ili iwe funzo kwa wengine,” alisema Chaula.

Alisema amebaini migogoro mingi ya ardhi inasababishwa na baadhi ya viongozi wenye tamaa ya kuuza ardhi, na kwamba atakabiliana na tatizo hilo kwa usimamizi makini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, alisema viongozi hao, wanapaswa kutekeleza majukumu yao ili wasiingilie kwenye migogoro hiyo.

Myenzi alisema baadhi ya wenyeviti wa vitongoji wanakaribishwa kwenye vikao vya maendeleo ya kata na kutoa uamuzi wakati hawapaswi kufanya hivyo.

“Mwenyekiti wa kitongoji siyo mjumbe wa kikao hicho, mtendaji wa kata unapaswa kutambua wajumbe wako ni wenyeviti wa vijiji na ndiyo wenye uamuzi na kupiga kura siyo wenyeviti wa vitongoji,” alisema.

Alisema miaka iliyopita kuna muhtasari uliandikwa kuwa wajumbe wa kamati hiyo, ni pamoja na wenyeviti wa vitongoji jambo ambalo siyo sahihi kwa kuwa viongozi hao, ni waalikwa na jukumu lao ni kutoa maoni na ushauri siyo uamuzi.

Diwani wa kata ya Terrat, Jackson Ole Materi, aliwapongeza wenyeviti hao, kuchaguliwa kushika nafasi hizo, na aliwaahidi kuwapa ushirikiano katika hatua ya kuwatumikia wananchi.

Ole Materi alisema uchaguzi umeshafanyika na umemalizika kilichobaki ni kazi ya kuwatumikia wananchi kwa kutekeleza yote waliyoahidi na kuyasimamia.




Mteja akiwa anachagua kofia kwa ajili ya kuvaa ili mvua isimnyeshee, katika eneo la Anex. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Hamasa elimu ya ufundi yahitajika

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZAZI na walezi wametakiwa kutoa hamasa kwa watoto kujifunza elimu ya ufundi ili kuendeleza vipaji vitakavyowasaidia kuajiriwa na kujiajiri wakati watakapohitimu mafunzo yao.

Rai hiyo, ilitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Chuo cha Ufundi cha Help to Self Help, kilichopo jijini Arusha, Amani Golugwa, katika mahafali ya 20, na wanafunzi 93, waliohitimu kozi mbalimbali za ufundi. Alisema chuo hicho, kinatoa kozi mbalimbali za ufundi kwa wanafunzi hao, na wamewaanda kitaaluma kukabiliana na soko la ajira kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo watakapohitimu mafunzo hayo. Golugwa aliwataka wazazi kuwahamasisha watoto kujiunga na elimu ya ufundi ambayo itawawezesha kujiajiri kwa haraka na kuondokana na tatizo la kusaka ajira baada ya kuhitimu mafunzo.

Alisema tangu kuanza kwa chuo hicho, mwaka 1993, zaidi ya vijana 5,000, wamejiajiri na kufungua shughuli mbalimbali za kiufundi ndani na nje ya nchi.

“Pamoja na mafanikio tuliyonayo bado chuo chetu kinakabiliwa na tatizo la wazazi kutowalipa ada wanafunzi kwa wakati kwa kuwa vijana wengi wanashauku ya kujiendeleza, lakini tatizo limejitokeza kutokana na umuhimu wa kuwekeza kwenye elimu,” alisema Golugwa.Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Help to Self Help, Mchungaji Peter Golugwa, aliwataka wazazi kuongeza bidii ya kusomesha watoto wao, hususani kuwapa elimu ya ufundi ili waweze kujitegemea na kuondokana na tatiazo la kuwa tegemezi katika jamii.

Aliwataka wahitimu hao, kujiendeleza zaidi kwa kuwa elimu waliyoipata haitoshelezi mahitaji yao, pia aliwasisitiza kuitumia elimu hiyo, kuwa chachu ya mabadiliko katika jamii pamoja na kuwasaidia vijana wengine.

Mkuu wa chuo hicho, Eliza Kiwia, alisema chuo kimeanzisha kozi fupi ya umeme wa jua ambayo kwa mwaka 2019, waliohitimu daraja la kwanza wamepewa nafasi ya kusoma kozi hiyo, bure kwa udhamini wa chuo hicho.

Alitoa wito kwa wazazi na walezi kupeleka watoto kupata elimu ili waweze kujifunza zaidi kwa vitendo.

Eliza alisema chuo hicho, kina mpango mkakati wa kujenga maktaba ya kisasa na bweni ili kupunguza gharama za kukodisha mabweni. Mmoja wa wahitimu wa kozi ya umeme, Diana Dickson, alisema chuo hicho, kimewaandaa katika fani ya ufundi kwa vitendo zaidi, ikiwamo kozi za ushonaji, upishi, uhudumu, mapokezi ya wageni, ufundi umeme wa majumbani na wa nishati ya jua.

# Walalamikia bei ndogo ya kahawa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WADAU wa kahawa nchini, wasema bei ndogo ya zao hilo katika soko la dunia hasa ile inayostawishwa Tanzania ni moja ya mambo yanayokwamisha jitihada za serikali kufufua kasi ya uzalishaji wake.

Pia mabadiliko ya tabia nchi nayo yanatajwa kuwa moja ya matatizo ambayo linaikabili sekta hiyo kwa sasa.

Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Wadau wa Kahawa Tanzania, Noel Yatera, alieleza hayo jana juu ya mtazamo wao kuhusu maendeleo ya zao hilo.

Kwa mujibu wa Yatera, zinahitajika jitihada za makusudi kuhakikisha wakulima wanapata masoko ya uhakika na bei nzuri ya kahawa licha ya kuwapo kwa matatizo hayo.

Alisema kwa miaka mitatu sasa, bei ya kahawa nje ya nchi imeshuka kwa zaidi ya asilimia 30.

Makamu Mwenyekiti huyo ameeleza kuwa hali hiyo ndiyo inayochangia kupungua kipato cha wakulima na kufanya wengi kukumbia kilimo hicho, huku uzalishaji ukiendelea kuwa wastani wa tani 50 kwa mwaka.

"Asilimia zaidi ya 90 ya kahawa inayozalishwa nchini, inategemea soko la nje, hivyo kuporomoka kwa bei ni kikwazo kikubwa kwa wakulima, na kumefanya wengi kukata tamaa ya kuendelea na kilimo hichi, na hiki ni kikwazo katika kuongeza uzalishaji wa zao hilo," alisema Yatera.

Pia alisema changamoto nyingine inayoikabili sekta hiyo ni mabadiliko ya mara kwa mara ya sera zinazotawala tasnia ya kahawa, jambo ambalo limekuwa likiwaathiri wawekezaji.

"Kumekuwa na mabadiliko mengi ya sera na yamesababisha, wawekezaji katika tasnia ya kahawa kuathirika na kuvuruga mpango wao na wengine kujikuta wakifunga kampuni zao za kahawa," alisema.

# Waeleza kasoro fomu za madaktari kuhusu ubakaji

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MJADALA umeibuka kuhusu maelezo yanayotolewa na kujazwa na madaktari kwenye fomu namba tatu ya Polisi (PF3), hasa yale yanayohusiana na vipimo vya uchunguzi wa matukio ya ulawiti na ubakaji kuwa yanaingilia utoaji wa haki mahakamani.

Jana, mahakimu wawili ambao ni Hakimu Mkazi Mfawidhi Moshi, Bernazitha Maziku na Hakimu Mkazi Julieth Mawole, walijikuta wakieleza namna mahakimu wanavyopata ugumu kutokana na majibu ya madaktari katika ujazaji wa fomu hiyo katika kesi hizo.

Walikuwa wakizungumza katika mafunzo yanayoendelea mjini hapa kuhusu shughuli za uendeshaji wa vituo vya huduma jumuishi kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia (One Stop Centre) kwa wilaya za Moshi na Siha.

Mjadala huo uliibuka katika mafunzo hayo ya siku nne yanayoendeshwa na Shirika la Kwieco kwa ufadhili wa Taasisi ya Friedrich Naumann Foundation for Freedom-East Afrika (FNF).

Mjadala huo ulioanza baada ya Hakimu Mawole kueleza uzoefu wake kuhusu matukio yanayopelekwa mahakamani kuhusiana na kesi za jinai kama kujaribu kubaka zinavyokuwa na ugumu kuthibitisha.

"Madaktari wengi wanapoitwa mahakamani kutoa ushahidi wao baada ya kufanya uchunguzi wa kitabibu na kujaza PF3, wanatamka kwamba amekuta mtoto amebakwa badala ya kutamka alichokiona kwenye uchunguzi wake mfano 'penetration' (kama kuna kitu kiliingia).

"Sasa majibu kama hayo yanamfanya mshtakiwa atabiri kitakachotokea na matokeo yake anatafuta njia ya kutoroka, lakini unatoa hukumu kabla ya mahakama kumaliza kusikiliza pande zote," alisema.

Wakati Maziku anachangia mjadala huo kuhusu masuala ya ubakaji, alisema daktari kuandika majibu ya moja kwa moja katika PF3 kwamba amekuta mtoto amebakwa au kulawitiwa, si sahihi kwa vile huko ni kutoa hukumu badala ya mahakama kufanya hivyo.

"Kuna haja katika kesi za ukatili wa kijinsia hasa masuala ya ubakaji, ulawiti na hata kukeketa kama daktari atapelekewa mwathirika kwa ajili ya kumpima na kuandika majibu ya uchunguzi wake aandike tu kile alichokiona, lakini si kuthibitisha kwamba amekuta amelawitiwa au kubakwa. Hilo si jukumu lake.

"Wanaoshtakiwa mahakamani kwa makosa hayo wanatumia akili na ujanja mwingi kukwepa adhabu hasa wanapojua daktari amesema tayari kabaka au kalawiti. Kuna haja PF3 ikafanyiwa marekebisho katika baadhi ya vipengele ili kuruhusu haki kuchukua mkondo wake. Huwezi daktari kutoa hitimisho, unahukumu wewe badala ya mahakama," alisema.

Dk. Isaya Bagwela wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi na Dk. Joseph Temba wa Hospitali ya Wilaya ya Siha, kwa nyakati tofauti walijibu mambo yaliyoelekezwa kwao wakisema wao hujaza kwa kufuata maelekezo ya vipengele vilivyomo katika fomu hiyo.

Ofisa wa Dawati la Polisi la Wilaya ya Siha, Eusebius Ndauka, alisema wao hawawezi kufungua kesi ya kubaka au kulawiti mpaka daktari athibitishe kwamba mtoto au mwanamke fulani amefanyiwa kitendo hicho.

Awali, Mtaribu wa Mafunzo hayo, Elizabeth Mushi, kutoka Shirika la Kwieco, alisema wadau waliohusishwa katika mafunzo hayo ni madaktari, polisi, wataalamu wa maabara na maofisa ustawi wa jamii kutoka wilaya za Moshi na Siha mkoani Kilimanjaro.



Mratibu wa Haki za Binadamu wa Shirika la Kiraia la Kwieco, Elizabeth Mushi, akitoa maelekezo kwa maofisa wa serikali wilaya za Moshi na Siha kuhusu shughuli za uendeshaji wa vituo vya huduma jumuishi kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# RC atumia wageni kutangaza vivutio

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ameanzisha kampeni maalum ya kuwatumia wageni kutoka nje ya nchi kutangaza vivutio vya utalii kama njia mojawapo ya kuongeza idadi ya watalii wanaoitembelea Tanzania.

Wageni hao ni kutoka Uingereza, Marekani, Ujerumani, Sweden, Oman, Canada, Kenya na Umoja wa Falme za Kirabu.

Mghwira alioanza kampeni hiyo juzi alipokwenda kushuhudia mashindano ya magari yanayofanyika katika nchi za Afrika ya Mashariki yakijumuisha nchi 14 duniani ikiwamo Tanzania.

Akiwa katika Wilaya ya Same, alikutana na madereva na mawakala wa mbio hizo za 'East African Safari Classic Rally' na kuwasilisha mkakati huo wa kuzitangaza kimataifa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (Kinapa).

"Haya magari yote yanapita katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na hii hifadhi inahitaji kutangazwa zaidi kimataifa ili ijulikane namna ilivyo na vivutio adimu. Lakini Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro tunawaomba mnapotoka Tanzania mkawe mabalozi wazuri kwenye nchi zenu," alisema.

Katika mkakati wake huo, Mghwira alisema katika mkoa wa Kilimanjaro kuna fursa nyingi za uwekezaji kwenye sekta ya utalii na kwamba mpaka sasa waliowekeza ni wachache kuliko eneo lililotengwa. Zaidi ya wageni 400 ambao ni madereva, wasaidizi wao na mashabiki wa mbio hizo za magari, waliweka kambi kwa siku kadhaa katika wilaya za Same na Mwanga mkoani Kilimanjaro wakijiandaa kabla ya kuanza rasmi mashindano hayo. Kutokana na umuhimu wa sekta ya utalii katika kuchangia pato la taifa, Dk. Mghwira alitumia nafasi hiyo kuweleza juu ya fursa za utalii na kuwataka wakati mwingine kuzingatia kutenga muda wa wageni kutembelea hifadhi hizo. Mwaka jana, Mjukuu wa Malkia Elizabeth II wa Uingereza, Prince William (Duke of Cambridge), alitumia saa 48 kuishi katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi iliyoko wilayani Same kujionea na kujifunza maisha halisi ya ndege aina ya tai. Mlima Kilimanjaro ni miongoni mwa vivutio vinavyojulikana zaidi duniani na mwaka huu uko katika kinyang'anyiro cha kuwania tuzo ya dunia ya kivutio bora cha utalii kinachoongoza kwa mwaka 2019.

ama

ALHAMISI DESEMBA 12, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Muhimbili awamu mpya ilivyookoa mabilioni, pia huduma mpya kibao**



AFYA

Ukurasa 16

Mchungaji Korokoni: Nimevua gwanda la madhabahuni, kumsaka 'shetani' ukeketaji



Ukurasa 20

MAZINGIRA



# Msitu wa kipekee duniani utunzwao na wana jamii kwa mila na desturi

Ukurasa 18

# Aingia na bunduki na kuua sita hospitali

**Ostrava, Check**

MTU mwenye silaha, ameingia hospitalini nchini hapa akiwa na bunduki na kuwashambulia kwa risasi wagonjwa sita na kuwauwa , kabla naye kujiua baadaye huko alikokimbilia.

Waliouawa ni wanaume wanne na kinamama wawili, huku kukiwapo wengine waliojeruhiwa na Polisi, walisema mtu huyo alikutwa kajiua akiwa ndani ya gari lake saa tatu baadaye, akihisiwa naye alikuwa mgonjwa wa hospitali hiyo ya Chuo Kikuu cha Ostrava.

Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Jiri Havrlant, alisema, tukio la shambulizi hilo lilifanyika bila ya kauli yoyote au ujumbe wa tahadhari.

Shuhuda wa tukio ambaye anafanya kazi hospitalini, huku akiwa na hofu alisema ni tukio lililoibua msukosuko mkubwa mahali hapo, ambao anadai 'hauelezeki.'

Mtuhumiwa huyo alitenda hilo na kutoweka ndani ya muda mfupi na gari lake. Baadaye mtuhumiwa aligundulika ana umri wastani wa miaka 42.

Polisi walipata picha zake kwa kutumia kamera za usalama na walitoa tangazo kwa jamii kusaidia kuwafahamisha endapo watamuona, huku wenyewe wakizunguka kwa msaada wa ndege za helikopta kufanya kazi hiyo ya kumsaka.




Polisi walipozingira hospitali iliyotokea mauaji. **PICHA: MTANDAO**.

AFYA

# Muhimbili awamu mpya ilivyookoa mabilioni, pia huduma mpya kibao

**Na Mary Geofrey**

- Chimbuko lake ziara ya ghafla JPM
- Yasuka upya wataalamu ughaibuni
- Mapato yapaa bn 2.6/- hadi bilioni 5

MNAMO Novemba 9 ya mwaka 2015, akiwa mgeni madarakani, kwa mara ya kwanza Rais Dk. John Magufuli, alifanya ziara ya kushitukiza katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na kusikiliza kero za wagonjwa.

Baada ya hapo, alitoa maelekezo na fedha za kumaliza matatizo, zikiwamo za uhaba wa vitanda, magodoro, wodi za wagonjwa, vifaa tiba na dawa.

Kuanzia hapo hadi sasa, Mkurugenzi Mtendaji, Prof. Lawrence Museru, anasema ameshatumia Sh. bilioni 37.4 kununua vifaa tiba na mashine za uboreshaji miundombinu na kujenga uwezo wa wataalamu katika miaka hiyo minne.

Akizungumza katika mkutano wake na waandishi wa habari, Prof. Lawrence Museru, anasema maboresho makubwa, MNH imefanikiwa kuongeza mapato kutoka Sh.bilioni 2.6 kila hadi Sh. bilioni tano wa mwezi.

"Katika kipindi cha siku 1,460 tangu Rais Magufuli atembelee Muhimbili na kutoa maagizo kadhaa. Tumeshatumia zaidi ya Sh. bilioni 37.4 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali," anasema Prof. Museru.

**MAELEKEZO YA JPM**

Anaeleza Rais Dl. Magufuli aliwaagiza waondoe kero zilizokuwapo kwa wananchi kuhusu vipimo anavyovitaja MRI na CT-Scan, kutokana na kuharibika kwa muda mrefu.

Mkurugenzi huyo anasema, waliagizwa kushughulikia shida ya ukosefu wa dawa, wagonjwa waliokuwa wakilala chini wapatiwa vitanda na kulipa stahiki za wafanyakazi, zikiwamo posho na nauli za likizo.

Prof. Museru anasema, pia waliagizwa kutoa huduma za ubobezi kupunguza rufaa za nje ya nchi, kuboresha mazingira ya kazi, kununua na kukarabati vitendea kazi.




Mkuu wa Idara ya Mionzi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk Flora Lwakatare, akieleza matumizi ya kifaa hicho. **PICHA ZOTE: MTANDAO**.

> **Katika kipindi cha siku 1,460 tangu Rais Magufuli atembelee Muhimbili na kutoa maagizo kadhaa. Tumeshatumia zaidi ya Sh. bilioni 37.4 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali**

Anasema, baada ya maboresho walifanikiwa kuokoa Sh. bilioni 32 ambazo zingetumika kupeleka wagonjwa kutibiwa nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Prof. Museru, huduma zilizoanza kutolewa MNH na kiasi kilichokookolewa kwenye mabano ni, upandikizaji wa figo (Sh. bilioni 4.5), upandikizaji vifaa vya kusaidia kusikia (Sh. bilioni 2), huduma ya mfumo wa chakula na ini (Sh. bilioni 1.3) na huduma ya radiolojia (Sh.bilioni 24).

Prof. Museru anasema, pia wametoa dawa bure kwa wananchi zinazogharimu Sh. bilioni 72 katika miaka minne ya uongozi wa Rais Magufuli, ikiwa ni sawa na Sh. bilioni 1.5 kwa mwezi.

"Tofauti na miaka ya nyuma, tulikuwa tukitumia Sh. milioni 400 hadi 700 kila mwezi kwa ajili ya dawa za wagonjwa wasiyoweza kumudu gharama za matibabu," anasema Prof. Museru.

Mtendaji huyo mkuu wa MNH, anafafanua kwamba kila , mwezi wanatumia Sh. milioni 600 kutibu wagonjwa wasiyo na fedha za matibabu.

Prof. Museru anataja kingine, walifanya matengenezo ya mashine ya MRI (Magnetic Resonance Imaging) ambacho si cha upasuaji kinachotumika kuchunguza magonjwa mwilini, kupitia mawimbi ya sumaku, redio na kompyuta, kutengeneza picha inayoonyesha sehemu husika inayochunguzwa.

Anasema matengenezo ya mashine ya kuchughuza mwili ya CT-Scan, nayo yalifanyika na inaendelea kufanya kazi vizuri tangu Desemba mwaka 2015.

Kuhusu ukosefu wa dawa, anasema wameboresha na hadi sasa wagonjwa wanapata dawa kwa zaidi ya asilimia 96 kutoka kwenye maduka ya hospitalini, kulinganisha na wastani wa 40 kabla ya uboreshaji hpo.

"Hospitali ilianzisha mfuko maalumu kwa ajili ya dawa ambapo fedha zote zinazopatikana kutokana na mauzo ya dawa hutumika kwa ajili ya ununuzi wa dawa," anasema Prof. Museru.

Anaeleza kuwa, kwa sasa Sh. bilioni 1.5 zinatumika kununua dawa kila mwezi sawa na Sh. bilioni 18 kwa mwaka na katika miaka minne, hospitali imenunua na kuwapa wagonjwa dawa zenye thamani ya Sh.bilioni 72.

**MATATIZO?**

Kuhusu changamoto ya wagonjwa kulala chini, Prof. Museru, anasema walitekeleza kuhamisha wagonjwa wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI) kutoka wodi mbili walizokuwamo na chumba cha wagonjwa wa uangalizi maaluma (ICU), yenye vitanda 15.

Pia, anasema Rais alipatia hospitali jengo lililotumiwa na Wizara ya Afya, Meandeleo ya

INAENDELEA UK.15

AFYA

# Muhimbili awamu mpya ilivyookoa mabilioni, pia huduma mpya kibao

INATOKA UK.14

Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, sasa ni wodi yenye nafasi ya vitanda 91.

Eneo lingine walilofanyia marekebisho ni matatizo ya watumishi, kwamba katika kipindi cha miaka minne, MNH imelipa malimbikizo ya madai ya wafanyakazi, ikiwamo muda wa ziada, wauguzi usiku na posho za watendaji wa tiba

"Hali hii ilishusha morali kwa kiwango kikubwa sana na hivyo wafanyakazi kupunguza kasi ya ufanyaji kazi kwa kujituma na matokeo yake ni kukosekana tija katika utoaji huduma. Kwa sasa, wafanyakazi wengi wa MNH wana ari," anasema Prof. Museru.

KWENYE MABORESHO

Kuhusu upunguzaji rufani za nje ya nchi, anasema kwa nyakati tofauti MNH imepeleka wataalamu wake nje ya nchi, kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

Anataja kada ya wataalamu waliopata ujuzi na elimu ya kutoa huduma hizi kwa ufanisi, ni katika fani anazozitaja kuwa; madaktari bingwa, wauguzi, maabara, radiolojia, magonjwa ya mfumo wa chakula na ini, saratani za damu

Prof. Museru anasema, ni mafunzo yaliyogharimu Sh. bilioni 3.597 na kwamba yamewasaidia Watanzania wengi kuhudumiwa nchini, badala ya kupelekwa nje, vivyo hivyo kiasi kikubwa cha fedha za serikali.

Anataja eneo lingine lililoboreshwa ni kuanzishwa huduma za upandikizaji vifaa vya kusaidia watoto kusikia na kunufaisha wagonjwa 34 na wawili walijigharamia.

Jumla serikali ilitumia Sh. bilioni 1.15, sawa na Sh. milioni 36 kwa kila mgonjwa, tangu Juni mwaka 2017 na kufanikiwa kuokoa Sh. bilioni 2.05 kama wangetibiwa nje ya nchi.

Profesa Mseru anasema, Tanzania ni nchi ya kwanza kutoa huduma hiyo kupitia hospitali za umma katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Prof. Museru anasema katika mwaka huo 2017, Tanzania iliandika historia ya pili kupitia MNH kufanya upandikizaji figo kwa mara ya kwanza na hadi sasa, kuna wagonjwa 51 kwa gharama Sh. milioni 30 kila mmoja, sawa na Sh. bilioni 1.530.

Anaeleza, mbadala wake kama tiba hizo zingelenga kufanyika nje ya nchi, serikali ingetumia Sh. bilioni 6.120 sawa na Sh. milioni 120 kwa kila mgonjwa. Hivyo, imeokoa fedha Sh. 4.590.

"Kabla ya huduma hii kuanza nchini, serikali ilisafirisha wagonjwa 150 nje ya nchi katika kipindi cha miaka 15, wastani wa wagonjwa 10 kwa mwaka," anasema Prof. Museru na kuongeza:

"Kwa miaka miwili, Muhimbili imefikia asilimia 34 ya wagonjwa waliopelekwa nje ya nchi kwa kipindi cha miaka 15," anasema

**RADIOLOJIA NCHINI**

Anataja Novemba mwaka 2017, MNH ilianzinzisha kwa mara ya kwanza huduma za tiba radiolojia ikishirikiana na watalaam kutoka Kenya na Chuo Kikuu cha Yale, Marekani na kuna wagonjwa 558 waliopatiwa huduma, kati yao 274 walikua na uvimbe wa kinywa.

Profesa anasema imeigharimu hospitali Sh. bilioni 2.192 sawa Sh. milioni 8 kwa mgonjwa mmoja.

"Kama wangeenda nje ya nchi ingeigharimu Serikali kiasi cha Sh. bilioni 26.304 sawa na Sh. milioni 96 kwa mgonjwa mmoja kwa safari nne zinazohitajika. Serikali imeokoa Sh. bilioni 24.112 kutoa huduma hizi nchini," anasema Prof. Museru.



Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof. Lawrence Museru.

**Kama wangeenda nje ya nchi ingeigharimu Serikali kiasi cha Sh. bilioni 26.304 sawa na Sh. milioni 96 kwa mgonjwa mmoja kwa safari nne zinazohitajika. Serikali imeokoa Sh. bilioni 24.112 kutoa huduma hizi nchini**

Anasema, MNH ilianzisha na kuboresha huduma za uchunguzi kwa wenye matatizo ya mfumo wa chakula na ini. Wagonjwa 380 walihudumiwa kwa Sh. milioni 116.8 na hospitali imefanikiwa kuokoa Sh. bilioni 1.397.

**SARATANI**

Pia, Prof. Museru anasema wametoa huduma ya saratani iliyoanza kutolewa, ikiwamo uchunguzi wa ugonjwa huo na matibabu ya awali kwa wagonjwa.

Anasema hospitali inakamilisha mipango ya uanzishwaji wa huduma ya upandikizaji uloto (bone marrow transplant) muda wowote kuanzia sasa. Ilidharimiwa kati ya mwezi huu na mapema mwakani.

Kwa mujibu wa Profesa Museru, hospitali husika imeshatumia Sh. milioni 117 kwa ajili ya mafunzo hayo na fedha hizo zimetokana na vyanzo vya ndani vya hospitali.

Kingine anachokitaja mkurugenzi ni kuendelea kuboresha mazingira ya kazi katika kipindi cha miaka minne, ikighalimu jumla ya Sh. bilioni 10, ikijumuisha vyumba vya upasuaji, ili kuendana na kasi ya ongezeko la wagonjwa na uanzishwaji wa huduma mpya hospitalini.

Prof. Museru anasema wamefanikiwa kukarabati na kuongeza vyumba vya upasuaji kutoka 13 hadi 20. Anafafanua: "Hospitali imepunguza msongamano wa wagonjwa kusubiri tarehe ya mbali ili kufanyiwa upasuaji. Jumla ya Sh. bilioni 2.46 zilitumika kiufanya kazi hiyo."

Anasema, pia hospitali iliweza kukarabati na kuongeza vyumba vya wagonjwa wenye kuhitaji uangalizi maalumu, yaani ICU kutoka vitanda 25 hadi 78 na vimejengwa na kuwekewa vifaa tiba.



Rais Dk. John Magufuli alipotembelea Hospitali ya Taifa Muhimbili.

AFYA

# Mchungaji Korokoni: Nimevua gwanda la madhabahuni, kumsaka 'shetani' ukeketaji

- Wanaofanya kabila lake, ana siri zao kibao
- Ana maumivu miaka 39 kifo mdogo wake
- Imani iliyopo 'Julai marufuku kukeketa'

**Na Sabato Kasika,** ALIYEKUWA SERENGETI

"Wamekuwa na tabia ya kukeketa kila mwezi Desemba ya mwaka katika kile wanachokitafsiri kiimani 'mwaka unaogawanyika kwa mbili' na kuacha ule 'unaogawanyika kwa saba tu."

MARA ni mkoa unaotajwa kushika nafasi ya tatu, katika mikoa mitano inayotajwa kuongoza kwa mila potofu za ukeketaji watoto wachanga na wasichana, Serengeti na Tarime.Watangulizi wake Manyara, Dodoma na Singida.

Ziko sababu zinazotajwa kuchangia kuendelea kuwapo vitendo vya ukeketaji, kwenye baadhi ya kabila. Mojawapo ni usiri mkubwa uliopo katika jamii husika zikiamini kukeketa ni sehemu ya mila na desturi zao.

Ni kabila zinazotunza siri za wanaoendeleza vitendo hivyo, ili kuwaepusha wanaokeketa na mkono wa dola. Hali inayosababisha mabinti na kinamama kuendelea kunyanyasika, bila ya kupata msaada.

Inaekezwa kuwapo kabila linaotajwa kuwa kinara wa kuendeleza ukeketaji wilayani Serengeti, licha ya vitendo hivyo kupigwa vita kila kona wanaendeleza, isipokuwa mwezi wa saba ndio hawakeketi wala kufanya sherehe kwa madai 'una mikosi.'



Maonyesho ya sanaa yanayohamasisha kupinga ukeketaji, wilayani Serengeti. **PICHA: MTANDAO.**

**KULIKONI HIVYO?**

Nipashe ilifanya udadisi kwa kumhoji Mchungaji Stephen Korokoni, mkazi wa Mugumu, Serengeti anayetokea katika kabila lililokubuhu kwa tabia hiyo, naye akawa na mengi ya 'kufunguka.'


Ni ushuhuda aliyoutoa kutoka wenye mahafali ya wasichana wahitimu wa mafunzo ya ujasiriamali katika Nyumba Salama inayohudumia kukwepa ukeketaji, inayomilikiwa na taasisi ya Hope for Girls and Women Tanzania, iliyopo Mugumu, Serengeti.

"Mimi ni mtumishi wa Mungu. Nimefanya kazi ya uchungaji katika Kanisa la...(dhehebu kubwa nchini) kwa zaidi ya miaka 20, kisha nikawa huru ili kupambana na vitendo vya ukatili huu," anasema Korokoni.

Anaeleza sababu ya kujiengua alikokuwa mwaka 1994 hadi 2017 aliporejesha safari ya kuwa nje ya ajira, ili awe huru kwenye kazi ya uchungaji kumudu kupinga vizuri vita dhidi dhidi ya ukeketaji.

"Ninaweza kusema kuwa kwa sasa mimi ni mchungaji huru, ambaye nimejikita zaidi katika kupambana na ukeketaji kuanzia kwenye koo za Wangoreme ninakotokea na nyingine za Wilaya ya Serengeti," anasema.

> **Mimi ni mtumishi wa Mungu. Nimefanya kazi ya uchungaji katika Kanisa la...(dhehebu kubwa nchini) kwa zaidi ya miaka 20, kisha nikawa huru ili kupambana na vitendo vya ukatili huu**



Mchungaji Stephen Korokoni, askari wa vita dhidi ya ukeketaji, wilayani Serengeti.



Mkurugenzi wa Hope for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samwelly. **PICHA ZOTE: SABATIO KASIKA**

Anasema, kwa kabila lao (jina tunalo) wamekuwa na tabia ya kukeketa kila mwezi Desemba ya mwaka katika kile wanachokitafsiri kiimani 'mwaka unaogawanyika kwa mbili' na kuacha ule 'unaogawanyika kwa saba tu."

"Wanakeketa miezi yote isipokuwa wa saba tu. Wanakeketa miaka yote inapokuwa unaoishia na saba mwishoni, pia hawafanyi sherehe yoyote mwezi wa saba wala mwaka unaoshia saba (mfano 2017)," anasema.

Mchungaji Korokoni, anasema ni dai la jamii na wana- imani hao wa ukeketaji kwamba wanaitenga herufi 'saba' wakiitafsiri ina mkosi

"Ninaweza kusema kuwa ni mwiko kwa (kabila hilo) kukeketa au kufanya sherehe zozote mwezi wa saba au mwaka unaoishia na saba, lakini miezi mingine na miaka mingine yote, shughuli ni kama kawaida," anasema.

**ANAVYOFANYA KAZI**

Mchungaji huyo anasema, namna anavyifanya kazi sasa amekuwa wakala wa taasisi ya Hope for Girls and Women Tanzania, katika uhamasishaji jamii kuachana na na ukeketaji wilayani Serengeti.

Anaainisha jukumu lake ni kwamba, anawajibika kuwa mshauri wa mambo ya kiroho, imani na mila za ambazo zinainyanyasa jamii na hasa kinamama, huku haziwaachi salama watoto wa kike.

Anasema, licha ya kuacha jukumu lake la uchungaji kanisani, bado ana heshima hiyo inayosaidia asikilizwe, kuwaondoa wana jamii katika mila potofu.

"Nikuhakikishie kuwa nimesaidia familia yetu kuachana na mila hizo, kwani mimi watoto wangu wote watatu wa kike hawajakeketwa na hata wa ndugu wakiwamo wa dada zangu," anasema Korokoni.

Pamoja na mafanikio hayo, ana kumbukumbu ya majuto ya kufiwa na mdogo wake mwaka 1980, baada ya kukeketwa akiwa amehitimu darasa la saba.

Anasema, ni tukio linalogusa nafsi yake hadi sasa na kumfanya aongeze kasi ya kupambana na ukeketaji hatua aliyoianza muda mrefu, lakini kawa anakutana na vipingamizi kutoka kwenye familia na ukoo.

"Tangu kifo hicho, familia yetu imeachana kabisa na mambo ya ukeketaji, ambao kwa kweli ni mateso makali kwa mtoto wa kike, ambaye anahitaji kusoma kwa ajili ya maisha yake ya baadaye," anasema Mchungaji Korokoni.

Analalamika ukeketaji bado upo katika jamii na kwamba na imefikia kwa watoto wachanga, hivyo anashauri watoto wanapopelekwa hospitali wakaguliwe kama wamekeketwa.

"Daktari akimkagua mtoto na kubaini kuwa amekeketwa, basi mama yake akamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria, ili asaidie kuwapata waliofanya unyama huo," anasema.

Mchungaji huyo anasema hilo, akibianisha kugundulika tabia ya watoto wachanga, baada ya kuwapo ufuatiliaji wa serikali na hatua za kisheria.

Pia, anataja mbinu wanazotumia wazazi, wakeketaji na wazee wa mila kuwa ni kuwapeleka watoto porini usiku wa manane wakikwepa kugundulika na kuwafanyia ukatili huo bila huruma.

"Serikali na wadau wengine msichoke kuwafuatilia kwa karibu watu hawa, tuko nyuma yenu ili kukomesha vitendo vya ukeketaji kwa wasichana na watoto wachanga ambao kimsingi ni malaika wa Mungu," anasema.

Kwa mujibu wa sheria za nchi, ukeketaji ni kosa la jinai ambalo mtuhumiwa akitiwa hatiani wanaweza kufungwa hadi miaka 15.

"Kuna madhara mengi kiafya na kisaikolojia yanayosababishwa na ukeketaji kuanzia msihtuko, homa kali, kumwaga damu nyingi na mara nyingine hata kusababisha kifo, kuambukizwa virusi vya Ukimwi," anasema.

Pia, Mchungaji Korokoni, anataja msongo wa mawazo, kuathirika kisaikolojia, ulemavu, kovu la kudumu, maradhi ya fistula, mwanamke kupata shida wakati wa kujifungua na ugumba.

## TMDA: Miaka minne tayari ya kwanza dawa bora Afrika

**Na Yasmine Protace**

NI miaka minne ya mabadiliko makubwa ya kiutendaji katika Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na sasa inahesabu mafanikio makubwa.

Mafanikio hayo yametokana na utendaji kazi ambapo hata usimamizi mzuri wa vyanzo vya makusanyo umeongezeka kwa kasi.

TMDA inaeleza kujivunia kipindi cha miaka minne kwa kusimamia vyanzo vya makusanyo, kutoka Sh. bilioni 34.64 katika mwaka wa fedha 2015/16 hadi kufikia Sh. bilioni 53.31 kwa mwaka fedha 2018/19. Hiyo ni sawa na nyongeza ya asilimia 53.8, hata ikaiwezesha gawio kwa serikali kila mwaka kufikia Sh. bilioni 29.1.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, anasema jijini Dar es Salaam, kwamba ni 'utekelezaji wa kazi chini ya serikali iliyopo, wakapiga hatua kuvuka malengo hayo iliyojiwekea katika udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitenganishi ili kulinda afya za jamii.

Fimbo anaeleza kuwa, TMDA imeweka mifumo na taratibu za ndani za utoaji huduma bora, ili kukidhi mahitaji na matarajio ya wateja kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya (ISO 9001:2015) kwa shughuli za kiudhibiti na kwa huduma za maabara (ISO/IEC 17025:2015).

"Huduma za TMDA hutolewa kwa kuzingatia viwango vya mkataba wa huduma kwa wateja wa mwaka 2016." anasema Fimbo.

Anaongeza kuwa, mfumo wa usajili bidhaa umeendelea kuimarika na idadi za bidhaa zilizosajiliwa zinaongezeka kila mwaka.

Fimbo anasema, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2018/19, mamlaka imeweza kusajili jumla ya bidhaa 20,247 na anaongeza kwamba TMDA

imesajili jumla ya maeneo 32,860 ya biashara, zikiwamo maghala ya kuhifadhi bidhaa.

Aidha, anabainisha TMDA iko makini kudhibiti bidhaa zisizo makini kwa kuziteketeza, pale inapobainika hazikidhi viwango vya ubora na usalama.

"Katika mwaka 2017/18 jumla ya tani 140,705.25 za bidhaa za chakula, dawa na vifaa tiba zisizofaa kwa matumizi ya binadamu zenye thamani ya Sh. 22,394,078,744 ziliteketezwa, ikilinganishwa na tani 664.68 zilizoteketezwa mwaka 2018/19 na hii inaashiria kupungua bidhaa zisizokidhi viwango katika soko la Tanzania," anaeleza.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Adam Fimbo, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo) pichani. PICHA: YASMINE PRTOTACE.. **PICHA: MTANDAO.**

Fimbo anaongeza TMDA inafuatilia, kuondoa na kuteketeza bidhaa zisizokidhi vigezo vya ubora na usalama sokoni.

"Sampuli 1,136 za dawa za binadamu zilichunguzwa kwa kipindi cha miaka minne, asilimia 96 ziliendelea kukidhi vigezo vya ubora na kati ya sampuli 144 za dawa za mifugo zilizochunguzwa katika kipindi hicho cha miaka minne. Asilimia 90 ziliendelea kukidhi vigezo vya ubora," anasema.

Fimbo anasema, kwa upande wa vifaa tiba vitenganishi, kuna jumla ya sampuli 405 zilichunguzwa sokoni na kubainika kukidhi vigezo vya ubora.

Anajigamba kwamba TMDA imeshatambulika kimataifa, kutokana na kuwa na mifumo thabiti ya udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa dawa.

"Desemba 2018, TMDA imeweza kutambulika kufikia ngazi ya tatu (maturity level 3) ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya ubora wa mfumo wa udhibiti wa dawa," anaeleza.

Pia anafafanua WHO imeiona Tanzania nchi ya kwanza Barani Afrika kufikia hatua hiyo na mataifa mengine ya Afrika sasa yanafikia nchini kujifunza jinsi yan kufikia mafanikio.

Hadi sasamebaki hatua moja pekee ya kufikia hatua ya nne (level 4) ambayo ndio ya juu za zaidi katika ubora duniani kote, na nchi nyingi zilizoendelea zimeshafikia.

Fimbo anasema, TMDA imekuwa karibu na jamii kwa kusogeza huduma zake, ili kupunguza gharama na usumbufu kwa kuwa na maabara kubwa za Kanda ya Ziwa, pia ikifunga mashine na mitambo ya kisasa yenye thamani ya Sh.bilioni 5.

Awali TMDA, ilifahamika kama Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kabla ya kupunguziwa baadhi ya majukumu yaliyohamishiwa kwingine.

MAZINGIRA

## KAYA KAUMA

# Msitu wa kipekee duniani utunzwao na wana jamii kwa mila na desturi

- Kuingia sala, kuutunza kwa sadaka
- Ndani wanaishi mababu, masharti...
- Unesco 'yaikubali' ufanisi uliotukuka
- Wana sheria  na adhabu za kuitunza

**Na Salome Kitomari,**
ALIYEKUWA MOMBASA

INAWEZEKANA katika baadhi ya jamii nchini, shughuli za kiutamaduni hasa katika eneo la hifadhi ya mazingira, zinakosa kipaumbele.

Pia, kuna maeneo ambayo jamii zao zina 'miwani' kuona mbali katika mtazamo wa utunzaji mazingira, kwa kuruhusu kundi fulani kutunza misitu ya asili kwa kutumia taratibu zao za kijamii, manufaa yake yakienda mbali katika sura ua manufaa ya kidunia.

Mtu anapofika katika Mkoa wa Pwani nchini Kenya, kuna misitu 45 ya asili inayotunzwa na jamii kuendeleza utamaduni wao, inayojulikana kama 'misitu ya kaya.'

Hiyo inahifadhiwa kwa taratibu na kanuni za kijamii na hakuna anyeruhusiwa kufanya shughuli zozote za kibinadamu humo, isipokuwa wazee wachache walioruhusiwa kuishi msituni.

Kaya hizo zinajulikana kama jamii ya Mijikenda, ikiwa na maana ya vijiji nane vya makabila ya Wadigo na Waduruma kutoka jimbo la Kwale, Wagiriama, Chonyi, Ribe, Rabai, Wakamba, Kauma na Jibana wanaotoka Jimbo la Kilifi.

Msitu wa Kaya Kauma, katika eneo la Mijikenda, una ukubwa wa hekta 78, huku maeneo mengine ya kaya yakiwa na hekta 86.8.

**MAISHA YAO**

Utaratibu wao ni kwamba, kila msitu wa kaya una njia mbili za kuingia na kutoka, katikati ya msitu. Ndiko kwenye makazi ya msituni, lakini kutokana na ongezeko la watu, wamebaki humo wazee wachache huku wengine wanaishi nje ya msitu.

Kwenye kila msitu kuna maeneo ya makaburi, kufanyia vikao, maeneo ya kufanya mila na utamaduni, walinzi na viongozi wa idara mbalimbali katika kuhakikisha msitu unatunzwa vyema.

Kuingia kwenye kaya hiyo ni lazima mtu afuate taratibu na kanuni, kwa sababu kinyume na hapo anaingia katika kuwa bila




Bango la kuonyesha mradi wa vipepeo wanaouzwa nje ya nchi na kuipatia jamii ya Kaya Kauma fedha za kutunza msitu huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

> **Ukiwa kwenye lango la kwanza kuna salamu maalum ambayo huanzishwa na Mwenyekiti wa Kaya, anayetamka "kaya, kaya, kaya..." na wanasalimana naye, wageni au wenyeji wanaitikia 'kaya!' Baada ya hapo, linalofuata ni sala maalum ya kuomba kibali cha kuingia msituni.**

ya kufanya hivyo, mtu anajikuta kwenye mgogoro mkubwa na wanajamii hiyo na iwapo atakamatwa, anapalekwa kwenye kikao cha wazee wa kimila na kutozwa faini.

Ukiwa kwenye lango la kwanza kuna salamu maalum ambayo huanzishwa na Mwenyekiti wa Kaya, anayetamka "kaya,kaya,kaya..." na wanasalimana naye, wageni au wenyeji wanaitikia 'kaya!' Baada ya hapo, linalofuata ni sala maalum ya kuomba kibali cha kuingia msituni.

Mwenyekiti wa Kaya Kauma, Hilary Mwasuma, anasema jamii za Midikenda eneo la Kilifi, ndio jamii kubwa ya wana Kauma ambao wanaamini katika utamaduni wa kutunza uoto wa asili.

Anasema, chimbuko la kaya hizo ni nchini Afrika Kusini, wakaingilia Uganda, Sudan Kusini eneo la Juba , hadi Somalia ambako waliweka makazi na baadaye wakatawanyika kwenye nchi za Afrika Mashariki.

**UINGIAJI MSITUNI**

Mwasuma, aliwaongoza wageni wanahabari kutoka nchi za Afrika Mashariki Kenya, Uganda, Tanzania na Rwanda waliokuwa mafunzoni, kuripoti habari za mazingira kwa ufadhili wa asasi ya Earth Journalism Network, waliingia msituni huku mbele kukiwapo mwanamke aliyebeba mzigo wa kuni na galoni la maji.

Anasema walitawanyika ukanda wa Pwani hadi eneo la mto Tana na baadaye eneo la mpaka wa Tanzania, lakini waliweka makazi ukanda wa Mombasa.

Kwenye eneo hilo msitu unapoanza, wapokeaji ni kinamama waliovaa khanga wanaume wamefunga vikoi vya rangi ya bluu.

**SHARTI LA KUINGIA**

Kabla ya kuingia kwenye msitu huo ulioko umbali wa kilomita 10 kutoka Mtwapa Mjini na kilomita tano kutoka barabara kuu, lazima mtu apate kibali cha wazee, ambao  nao huanzisha sala rasmi kwa miungu yao na baadaye ndio inatolewa ruhusa kuingia.

Sharti la kuingia msituni humo kwa kinamama ni ambao hawashiriki tendo la ndoa walau kwa siku mbili, vivyo hivyo walio katika hedhi haruhusiwi.

Umbali wa mita 300 kutoka eneo la kuingilia ndiko kuna lako kuu ambalo kulia kwake kuna kibanda maaluma, ambacho kila anayekwenda katikati ya msitu, anapaswa kufanya maombi na kuacha sadaka yake.

"Hapa ndipo ambako tunasali wakati wa shida, majanga mbalimbali, tunakuja kuuliza juu ya nini kifanyike kwa yaliyotokea kama kuna mahali tumekosea.

"Tunaamini kwa kuwaomba Miungu yetu ndiyo tunaongea na Mungu. Kabla ya kuingia eneo la ibada lazima upite hapa kwa ajili ya kupata kibali," anasema Mwasuma.

Anafafanua kwamba, kwenye eneo hilo wanaweka mikate na maji kama sadaka ya maombi yao yapokewe na kwamba kama kuna adui, hawezi kuvuka kwenye lango kuu la kuingia.

Ili kuingia kwenye kiini cha kaya Kauma, ni sharti kupita mageti matatu na katika geti la pili, ndiko kuna miti mikubwa miwili na ambao mtu anaingia.

Lango la geti hilo lina miti mikubwa ya mikone, ambayo ni migumu inayotumika kutengenezea majeneza na kwamba hata wakitengeneza bila hilo, wanawekwa walau kipande kuonyesha uhai wa mazingira na binadamu.

Kwenye geti hilo, kila mtu anapaswa kuvua viatu vinavyohifadhiwa katika eneo maalum. Baada ya kuvua viatu, kiongozi anawakabidhi waingiaji kila mmoja jani lake la mti atakalolishika kwa mkono wa kushoto na kuliweka chini baada ya hatua tatu.

Baada ya kuingia, mtu anakwenda kwenye geti la tatu lenye miti kama vile ya geti la kwanza, ndipo anasonga umbali wa mita 50 na kukutana na eneo la Baraza la Wazee.'

Hapo ndiko wanakutana na kujadili mambo mbalimbali au kufanya vikao na jirani wa eneo hilo. Ni mahali anaishi mzee mwenye umri mkubwa kuliko wote, ambaye kwa sasa amebaki na mkewe.

Aidha, mbele kidogo kuna geti lingine ambalo upande wake wa kushoto kuna makaburi kwa ajili ya wazee waanzilishi na wote wa-

**INAENDELEA UK.19**

MAZINGIRA

# Msitu wa kipekee duniani utunzwao

INATOKA UK.18

takaofia ndani ya eneo la msitu.

"Ikitokea mwana kaya amekufa nje ya eneo la msitu, lazima tuwaulize mababu chanzo cha kifo na kama anastahili kuzikwa ndani ataruhusiwa kuzikwa huku. Akifia ndani, moja kwa moja anazikwa kwenye eneo hilo," anafafanua.

Anasema, anafanya mambo kama nchi inapitia changamoto mbalimbali, ikiwamo kutoa sadaka ili kupata jibu la matatizo yaliyopo.

**UTUNZAJI MAZINGIRA**

Msitu huo umefunga vizuri na kinachosikika ni sauti za ndege na hali ya hewa yenye utulivu wa kutosha.

Mwenyekiti huyo anasema, kutokana na uhifadhi kwenye eneo hilo, kwa sasa kuna ongezeko la wanyama kama kima, fisi, paka, nguruwe na wengineo.

"Haturuhusu yeyote kuvuna miti au chochote kwenye msitu wetu.; Tuna walinzi ambao kazi yao kubwa ni kulinda msitu, kwa sasa kuna mabadiliko makubwa tofauti na zamani watu walivuna watakavyo," anasimulia.

Mwenyekiti anaendelea: "Tunaruhusu uchimbaji wa dawa ambao tunachimba wenyewe tofauti na wanaochimba kwa ajili ya biashara."

**VIKAO, IBADA, MABABU**

Hapo kwenye makazi ya mzee mwenye umri mkubwa kuliko wazee wote, eneo la ibada na vikao na eneo la mababu ambako kuna sanamu zao kuonyesha uzao wa kwanza wa waanzilishi na vimewekwa chini ya mbuyu mkubwa na eneo hilo kusafishwa vyema.

Wanapofika kwenye eneo hilo, kuna koo tano na kila mmoja anakaa nyuma ya ukoo wake. Huo ni utaratibu wa kuwavalisha nguo mpya kwa mwaka mara moja na kuna mzee mwenye mamlaka na hilo.

"Tunaamini kabisa huwezi kwenda kwa Mungu bila ya kupita kwa mababu zetu. Tunawaomba na kuleta sadaka zetu kwao, ili maombi yetu yapate kukubalika kwa Mungu.

"Wapo wanaodhani ni uchawi au imani za kishirikina, lakini siyo hivyo, bali tunafanya kwa mujibu wa utamaduni wetu na miongoni mwetu, wapo Wakristo na Waislamu ambao wanahudhuria ibada maeneo yao," anafafanua.

Anasema, yeye kama Mwenyekiti wa Kaya Kauma, hana mamlaka kwenye baadhi ya vitengo kwa kuwa vipo vitengo kama vya wanawake, mtunza fedha na eneo la mababu.

**VIKAO BARAZA**

Kwenye eneo la vikao vya baraza lao ni lazima Mzee Kiongozi amwage pombe kuongea na Miungu, kabla ya kuanza shauri lolote na iwapo itasambaa na kutochimba kishimo kidogo, basi mababu watakuwa wamekataa. Hapo hakuna kitakachoendelea hadi watakapokubali.

Anasema mahakama ya kimila inashughuikia kesi ndogo ndogo kama mtu amekata miti miwili au kukutwa na mazao ya msitu na iwapo atakutwa na mengi atapelekwa kwenye mahakama nyingine.

"Faini zetu ni mbuzi, kondoo, kuku na iwapo shauri lake ni kubwa, atapelekwa kwenye ngazi za juu ambazo hukutanisha wazee wengi kwenye Kaya Rabia na ikishindikana wanapekekwa mahakama za serikali," anasema.

**MSITU & UTAFITI**

Anasema, asilimia 70 ya miti asili inapatikana kwenye msitu huo na wanapata kipato kwa kutembelewa na wageni kutoka sehemu mbalimbali duniani, ikiwamo wakufunzi na watafiti wanaofanya tafiti mbalimbali.

"Msitu huu na mingine ya wana Mijikenda imekuwa kielelezo cha utunzaji wa mazingira duniani, kwa sasa msitu unasaidia dunia kupata hewa safi na kupunguza hewa ukaa, hii ni kutokana nasi kujitolea kutunza mazingira bila kujali," anasema.

**MATATIZO YAO**

Mwasuma anasema, changamoto kubwa iliyopo ni jamii kutoelewa wanachofanya. Wanahusisha na vitendo vya imani za kishirikina, kwa sababu hivi karibuni kulikuwapo mauaji ya wazee.

Anasema, wamefanya vikao kuwaelimisha vijana kinachofanyika ni kwa faida ya dunia na kingine ni wafanyabiashara wa dawa na kienyeji wanaongia kinyemela kuvuna kwa namna ya uharibifu, akifafanua "wanachofanya wao ni uvunaji wa dawa endelevu kwa ajili ya matumizi yao na siyo biashara."

**SERIKALI &HATI MILIKI**

Mwenyekiti huyo anasema, ameshawahi kuwa Mwenyekiti wa Makaya Kauma kwa miaka minane na walipigania kupata hati kwa jina la Kaya, lakini serikali imekisita kuhalalisha ombi hilo.

"Tumefika kwa viongozi mbalimbali ikiwamo serikali, tumepeleka hoja zetu kuwa tunataka kumiliki maeneo haya kisheria lakini yasiwe kwa jina la yeyote lakini bado serikari haijatupa,"anasema.

Anafafanua: "Hakuna bajeti ya kutunza misitu hii. Tunafanya wenyewe kwa nguvu zetu lakini bado wameshindwa kutumilikisha"

"Tumefika hadi bungeni kuwaeleza jinsi mila na itamaduni zinavyotunza mazingira, lakini wameshindwa kutupa hati miliki, ingawa wanatambua uwepo wetu na Unesco inayatambua maeneo yetu," anawekeza kiongozi huyo mtunza msitu.

**UNESCO?**

Ofisa Uhifadhi wa Misitu kanda ya Pwani ya Kenya, eneo la Kilifi, Lawrence Chiro, anasema kuna misito ya aina hiyo 45 iliyotangazwa kwenye gazeti la serikali, huku kaya tisa zikiorodheshwana Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco, mwaka 2008.

Kwenye lango la kuingilia, Unesco wameweka bango la kulitambua eneo hilo kama urithi wa ulimwengu, chini ya mfumo wa shirika hilo na linasomeka:

"Kaya Kauma zilizotapakaa katika eneo linalokisiwa kuwa na kilomita 200 za mkoa wa Pwani wa Kenya ni sehemu za misitu. Sehemu hizo zapatikana juu ya milima, zenye ukubwa wa kati ya hecta 30 na 300 ambayo ndani yake ni mabaki ya miji ya zamani iliyofichika Makaya ya Mijikenda."

Bango hilo linafafanua eneo Makaya ilianza kutotumika mwanzoni wa Karne ya 20 na sasa zinatambuliwa kama kumbukumbu za imani ya kiroho ya Wamijikenda na ishara ya utakatifu ya watu wao wa kale."

Unesco inafafanua:"Misitu inayozunguka Makaya imetunza na jamii ya Wamijikenda ili kulinda maeneo takatifu ya makaburi. Sasa yanakaribia kuwa maeneo ya kipekee yaliyosalia, kutokana na eneo la msitu ambalo wakati fulani ulikuwa msitu mkubwa wa Nyanda za Chini za Ukanda wa Pwani."

Kwa mujibu wa Chiro, changamoto kubwa iliyopo sasa ni ukataji miti kwa ajili ya kuuza, nishati na kufungua mashamba, uchomaji moto na vijana kutoheshimu wazee, jambo linalochangia kuuawa kwa baadhi ya wazee kwa madai ya imani za kishirikina.

Jingine, ni uchimbaji madini kwenye eneo la Kaya Kambe na Kauma, jambo lililoharibu msitu kwa kiasi kikubwa, huku serikali ya eneo hilo ikiangalia mapato yatokanayo na uchimbaji huo.

Anasema Mamlaka ya Hifadhi ya Misitu, inachukua hatua mbalimbali kuilinda kwa kushirikiana na jamii hizo, kutoa elimu, tafiti, kufuata taasisi na kaya kutunza maeneo hayo.



Haya ndio maisha ndani ya msitu wa Kaya Kauma.

> **Wapo wanaodhani ni uchawi au imani za kishirikina, lakini siyo hivyo, bali tunafanya kwa mujibu wa utamaduni wetu na miongoni mwetu, wapo Wakristo na Waislamu ambao wanahudhuria ibada maeneo yao**



Mwenyekiti wa Kaya Kauma, Hilary Mwasuma, akiwaonyesha waandishi wa habari, eneo linalotumiwa kutoa sadaka kabla ya kuingia kwenye lango kuu la msitu unaotunzwa na jamii ya Mijikenda. **PICHA ZOTE: SALOME KITOMARI.**

DOKEZO KWA WATAFITI

# Ilivyo kitedawili cha kutumia gesi na 'kuacha mkaa, kuni'

**Na Nimi Mweta**

WAKATI matumizi ya gesi yamepanuka kwa sehemu kubwa na hasa mijini, kuna maeneo mengi ambako suala siyo gharama za kutumia gesi, ila ufanisi wa nishati hizo mbili kwa ubora wa kinachohitajika.

Ni eneo linalohitaji utafiti wa ziada, kwani hakuna uhakika nchi zinazotengeneza mitungi ya gesi ya kupikia, zimewahi kukutana au kutambua kuwa kuna tatizo katika eneo hilo, au analitatua kwa njia nyingine.

Kwa mfano, kuna matumizi ya umeme ambayo nchi iko bayana ni ghali sana, hivyo mapishi ya gesi au mkaa, ndio yanabaki kipaumbele.

Mtu anapopita mitaani kunakouzwa chipsi na nyama choma au kuku, anaweza kusikia hoja kwamba 'inafaa kuchoma nyama, kwani inaiva taratibu zaidi na vyema zaidi.'

Matumizi ya gesi yanahusishwa na kuivisha mboga haraka kwa 'kubabia' katika baadhi ya mboga, huku walaji na wahudumu wao wanajua, mkaa ni bora zaidi kutumia kuliko gesi.

Ili kupata chakula kilichoiva vizuri, inalaezwa siyo rahisi kuleta hisia ya mazingira kushawishi matumizi zaidi ya gesi, ilhali inaleea chakula kisichoridhisha.

Wakati inawezekana kuwa kuna tatizo la jumla la viwango katika utengenezaji wa mitungi ya gesi, pia kuwa zipo nchi zisizotegemea gesi kwa kiwango kikubwa, pake umeme wao unakuwa wa gharama nafuu.

**VIWANGO VYAKE**

Kuna tatizo la viwango, ambavyo si lazima viwe vya kimataifa, mfano kuhusiana na 'valvu' za mitungi ya gesi. Ni tatizo linaloendana na mabadiliko ya kiteknolojia.

Katika miaka ya 1960, zililetwa 'stovu' za Uingereza na pale zilipoondolewa, zikaja za Kichina ambazo nazo zikafa, nafasi ikachukuliwa na majiko ya utambi, ambayo ni rahisi kutumia.

Hivi sasa kuna tatizo la 'valvu'zenye upana mkubwa zaidi ya mahitaji ya watumiaji na haihitaji utaalamu au kuwa fundi kujua upana wake na mengine ya ziada.

Wakati fulani, mtu anasikia matangazo ya kutaja usalama wa valvu kama kielelezo cha ubora wa aina hii au ile ya majiko, lakini inavyoelekea kuna tatizo la jumla.

Endapo kampuni zinazouza mitungi na majiko zingekuwa zimetatua hilo na wengine wangeiga, kwani ubora hayafichiki sokoni, wateja na umma wanapeana ufahamu wa

> **Kuna wateja wanaoletewa chakula bila ya kuwa na uzoefu wa karibu, kutathmini namna kinaivyoiva.**

kinachofaa. Hakuna kilichofichika tena.

Hapo inabeba mana kwamba, lipo tatizo la jumla la kuoanisha mahitaji ya watumiaji na viwango vya watengenezaji, ambao huenda wanatoka katika mazingira ya nishati mbadala ya kuni haishindani na gesi.

Mbadala unaokuwapo hapo, ni ushindani kati ya nishati ya umeme na gesi, jambo ambalo halipo wazi sana katika mazingira ya nchini, tofauti haionekani.

Ili kupata uliganishi katika hayo mawili, mtu anapaswa kwenda kwenye hoteli au migahawa mikubwa kuchimba namna nishati hizo mbili zinatumika kwa wingi muda wote, mkaa ukiwekwa kando.

Kuna wateja wanaoletewa chakula bila ya kuwa na uzoefu wa karibu, kutathmini namna kinaivyoiva.

Kisaikolojia, inawezekana nishati ya gesi ingefaa kutumika kuchoma nyama, lakini wateja wanapokuwa karibu, hawaipendelei nishati hiyo kwa madai "chakula hakiivi kwa namna inavyotakiwa."

Wanaiojua tofauti iliyopo, ni watumiaji majumbani na kwa vile haitaji la mkaa linaendelea kuwa kubwa hadi vizuizi vya kuvuna miti vitakapopandisha bei ya mkaa na kulazimisha mjini wabadili matumizi ya nishati.

Mbadala wa mkaa ni 'jiko la mchina' lisilohitaji gharama kubwa za ununuzi wa mafuta ya taa na kubadili.

Hitilafu iliyopo ni kwamba, juhudi za kubadili tabia za watumiaji majumbani na katika migahawa, kuondokana nishati ya kuni au mkaa na kuanza kutumia gesi peke yake haiwezi kufanikiwa kwa urahisi kutokana na hitilafu hiyo, kwani mbadala mwingine wa umeme, bado ni ghali.

Elimu inafaa kumpa mtu ufahamu wa jambo, lakini yenyewe haijitosheleza. Ni bei ya mkaa itakayowezesha zaidi wateja waache matumizi yake.

Hata hivyo, kuna upenyo wa utafiti unaowezekana katika utengenezaji valvu za gesi, hasa kwa vile kuna kampuni zinazotaka kuanzisha utengenezaji mitungi ya gesi nchini.

Teknolojia inatajwa kuwa na upungufu na katika mazingira ya Kiafrika na kwingineko, ladha na upendeleo wa nishati zinafanana. Kinachotawala sasa ni kupatikana ufanisi ambao sasa haupo, ili gesi itumike kirahisi, kufikia hatua ya kupendwa kwa hiari.

Katika utengenezaji wa valvu, yako maeneo mawili yanayoleta shida sasa. Moja ni upana wa valvu zenyewe, na hapo ndipo kunaleta uhitaji wa teknolojia, kwani uzembe kila siku ni kushindwa kulenga na kupata upana unaohitajiwa.

Tofauti na hapo, inaelezwa ni kulipua, itoke valvu inayotoa moto mwingi kwa kulazimisha na ukijaribu kupunguza inazimika na ndizo valvu zilizoko sasa.

Vyuma vya kutengenezea valvu hizo ili zisipanuke baada ya kuanza kutumika, vinapaswa kuangaliwa upya.

Katika baadhi maeneo yanayohitaji kufanyiwa kazi, ili gesi ishindane kikamilifu na mkaa na uzuiaji kuvuna miti ufanikiwe, vinginevyo inabaki kuwa tatizo la mahitaji ya kijamii kulazimika kutumia gesi na tabu ya bei kupanda.









Nyenzo mbalimbali za mapishi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**



## HABARI MBEYA

# Mbegu feki zapungua Nyanda Juu Kusini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TATIZO la uzalishaji na usambazaji wa mbegu feki za mazao mbalimbali kwa wakulima katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, limepungua na hivyo kuwa na matumaini ya wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao hayo.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Mfawidhi wa Taasisi ya Kudhibiti ubora wa mbegu nchini (Tosci), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Peter Nasari, wakati jopo la maofisa wa taasisi hiyo kutoka makao makuu mkoani Morogoro na wa Kanda waliposhirikiana kufanya ukaguzi kwenye maduka jijini Mbeya.

Alisema mwaka wa kilimo uliopita waliyafungia maduka 11 mkoani Mbeya na kuyapatia zuio maduka zaidi ya 20 kutokuuza baadhi ya mbegu mpaka zitakapothibitishwa ubora wake na mwaka huu wamelifungia duka moja pekee.

Alisema hali hiyo inaleta matumaini kuwa wafanyabiashara na wazalishaji wa mbegu wameanza kufuata sheria kutokana na elimu inayotolewa pamoja na hatua za kisheria ambazo zinachukuliwa dhidi yao. "Tumekuwa tukitembelea madukani na kwenye maghala ya kuhifadhia mbegu hizi, sasa mwaka huu tumelifungia duka moja pekee katika Wilaya ya Chunya ambalo tumekuta linauza mbegu ambazo hazina nembo ya ubora," alisema Nasari.

Alisema kwa sasa hata malalamiko ya wakulima kuhusu kuuziwa mbegu feki yamepungua kwa kiasi kikubwa na kwamba mbegu za sasa zinafanya vizuri shambani tofauti na ilivyokuwa miaka iliyopita.

Pia alisema katika Mkoa wa Songwe wamelifungia duka moja pekee mwaka huu kutokana na kuuza mbegu ambazo zimezalishwa nchi jirani ya Zambia, lakini hazina nembo ya ubora kutoka Tosci.

Kwa upande wake mkaguzi wa mbegu kutoka Makao Makuu ya Tosci, Emmanuel Mwakatobe, aliwataka wakulima kuendelea kuchukua tahadhari wanapokwenda kununua mbegu ili wasiuziwe mbegu feki.

Aliwataka wakulima kununua mbegu zenye nembo ya Tosci ambazo ndizo zimethibitishwa ubora wake na zinafaa kwa matumizi ya wakulima kote nchini. Alisema kuwa hata kama kuna mbegu ambazo zimezalishwa nje ya nchi na kuingizwa nchini, lazima zithibitishwe ya Tosci ambayo ina nembo maalum inayoonyesha uhalali wake wa kutumika nchini.

Alisema mbegu ambazo hazijathibitishwa zina madhara makubwa ikiwamo kutoota au kutoleta tija ya mavuno kwa mkulima na hivyo kuwaingizia wakulima hasara.

"Wakati mwingine wakulima wanapanda mbegu shambani, lakini hazioti vizuri jambo ambalo linawaingiza hasara kubwa, sasa tunawashauri wakulima kutunza risiti za mbegu wanazonunua ili iwe rahisi kufuatilia endapo zitaleta shida," alisema Mwakatobe.

Aliwataka wafanyabiashara na wazalishaji kuendelea kuwa waaminifu ili kuwasaidia wakulima kufikia ndoto zao na hata wao kuukwepa mkono wa sheria ambao ni pamoja na kufungiwa biashara zao na kushtakiwa mahakamani.

Alisema kwa sasa serikali inapambana kuufikia uchumi wa kati na kama wadau wa sekta ya kilimo ni lazima washiriki kuhakikisha uzalishaji wa mazao unakuwa bora.



Mkuu wa Jeshi la Magereza Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Magereza, Mathias Mkama, akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, kuhusu mmoja wa wafungwa walioachiwa kwa msamaha wa Rais ambaye alikuwa anadaiwa kugoma kutoka katika Gereza la Ruanda jijini Mbeya, ambapo alithibitisha kuwa mtu hiyo alichukuliwa na ndugu zake. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Vijana wapatao tiba dawa za kulevya waongezeka

**Na Nebart Msokwa,** KATAVI

IDADI ya vijana walioathirika na dawa za kulevya wanaopata tiba katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya imeongezeka kutoka vijana sita waliojitokeza wakati huduma hiyo ikianzishwa mwaka juzi hadi kufikia vijana 275 wanaoendelea kupewa huduma hiyo hivi sasa.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, alisema hayo juzi wakati akizungumza kwenye maadhimisho ya miaka 20 ya uwepo wa Ubalozi wa Marekani nchini yaliyofanyika Mpanda mkoani Katavi.

Alisema kuwa idadi hiyo ya vijana inaongezeka kutokana na wengi wao kupewa elimu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na kuamua kuachana na matumizi ya dawa hizo.

"Tangu kituo chetu cha kuhudumia watu walioathirika na dawa za kulevya kizinduliwe kwenye Hospitali ya Rufani ya Kanda ambayo ndiyo kitovu cha huduma za afya kwa mikoa yetu hii ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, vijana wamezidi kujitokeza kupata huduma na wakati tukianza tulikuwa na vijana sita na sasa wameongezeka na kufikia," alisema Dk. Mwanji.

Dk. Mbwanji aliishukuru serikali ya watu wa Marekani kwa kufadhili ujenzi wa kituo hicho cha kuhudumia watu walioathirika na dawa za kulevya kwa kuwa kimekuwa na msaada mkubwa wa kuwaondoa vijana kwenye wimbi la matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema mbali na msaada wa ujenzi wa kituo hicho, pia Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Walter Reed Army Institute of Research (WRAIR), imetoa mchango mkubwa kusaidia utafiti na huduma kwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi ikiwamo kutoa dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi kwa waathirika wa ugonjwa huo. Dk. Mbwanji alisema mpaka sasa zaidi ya watu 7,000 wanapewa huduma ya dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi hospitalini hapo na watu wengi wanaotumia dawa hizo kwa ufasaha afya zao zinaendelea vizuri.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Kupambana na Ukimwi Tanzania (Tacaids), Dk. Leonard Maboko, alisema Serikali ya watu wa Marekani kupitia Shirika lake ya WRAIR ni mdau mkubwa nchini katika mapambano dhidi ya Ukimwi nchini.

Alisema Marekani imetoa misaada mingi ya hali na mali katika kusukuma mbele mapambano dhidi ya Ukimwi ikiwamo kufanya utafiti kwa ajili ya kutafuta chanjo na tiba ya ugonjwa huo.

Dk. Maboko alisema kuwa pamoja na kwamba utafiti huo unaendelea, mpaka sasa hakuna dawa wala kinga ya ugonjwa wa Ukimwi hivyo akawataka Watanzania kuendelea kujikinga wasipate maambukizi ya ugonjwa huo.

# Hospitali ya kisasa kukomboa wananchi Tunduma

**Na Ibrahim Yassin,** TUNDUMA

BAADA ya kupata adha ya ukosefu wa huduma za afya huku wengine wakitembea umbali mrefu, hatimaye serikali inajenga hospitali ya kisasa itakayotoa huduma kwa watu zaidi ya 170,000 na kuondoa changamoto zilizopo.

Zaidi ya Sh. bilioni tisa zinatumika katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Momba, mkoani Songwe inayojengwa Kata ya Mpemba, katika mji wa Tunduma huku watu zaidi ya 170,000 wanatarajia kupatiwa tiba wakiwamo wa nchi jirani za Zambia na Malawi.

Anastazia Hezron, mkazi wa Mpemba, jana alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakitembea umbali mrefu kusaka tiba hali inayosababisha baadhi ya wajawazito kujifungulia njiani na wengine wakipoteza maisha na watoto waliojifungua.

Hassan Mrisho mkazi wa Tunduma, alisema, halmashauri ya mji wa Tunduma ina kata 15 na moja pekee ndiyo yenye kituo cha kutolea tiba hali inayosababisha kuwapo kwa msongamano mkubwa kutokana na wakazi wote kutegemea tiba katika kituo hicho.

Alisema kutokana na kadhia hiyo kwa sasa wameanza kufarijika baada ya kuona serikali inajenga hospitali kubwa na ya kisasa katika halmashauri hiyo na kwamba wanaamini kwa sasa wataondokana na kadhia hiyo ya kutembea umbali mrefu kusaka tiba hasa kwenda mkoani Mbeya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Regina Bieda, alisema halmashauri hiyo kwa sasa inategemea kituo kimoja cha afya chenye uwezo wa kuhudumia watu 11,000 na kwamba kukamilika kwa hospitali hiyo watu zaidi ya 170,000 watapatiwa tiba na pia wataondokana na shida iliyokuwa ikiwakumba ya kutembea umbali mrefu.

Mkuu wa wilaya hiyo, Juma Irando, akielezea umuhimu wa hospitali hiyo, alisema kwa sasa wananchi wategemee manufaa kutoka katika hospitali hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nickodemas Mwangela, alisema Halmashauri ya Mji wa Tunduma iko mpakani, na ina mwingiliano wa watu kutoka nchi zaidi ya tano hivyo serikali imeona ni vema kujenga hospitali kubwa itakayotoa huduma kwa watu wao.

Alisema hospitali hiyo tayari imepangiwa bajeti ya dawa na vifaa tiba vya kutosha hivyo ana uhakika kuwa wananchi wa Tunduma pamoja na wilaya za jirani zikiwamo nchi za Malawi na Zambia zitanufaika na huduma za matibabu katika hospitali hiyo.



# Dodoma wapewa somo la kisiki hai

**Na Mwandishi Wetu,** KONGWA

WANANCHI wa Mkoa wa Dodoma wameshauriwa kutunza mazingira kwa njia ya kisiki hai ili kukabiliana na athari za mabadilikio ya tabianchi.

Rai hiyo ilitolewa na mratibu wa kisiki hai mkoa humo, kutoka Shirika lisilo la Kiserikali la Lead Foundation, Theresia Kapinga, katika kongamano la uhamasishaji wananchi kutunza mazingira kwa njia ya kisiki hai lililofanyika wilayani Kongwa.

Kapinga alisema msimu huu wa kilimo ni vyema wananchi kuacha visiki hai katika mashamba yao ili kusaidia kubadilisha mazingira na kuleta mvua za kutosha.

"Lakini bila kusahau makinga maji, hiki ndio kipindi muhimu sana cha kuchimba makinga maji hasa wananchi waliopo kwenye mwinuko," alisema Kapinga.

Awali Mwenyekiti wa Umoja wa Machampion wa kata tano za Kongwa ikiwamo Chamkoloma, Mikaeli Jastini, alisema tangu mradi wa kisiki hai kuanzishwa kumekuwa na mafanikio mengi ni pamoja na jamii kuwa na uelewa juu ya utunzaji miti. "Baadhi ya wakulima na wafugaji bado ni changamoto kwa kuwa wanakata miti kwa ajili ya kuzibia mazizi ya mifugo yao na hawachukuliwi hatua yoyote tunaomba uongozi wa halmashauri kuiongelea katika vikao vyao," alieleza Jastini.

Aidha, aliutaka uongozi wa kijiji kutunga sheria ndogo zitakazosaidia kudhibiti watu wanaokata miti ovyo.

Naye Mratibu wa Kisiki Hai, Tarafa ya Mlali, Wilaya ya Kongwa, Salome Kifimbo, alisisitiza viongozi wa vijiji kutunga sheria ndogo za mazingira ili kuwadhibiti watu wanaojihusisha na vitendo vya ukataji miti ovyo.

"Tuna misitu ya hifadhi ya kijiji, tuombe serikali kuwe na utaratibu wa kutunza hizi hifadhi za kijiji ikiwezekana tuwe na ratiba za upogoleaji, ili kusaidia wananchi waone utunzaji wa mazingira ni wa kwao," alisisitiza Kifimbo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, akizungumza wakati wa kufungua mkutano wa 14 wa siku tatu wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSA) uliofanyika jana, jijini Dodoma.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ombi serikali kuondoa leseni ya biashara taasisi za dini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Kikristo ya Huduma za Jamii (CSSC), imeiomba serikali kutoa mwongozo kwa halmashauri ya kuondoa leseni ya biashara kwenye vyuo na shule zinazomilikiwa na taasisi za dini, kwa kuwa elimu wanayotoa ni hisani na sio biashara.

Ombi hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa Huduma za Elimu wa tume hiyo, Petro Masatu, katika kikao cha mwaka cha wakuu wa shule za sekondari zinazomilikiwa na kanisa nchini, kilichofanyika jijini hapa.

Alisema baadhi ya halmashauri zimekuwa zikidai leseni wakati taasisi hizo hazifanyi biashara bali zinatoa huduma ya elimu kuisaIdia serikali kufikisha huduma kwa jamii.

"Tunaomba Ofisi ya Tamisemi ishirikiane na mamlaka zingine kusaidia halmashauri zisidai leseni hizo, shule zetu pia zinatakiwa kulipia gharama za uendeshaji wa shule ([WCF) kwa watumishi ipo juu kwa waendeshaji wa shule zetu tunaomba ifanane na serikali, maana kule wanalipa asilimia 0.5 sisi tunalipa asilimia moja, " alisema.

Aidha, aliomba wizara kusitisha mitihani ambayo imeibuka ya kiwilaya tofauti na ile iliyopangwa kitaifa ikiwamo 'Mock' kwa kuwa inasababisha usumbufu na gharama kwa wazazi na shule.

"Tume inaendesha taasisi za elimu 1,033 ikiwamo elimu ya awali, msingi, sekondari, seminari, ufundi stadi, ualimu na elimu ya juu na kwa upande wa ufaulu kwa shule za kanisa umekuwa chachu nchini ambapo mwaka 2013 hadi 2018 matokeo ya kidato cha nne kwa shule zilizo na wanafunzi zaidi ya 40, shule 100 bora, kanisa limekuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 70," alisema.

Masatu alisema tume imeanzisha mitihani ya pamoja kwa wanafunzi wenye mitihani ya kitaifa kabla ya kufanya mtihani wa taifa ili kufanya ulinganifu wa mitihani hiyo.

Padri kutoka Jimbo Katoliki la Moshi mkoani Kilimanjaro, Padri William Ruwahi'chi, aliipongeza serikali kwa kuendelea kushirikiana na taasisi za dini.

"Tunashukuru sana kwa serikali kwa kuendelea kuthamini mchango wa shule za kanisa, tunaahidi kuhakikisha tunatoa elimu bora, changamoto kubwa kwetu ni hii ya kudaiwa leseni ya biashara wakati taasisi za kanisa zinatoa huduma na si za kibiashara," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Elimu, Kaimu Mkurugenzi wa Elimu na Utawala wa ofisi hiyo, Dk. George Idamva, alisema serikali inatambua na kuthamini mchango wa taasisi za kidini kwenye sekta ya elimu na ipo tayari kutoa ushirikiano.

Alishauri ombi la asilimia moja ya gharama za uendeshaji wa shule kufanana na ya serikali ya asilimia 0.5 liwasilishwe kwa maandishi kwa hatua zaidi.

# Changamoto za ugatuaji wa madaraka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUWAPO na mitazamo inayokinzana kati ya watendaji na viongozi wa kisiasa katika mamlaka za serikali za mitaa kwenye kuweka vipaumbele na kutekeleza miradi ya maendeleo, imetajwa kuwa ni miongoni mwa changamoto zinazoikabili Sera ya Taifa ya Ugatuaji wa Madaraka ya mwaka 1998.

Hayo yalielezwa na Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Afya, Ofisi ya Rais- Tamisemi Dk. Dorothy Gwajima, alipokuwa akifungua kikao kazi cha

wakurugenzi wa wizara zote wa Sera na Mipango wanaopitia na kujadili rasimu ya Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa wananchi, mkakati wa utekelezaji wa sera pamoja na programu ya kuimarisha Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Alisema changamoto hiyo inajitokeza kwa viongozi hao kwenye ngazi ya vijiji, kata na halmashauri.

Aidha, alisema changamoto nyingine ni mamlaka hizo kutegemea fedha kwa kiasi kikubwa kutoka Serikali Kuu na wizara za kisekta kutopeleka fedha zinazoendana na majukumu yaliyogatuliwa.

"Pia mfumo hafifu wa mawasiliano kwa baadhi ya Wizara za Kisekta na OR- Tamisemi pamoja kuwapo kwa sera ya ugatuaji iliyojengwa kwenye mfumo wa kisheria inayoelekeza mipaka, majukumu na utaratibu wa utekelezaji wake," alisema.

Kufuatia changamoto hizo, aliwataka wakurugenzi hao kutanguliza uzalendo katika kufanya mapitio ya sera hiyo mpya inayotengenezwa kulingana na mahitaji ya sasa.

"Wakurugenzi wote waliohudhuria kikao hiki ni wabobezi wa masuala ya mipango na bajeti katika wizara zao hivyo wanafahamu mahitaji ya

wananchi halikadhalika mahitaji ya wizara wanazofanyia kazi kwa upana wake, kwa hiyo wako katika nafasi nzuri ya kupitia sera hii na kutoa mawazo yenye tija kwa manufaa ya nchi yetu," alisema.

Alisema kazi hiyo ni nyeti kwa mustakabali wa Taifa, wanatakiwa kujitoa kwa dhati na kuweka uzalendo mbele ili kulinda maslahi ya nchi.

"Mjitume haswa katika kufanya kazi hii kwa weledi na moyo wote kwa sababu ninyi ndio wataalamu katika eneo hili, makundi mengine yamepitia sera hii lakini ninyi ni wataalamu na wabobezi wa sera, hivyo mchango wenu wenye ni muhimu sana kwa mafanikio ya sera hii," alisisitiza.

Akizungumzia mafanikio ya sera hiyo ambayo imemaliza muda wake, Dk. Gwajima alisema sera hiyo ilisaidia katika ongezeko la uelewa na ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo na utawala.

Naye Mkurugenzi wa Uratibu wa Sekta wa ofisi hiyo, Dk. Andrew Komba, alisema kuwa sera iliyopo sasa ni ya mwaka 1998 hivyo imekwisha muda wake na kuna kila sababu ya kufanya mapitio ya sera hiyo ili kuendana na mahitaji ya sasa na mabadiliko yaliyopo sasa.



# Serikali kuwachukulia hatua wanaojaribu kujiua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amevitaka vyombo vya sheria kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaojaribu kujiua kwa njia tofauti ikiwamo kula dawa au sumu na wengine kujaribu kujinyonga kwa kutumia kamba au nguo.

Akizungumza wakati akifunga kikao cha Baraza la Wawakilishi, alisema hilo ni wimbi jipya la masuala ya udhalilishaji na unyanyasaji linaloendelea kuwa janga la dunia ambalo kwa sasa linaonekana kuibuka na kuleta taharuki kwa upande wa Zanzibar.

Balozi Seif alisema sheria za nchi zinatambua kuwa kitendo cha kutaka kujiua ni kosa la jinai, hivyo ni busara wanaokumbwa na mchanganyiko wa mawazo wakaliepuka kwa kutafuta ushauri nasaha mapema utakaoleta amani ya roho kwao.

Akizungumzia uadilifu wa utumishi wa umma na utawala bora, alisema uwazi, uwajibikaji, maadili na ukweli ni chachu ya mafanikio kwa utumishi wa umma na taifa kwa jumla.

Balozi Iddi aliwataka watendaji wote wa taasisi na mashirika ya umma nchini kuzingatia na kufuata vyema uadilifu utakaowaongezea uchungu wa kuheshimu na kuthamini rasilimali za nchi na kuepuka kupanga mbinu za kuhujumu maeneo yao kwa kujibinafsisha kwa maslahi yao binafsi.

Aliwaomba watendaji wenye tabia hiyo kuacha mara moja hulka hiyo na kuwataka wasimamizi wa Tume ya Maadili ya Umma kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Utumishi wa Umma na Utawala Bora wajitahidi kufuatilia maadili ya watendaji na kuchukua hatua stahiki.

Balozi Iddi aliwaomba wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wananchi kutoa ushirikiano kwa serikali katika mpango wake shirikishi wa miaka 10 wa kupiga vita maradhi ya kipindupindu.

Alisema mpango huo wenye lengo la kuondoa kabisa usambazaji wa vimelea vinavyoeneza maradhi ya kipindupindu Zanzibar, umeipa fursa Wizara ya Afya Zanzibar kufanya utafiti wa kitaalamu wa kubaini chanzo cha maradhi hayo.

Alieleza kuwa utafiti huo utasaidia kuelewa maeneo hatarishi ya kipindupindu na kupanga mipango ya kukabiliana na ugonjwa huo utakaofanyika katika wilaya za Mjini, Magharibi "A", Magharibi "B", kwa upande wa Unguja na wilaya za Wete na Micheweni kwa upande wa Kisiwa cha Pemba.

Katika mkutano huo wa 16 wa Baraza la tisa la Wawakilishi Zanzibar, wajumbe wa Baraza hilo walipokea, kujadili na kupitisha miswada mitano ya sheria ambayo ni pamoja na wa sheria ya kuanzisha ofisi ya Mufti, namba 9 ya mwaka 2001 pamoja na muswada wa sheria ya kuanzisha Wakala Serikali mtandao na kazi zake.

Mengine ni muswada wa sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake, mswada wa sheria ya marekebisho ya sheria ya usafiri barabarani Na. 7 ya mwaka 2003 pamoja na mswada wa sheria ya kuanzisha wakala wa barabara Zanzibar.

Baraza la Wawakilishi limeahirishwa hadi Februari 5, 2020.

# Wakulima wanufaika kilimo cha mihogo, viazi vitamu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar imesema kuwa wakulima wa zao la muhogo na viazi vitamu wananufaika kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao hayo.

Hayo yalielezwa visiwani Zanzibar na Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo anayeshughulikia kilimo, Mansura Mossi Kassim, wakati akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa utafiti wa zao la muhogo na viazi vitamu.

Alisema zao la muhogo Zanzibar limeonekana kuwa ni la pili kuwa na faida katika mazao ya chakula likiongozwa na mpunga.

Alieleza kuwa utafiti unaonyesha kuwa kiasi cha tani 65 za muhogo zinazalishwa kwa mwaka na viazi vitamu tani 55 kwa mwaka. "Utafiti unaonyesha wazi kuwa wakulima wengi hivi sasa wa mazao hayo wamekuwa wakilima chakula na mazao mengine kuuza nje ya Zanzibar," alisema. Awali wakulima wa Zanzibar walikuwa hawana utaalamu wa kutosha wa mazao hayo, walikuwa wakichanganya kulima muhogo na viazi na husababisha kupata mavuno kidogo.

Vile vile, alisema Wizara ya Kilimo inaendelea kuwapa elimu wakulima kuhusu kilimo hicho.

Alisema licha ya kukua kwa mazao hayo, lakini bado kumeonekana changamoto mbalimbali ikiwamo ya wakulima wengi kutoweka mbolea katika mazao yao.

Kwa upande wake mjumbe wa mkutano mkuu huo anayeshughulikia zao hilo kutoka Tanzania Bara, Mombeki Wiston, alisema kilimo hicho kwa sasa kinakwenda vizuri kwa kiasi kikubwa na wakulima wameshaanza kupata faida.

Alisema wakulima wengi walikuwa wakichanganya mazao hayo jambo ambalo lilikuwa likiwakosesha kipato.

Alieleza kuwa baada ya kuja kwa mradi wa 'African Cassava agronomy intiative' mafanikio yameshaanza kupatikana kwa sasa. Alisema mradi huo unatekelezwa na nchi 12 Afrika ikiwamo Nigeria ambayo kwa sasa iko vizuri katika kilimo hicho. Mapema mratibu wa uandishi wa mradi huo wa 'International Institute For Tropical Agriculture' kutoka Nigeria, Dk. Bernard Vanlauwe, alisema wakulima wengi hawakufikia malengo ya kilimo hicho kutokana na mambo mbalimbali ikiwamo kukosa pembejeo za kilimo na kukosekana kwa watafiti.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akifunga kikao cha baraza hilo, huko Chukwani Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Alama barabarani kuwekwa maeneo yote ya shule

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imesema itaishauri serikali kuweka alama za barabarani pamoja na ulinzi katika maeneo yote yenye shule kando ya barabara kuu.

Akizungumza na uongozi wa Shule ya Sekondari Chaani na familia za wanafunzi wawili waliofariki dunia kwa ajali ya gari, Jumamosi iliyopita, Naibu Waziri wa wizara hiyo Simai Mohammed Said, alisema suala hilo ni muhimu ili kulinda usalama wa wanafunzi na watumiaji wengine wa barabara.

Simai aliyefanya ziara hiyo kuzifariji familia za wanafunzi hao pamoja na shule, alisema, ujenzi wa barabara ni muhimu kwa maendeleo, lakini wakati mwingine kunakuwa na changamoto ambazo jamii inapaswa kuzikabili.

Hata hivyo, aliwataka madereva wa vyombo vya moto kuwa waangalifu wanapokuwa barabarani hasa maeneo ya shule ambako watoto wanatembea na kuvuka barabara. Alisema wizara na serikali kwa jumla zimehuzunishwa na vifo vya wanafunzi hao ambavyo vimetokea wakiwa wamemaliza kufanya mtihani wa kidato cha pili, na kuzitaka familia kuwa na moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu.

Naye Mwenyekiti wa kamati ya shule hiyo, Haji Khamis Haji, aliishauri serikali kuweka vifaa vya kudhibiti mwendo katika kila shule iliyoko karibu na barabara na vituo vidogo vya polisi ili kuwafanya madereva wapunguze kasi.

Kwa upande wazazi wa wanafunzi hao, walisema ingawa ajali imeandikwa, lakini wakati mwingine husababishwa na uzembe wa madereva ikiwamo mwendo kasi.

Pamoja na kuishukuru serikali kwa kuwatembelea na kuwafariji, lakini wameiomba ihakikishe barabara zinakuwa na vifaa vya tahadhari, askari na kuzijengea matuta ili kuwanusuru watoto na watu wengine.

Naibu Waziri wa Elimu, alikwenda Chaani kwa ajili ya kuzifariji familia za marehemu hao pamoja na kutoa ubani kwa msiba huo uliowapata.

Desemba 7, mwaka huu, wanafunzi wawili, Zuleikha Miraji Ali (15) na Zainabu Vuai Dude (16) walifariki dunia kwa kugongwa na gari kando ya barabara karibu na shule yao baada ya kufanya mtihani wa taifa wa kidato cha pili.

# 1,312 wilaya waathiriwa ukatili kijinsia

**Na Anthony Gervas,** BUSEGA

WATU 1,312 katika Wilaya ya Busega mkoani Simiyu, wametajwa kuwa wameathiriwa na ukatili wa kijinsia.

Taarifa hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya hiyo, Tano Mwera, katika kilele cha maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia wilayani humo.

"Takwimu zinaonyesha idadi ya watu walioathiriwa na ukatili wa kijinsia waliofikishwa kwenye vituo vya afya na zahanati wilayani Busega na kuhudumiwa na kitengo cha ustawi wa jamii ni wanawake 934 na wanaume 378," alisema Mwera.

Mwera alieleza kuwa licha ya kuwapo ukatili huo, lakini pia takwimu za mimba za ututoni zilizowasilishwa ni 19, ambapo wanafunzi wa shule za sekondari ni 15 na wa msingi ni wanne.

Alisema wilaya hiyo imeunda kamati ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwa watoto katika kata 15, kuwa na dawati la jinsia katika kituo cha polisi kwa kuwa shughuli kuu za kamati hizo ni kuelimisha jamii kuhusu udhibiti wa ukatili huo.

Alisema kamati hizo zinafanyakazi chini ya mpangokazi wa taifa wa kutokomeza ukatili wa kijinsia (Mtakuwwa) ambazo zimekuwa zikipambana vikali kuhakikisha ukatili huo unapungua zaidi au kutokomezwa kabisa.

Alisema katika kutekeleza maadhimisho hayo, shughuli zinazoendelea kufanyika wilayani humo ni pamoja na kutoa elimu ya kuzuia unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika Shule ya Msingi Itongo, Shule ya Sekondari Masanza na kuelimisha jamii juu ya unyanyapaa kwa makundi maalum.

"Elimu ya kutokomeza unyanyapaa inaendelea kutolewa kwa watu wenye ulemavu wa viungo, watu wenye ualbino, watu wasioona, wenye uoni hafifu na watu wenye matatizo ya kusikia katika vijiji vya Lamadi, Nyakaboja, Kiloleli, Badugu pamopa na Ijitu," alisema.

Alisema pia jamii imekuwa ikielimishwa juu ya haki na sheria kupitia mikutano ya hadhara katika vijiji wilayani humo ili kutambua na kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia katika vyombo vinavyojihusisha na udhibiti wa vitendo hivyo kwenye jamii.

Alisema kuwa awali kwa miaka mingi waganga wa jadi wamekuwa wakishtumiwa vikali na jamii, madhehebu ya dini na wadau wengine wa maendeleo kuwa walikuwa chanzo cha kuagiza viungo vya watu wenye ualbino kwa madai ya kuwapatiwa watu utajiri, kutibu maradhi yasiyotibika na hata kutafuta uongozi kutokana na kupiga ramli chonganishi. Hivyo alisema viongozi wa dini na waganga wote wa jadi kutoka kata 15 za wilaya hiyo wamepatiwa elimu ya kuachana na ukatili huo katika jamii pamoja na viongozi wa dini kujengewa uelewa wa kuhubiri amani na upendo kwa wananchi.



Muuza mananasi wa soko la Buguruni jijini Dar es Salaam akiwa mwenye fikra katikati ya biashara yake, ambapo matunda hayo yamekuwa mengi na kusababisha bei yake kushuka, nanasi moja huuzwa kati ya Sh. 500 hadi Sh. 2000. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Baba mbaroni tuhuma kubaka binti yake

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba linamshikilia mkazi wa Taifu Wilaya ya Wete kwa tuhuma za kumbaka mtoto wake wa kumzaa mwenye umri wa miaka 12.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mohamed Shehan Mohamed, alisema tukio hilo lilitokea Novemba 11, mwaka huu usiku, katika kijiji cha Taifu Shehia ya Kinyasini Wilaya ya Wete Pemba.

Alisema baba huyo (43), anadaiwa kumwingilia binti yake wa kumzaa ambaye alikuwa anaishi na shangazi yake Wingwi Wilaya ya Micheweni, na kwamba wameshamkamata.

"Mtoto huyo alikuwa anaishi na shangazi yake, lakini baba yake alikwenda kumchukua ili aishi nae, ingawa alifanya kinyume cha alivyosema wakati anamchukua," alisema.

Alieleza mtuhumiwa aliachana na mkewe ambaye ni mama wa mzazi wa mtoto huyo, na kuwa mtoto alipelekwa kwa shangazi yake Wingwi kulelewa, ingawa baba baada ya muda alikwenda kumchukua mwanaye kwa madai ya kuishi nae nyumbani kwake Taifu.

"Kwa kweli ni mtihani kwa sababu huyo baba hana mke mwingine, hivyo baada ya kwenda kumchukua walikuwa wanaishi wawili peke yao na cha kusikitisha zaidi alikuwa analala naye kwenye godoro moja," alisema kamanda huyo.

Kamanda Shehan alisema mtuhumiwa wamemkamata na upelelezi utakapokamilika, watamfikisha mahakamani.

Katika hatua nyingine, Kamanda Shehan alisema jeshi hilo linamshikilia Suleiman Zahor Omar (28), mkazi wa Bopwe Wete kwa tuhuma za kumtorosha mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 17.

Alisema tukio hilo lilitokea Desemba 4, mwaka huu usiku, ambapo mtuhumiwa alimchukua mtoto huyo Gando na kumpeleka Mangwena Wilaya ya Wete.

"Mtoto huyo aliaga kwao anakwenda kununua chipsi, lakini hakurudi tena na baada ya wazee wake kumfuatilia, walimkuta Mangwena," alisema Kamanda Shehan.

Aliwataka wananchi kuacha kuwafanyia watoto vitendo vya udhalilishaji, kwani Jeshi la Polisi limejipanga vya kutosha kuwashughulikia wote watakaotuhumiwa kwa makosa hayo.

"Sisi kama Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) tunaudhika sana kusikia matukio haya kila siku, lakini kwa hili la baba anayetuhumiwa kumbaka mtoto wake tutasimama kidete kuhakikisha anachukuliwa hatua za kisheria iwapo atabainika kuwa ni mkosaji, ili haki itendeke," alisema Mratibu wa TAMWA-Pemba, Fathiya Mussa Said.

# Waziri azitaka halmashauri kujifunza Ikungi

**Na Juster Prudence**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais , Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amezitaka halmashauri nchini kwenda kujifunza Ikungi, mkoani Singida ambao wamejenga majengo kwa viwango na kwa fedha kidogo iliyotolewa na serikali.

Akizungumza juzi alipotembelea miradi ya ujenzi wa ofisi ya mkuu wa wilaya na majengo ya halmashauri hiyo, alisema umoja wa Mkuu wa wilaya hiyo na Mkurugenzi Mtendaji umewezesha miradi ya maendeleo kutekelezwa kwa ubora na wakati.

"Nilidhani mnaigiza kwamba mmesikia waziri anakuja mkaanza kujenga ila ninaona hapa ujenzi unaendelea vizuri, nawapongeza sana Mzinga, jukumu letu ni kutafuta kazi, tunataka jengo likamilike wananchi wapate huduma, wafanyekazi kwenye ofisi na siyo madarasa," alisema.

Aidha, alisema Halmashauri ya Ikungi ni ya kuigwa kwa kuwa wametumia Sh. bilioni 1.5 kujenga ukumbi na ofisi za watumishi, na kwamba wapo wanaong'ang'ani kujenga ghorofa na kutumia fedha nyingi.

"Unakuta Mkurugenzi anang'ang'ania kujenga ghorofa ametumia bilioni mbili au sita halafu watumishi bado wanakaa kwenye vichaka, hapa Sh. bilioni 1.4 mmepata ofisi safi na watumishi wanakaa pazuri. Watu waje kujifunza Ikungi kwenye matumizi ya fedha za umma," alisema Jafo na kuongeza:

"Nikusifu sana mkurugenzi na ofisi yako ni nzuri na safi sana, nimeenda Wanging'ombe nimekuta ofisi imegeuzwa karakana, mipira imejaa ndani, uchafu tuu, hapa ofisi mtu akifika safi inapendeza:

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri wa Ikungi, Justice Kijazi, alisema ukumbi wa halmashauri limejengwa jengo kwa Sh. milioni 420 na kuweka samani ndani, na kwamba kwa sasa vikao vya halmashauri vinafanyika humo ikiwamo kukodisha kwa ajili ya sherehe mbalimbali.

Wakati huo huo, akiwa wilaya ya Iramba, alieleza kuchukizwa na wizi wa vifaa ya ujenzi unaoendelea na kwamba limekuwa jambo la kujirudia mara kwa mara licha ya kwamba aliwahi kukataza jambo hilo kabla na kuongeza kuwa vifaa vinavyoibiwa ndivyo vinavyotegemewa katika ujenzi wa miradi mbalimbali.

Jafo aliwataka Mkuu wa Wilaya hiyo pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Iramba kutoa maelezo juu ya tukio hilo ifikapo Ijumaa ya Desemba 13, mwaka huu.

## HABARI KIMATAIFA

# Meya Nairobi aachiwa kwa dhamana

**NAIROBI,** Kenya

GAVANA wa Nairobi, Mike Mbuvi Sonko, hatimaye ameachiliwa kwa dhamana ya Dola za Marekani 150,000, lakini amepewa marufuku ya kutohudumu katika ofisi yake.

Katika uamuzi uliotolewa katika Mahakama ya Milimani jana,

pia amezuiwa kutumia ofisi yake isipokuwa iwapo ataandamana na ofisa wa uchunguzi ama mtu yeyote aliyeruhusiwa na mahakama.

Atakapoenda katika ofisi yake akiandamana na ofisa aliyeruhusiwa, ataruhusiwa kubeba vitu vyake pekee.

Sonko na washukiwa wenzake pia wamepigwa marufuku kutosafiri na watahitaji ruhusa ya mahakama kabla ya kufanya hivyo.

Mkuu huyo wa kaunti ya Nairobi, pia ametakiwa kuhakikisha kwamba wafuasi wake wanaweka amani.

BBC

# UN yabaini chanzo cha machafuko ya Libya

**TRIPOLI,** Libya.

RIPOTI moja ya Umoja wa Mataifa inasema makundi kadhaa yaliyojihami kutoka Sudan na Chad yalihusika katika machafuko ya Libya mwaka huu.

Hata hivyo, ripoti hiyo haikutaja uwapo wa vikosi vya wapiganaji wa Urusi kama ilivyoainishwa kwenye vyombo vya habari hivi karibuni.

Urusi imekataa kwamba wapiganaji wake wanamuunga mkono mbabe Khalifa Haftar, ambaye alianzisha mashambulizi Aprili ya kuuchukua mji mkuu Tripoli kutoka kwa serikali ya muungano inayotambulika kimataifa.

Ripoti hiyo imeyataja makundi matano ya Sudan na manne kutoka Chad

ambayo yote yamechangia kutoa maelfu ya wapiganaji katika sehemu zote mbili za mzozo huo.

Lakini mwanadiplomasia mmoja ambaye hakutaka kutambulishwa, alisema kuna wapiganaji kutoka Urusi wanaoshiriki vita hivyo.

Aidha, alisema jopo linalohusika na uchunguzi linakusanya ushahidi wa wapiganaji wa Urusi wanaohusika na wataifahamisha kamati ya UN katika miezi kadhaa ijayo.

Ripoti hiyo imefichua kwamba Jordan na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), wamekuwa wakimuunga mkono Haftar, huku Uturuki ikiiunga mkono serikali.

DW



Gavana wa Nairobi, Mike Mbuvi Sonko(kulia), anayetuhumiwa kwa rushwa akiwa katika Mahakama ya Milimani.**PICHA:BBC.**

# Uingereza wakabiliwa na chaguo gumu

**LONDON,** Uingereza

WAKATI wapigakura wa Uingereza wakijiandaa kushiriki katika uchaguzi muhimu ukiwa ni wa tatu mwaka huu, wanakabiliwa na chaguo gumu linalohusisha viongozi wawili wasiopendwa.

Nick Boles, mbunge wa zamani wa chama cha uhafidhina, anasema kwamba wanakabiliwa na 'chaguo la kutisha' kati ya mtu 'asiyeaminika na dikteta'.

Ni kama uchaguzi wa 2016 ambapo wagombea wote walionekana kuwa na 'dosari na wasioaminika, na swala hilo linaonekana tena miaka mitatu baadaye katika upande wa pili wa Atlantic.

"Watu wana wasiwasi na kusema kwamba wamechoka", Mary Roberts mgombea wa chama cha Leba katika eneo la bunge la Kaskazini mwa Wales la Ynys Mon, aliwaambia wafuasi wake katika mkutano wa hadhara Jumapili.

Hii ni fursa ya kwanza ya Boris Johnson kusimama mbele ya wapigakura wa Uingereza kama Waziri Mkuu wa Uingereza. Ni uchaguzi alioutaka licha ya kwamba kampeni zenyewe hazijakosa panda shuka.

Wakosoaji wamezua hofu kuhusu uaminifu wake, suala muhimu wakati ambapo Johnson anajaribu kuwahakikishia wapigakura kwamba anaweza kuiongoza Uingereza nje ya Muungano wa Ulaya (EU) ifikapo mwisho wa Januari na baadaye afuatilie hilo na mazungumzo mazuri ya uhusiano wa kibiashara.

Wengi wamedai kumekuwa na msururu wa ahadi ambazo hazikutekelezwa, ikiwamo matamshi ya kupotosha, kuhusu bima ya afya, na mipango yake ya kujiondoa kwa Ireland Kaskazini.

Pia amekosolewa kwa kukataa kuzungumzia kuhusu idadi ya watoto alionao, suala ambalo pia liliangaziwa na vyombo vya habari vya Marekani. Suala linalojiri mara kwa mara katika maswali yetu ni uaminifu, mwandishi wa BBC, Andrew Neil, alisema katika mahojiano aliojiandaa kumfanyia Johnson .

Johnson alikataa mahojiano wakati wa uchaguzi katika kipindi cha Neil- akiwa ndiye mgombea pekee kufanya hivyo katika uchaguzi wa hivi karibuni. Pia alikataa kuhudhuria mjadala kuhusu hali ya hewa na badala yake akawakilishwa na donge la barafu lililokuwa likibubujika.

Pengine kitu ambacho kimemuharibia sifa Johnson katika siku za mwisho za kampeni yake ni chapisho la Jumatatu kuhusu picha ya mtoto

mdogo mwenye miaka minne, aliyelazwa katika hospitali moja mjini Leeds akiwa amelala katika sakafu kwa kuwa hakukuwapo vitanda zaidi katika hospitali hiyo. Picha hiyo iliosambaa mitandaoni na hususan katika mitandao ya

kijamii, imekitia wasiwasi chama cha uhafidhina, huku kikiomba msamaha kuhusu kile kilichomtokea mtoto huyo mbali na kujitetea dhidi ya madai kwamba kisa hicho kinatokana na ufadhili wa chini katika mfumo wa afya nchini humo.

Johnson alijibu katika mahojiano na ripota mmoja wa ITV, huku akikataa kutazama picha ya kijana huyo katika simu ya ripota huyo baada ya kuichukua simu hiyo na kuingiza katika mfuko wake akisema ataifuatilia baadaye.

Tabia yake ilionyesha wazi kwamba huenda waziri huyo mkuu hajajihami vya kutosha kukabiliana na ukosoaji dhidi yake, huku akishindwa kuonyesha huruma.

Kiongozi wa chama cha Labour, Jeremy Corbyn, aliingilia akisema chama cha wahafidhina kimekuwa uongozini kwa miaka tisa na sasa kinasema kinafadhili mfumo wa afya, na kwamba ni uongo, hawajaanza hata kurekebisha upungufu waliokuwa nayo katika kipindi cha miaka tisa iliopita.

**BBC**

# Wavamizi wa hoteli wadhibitiwa

**MOGADISHU, Somalia**

VIKOSI vya usalama nchini Somalia, vimewashinda washambuliaji waliovamia hoteli ya SYL katika mji mkuu wa Mogadishu.

Makabaliano hayo ya saa saba yamesababisha vifo vya wanajeshi wawili na raia watatu. Mamlaka ya usalama nchini humo inaripoti kuwa wanajeshi wengine wawili na raia tisa walijeruhiwa.

"Kufikia sasa vikosi vya usalama vimewaokoa watu 82.wakiwa raia na maofisa wa serikali, "Naibu kamanda wa polisi wa Zakia aliandika kwenye mtandao wa Twitter.

Washambuliaji watano wanadaiwa kutekeleza shambulizi hilo wakati kundi la wapiganaji wa Al Shabaab likikiri kutekeleza shambulizi hilo.Washambuliaji walitumia bunduki na bomu kuvamia maofisa wa vikosi vya usalama waliofika kukabiliana nao.

Washambuliaji wote watano waliwaua katika makabiliano kwa mujibu wa maofisa wa usalama. Hata hivyo, idara ya polisi imeonya kuwa idadi ya raia waliowaua inaweza kuongezeka.

Wanamgambo wa Alshabab nchini Somalia wamekiri kuhusika na shambulio linaloendelea katika hoteli ya kifahari mjini Mogadishu SYL nchini Somalia na makabiliano yanaendelea.

Polisi inasema imewaokoa watu 82 waliokuwamo ndani ya hoteli hiyo. Taarifa zinasema makundi ya wanajeshi wanaonekana kwenye barabara inayoelekea katika kasri ya rais.

Taarifa ambazo hazijathibitishwa, zinasema makumi kadhaa ya watu waliokuwamo ndani ya hoteli ya SYL wanaripotiwa kuokolewa, na washambuliaji wawili wameuawa na vikosi vya usalama vya Somalia, huku wengine watatu wakiendesha mashambulio ndani ya hoteli.

Kituo cha redio cha Dalsalam mjini Mogadishu, kimesema kwenye ukurasa wake wa twitter kuwa wabunge wawili kwa jina Mahgan pamoja na waziri wa zamani wa mambo ya ndani wa Somalia, Abdulkadir Ali Omar wamejeruhiwa.

Vyombo vya habari nchini humo vimeripoti kuwa shughuli ya uzinduzi wa kitabu ilikua ikiendelea ndani ya hoteli ya SYL wakati shambulio hilo lilipotokea ambapo watu zaidi ya 70 walikuwa wamekusanyika kwa ajili ya tukio hilo.

**BBC**

# Watumishi umma waonywa maadili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), George Mkuchika, ameonya baadhi ya watumishi ambao bado wanakiuka misingi ya uadilifu, hivyo kusababisha usumbufu kwa wananchi na kuharibu taswira ya serikali.

Amesema serikali haitawavulia, na kuzikumbusha mamlaka za ajira kutosita kuchukua hatua stahiki dhidi ya watumishi wote wasiozingatia maadili katika utendaji wao.

Aidha, Mkuchika ameziagiza taasisi zote za umma kusimamia utekelezaji wa mkakati wa Taifa dhidi ya rushwa na mpango kazi wake kwa kuwa na kamati za kusimamia uadilifu na kusimamia ipasavyo utekelezaji wa mkakati huo.

Alitoa maelekezo hayo jana alipokuwa akifungua kongamano la kuadhimisha Siku ya Maadili na Haki za Binadamu jijini hapa.

Alibainisha kuwa kila mtu anafahamu namna ambavyo serikali inavyosimamia maadili katika utumishi wa umma hususan katika kipindi hiki cha miaka minne cha mabadiliko makubwa.

Alifafanua kuwa kiwango cha uadilifu katika utumishi wa umma kimeongezeka kwa kiasi kikubwa, hivyo kuwapongeza watumishi ambao wameitikia wito wa serikali wa kuzingatia maadili katika utumishi wa umma.

"Hata hivyo, kuna baadhi ya watumishi ambao bado wanakiuka misingi ya uadilifu na wamekuwa wakisababisha usumbufu kwa wananchi na kuharibu taswira ya serikali.

Ningependa kutumia nafasi hii kuwaonya watumishi hao kuacha tabia hiyo, maana serikali haitakuwa tayari kuwavumilia watumishi wa aina hii," alisema.

Alizikumbusha mamlaka za ajira kutosita kuwachukulia hatua stahiki dhidi ya watumishi wote wasiozingatia maadili katika utendaji kazi wao.

Alibainisha hatua ambazo serikali imezichukua katika kuhakikisha kwamba utumishi wa umma unazingatia maadili ambazo ni kutunga sheria zinazosimamia utendaji katika utumishi wa umma kama sheria namba 13 ya maadili ya viongozi wa umma ya mwaka 1995 na miongozo mingine ya kiutumishi.

Alieleza katika kuimarisha uadilifu katika sekta ya umma, serikali pia imetekeleza mkakati wa Taifa dhidi ya rushwa na mpango kazi wake ambapo taasisi zote za umma zinapaswa kuwa na kamati za kusimamia uadilifu.

Aliziagiza taasisi zote za umma nchini kusimamia utekelezaji wa mkakati huo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba kila taasisi inakuwa na kamati za kusimamia uadilifu ili kuweza kusimamia ipasavyo utekelezaji wa mkakati huo.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Mary Mwanjelwa, alisema serikali imejikita kwa kiasi kikubwa kwenye uadilifu na uzalendo, na kuwataka watendaji kukemea suala la rushwa bila woga na kusimamia yaliyo mema.

"Sisi tuliopewa jukumu la kusimamia maadili tuishi katika yaliyo mema kwa kuhakikisha tunakuwa barua ya kujisoma wazi mbele ya wengine," alisema Mwanjelwa.

Alisema ruswa, ukwepaji kodi na utakatishaji fedha ni miongoni mwa sababu zilizoelezwa kukwamisha jitijada za nchi nyingi pamoja na Tanzania katika kutoa huduma muhimu za kijamii na maendeleo.

Kwa mujibu wa mwakilishi wa Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Paul Mlemya, alisema kila mwaka fedha nyingi duniani zinatumika katika kulipa rushwa au zinaibwa katika mifumo mbalimbali isio rasmi, hali inayochochea kuongezeka kwa wimbi la ukiukwaji wa haki za binadamu.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Barclays Tanzania, Simon Mponji (kulia), akizungumza na baadhi ya wateja katika hafla waliyowaandalia baada ya uzinduzi wa tawi jipya ya Benki ya Absa Tanzania mjini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukarabati gati Sengerema wakamilika

**Na Elizabeth Zaya,** SENGEREMA

WAKAZI wa Kijiji cha Kanyala, Kata ya Bulyaheke wilayani Sengerema mkoani Mwanza, wamesema kukamilika kwa ukarabati wa gati la kushusha na kupandisha mizigo na abiria katika Bandari ya Lushamba kutaongeza kasi ya biashara katika visiwa vinavyozunguka bandari hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika bandari hiyo, Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Benjamini Nhungwizi, alisema awali biashara ilikuwa inasuasua katika eneo hilo kutokana na kukosekana kwa miundombinu hiyo.

Alisema kabla ya kujengwa kwa gati hilo, watu walikuwa wakilazimika kuwekewa ngazi ya kupita au kubebwa na vijana waliokuwa wamejiajiri kwa kazi hiyo.

"Vijiji vingi katika kata hii ya Bulyaheke viko visiwani, kwa hiyo usafiri mkubwa katika eneo hili ni kupitia njia ya maji. Bila kuwapo kwa miundombinu imara, shughuli zetu hazifanyiki vizuri na kwa ufanisi, kwa hiyo tunaishukuru Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) kwa kutujengea gati hili," alisifu.

Meneja wa TPA katika Bandari za Ziwa Victoria, Morris Mchindiuza, alisema ujenzi wa gati hilo utasaidia kutoa huduma katika visiwa zaidi ya sita vya Ikosalozi, Soswa, Gombale, Shembaya, Shemagati na Zilagula.

Alisema gati hilo linatarajiwa kuanza kazi mwezi huu na vyombo vyote vinavyofanya kazi katika visiwa hivyo vitawekwa katika eneo moja na vitakuwa vinasimamiwa na kuwekewa utaratibu maalum.

Mchindiuza alisema wanatarajia kutumia gati hilo kupitishia shehena kubwa, wakitarajia pia kuongezeka kwa idadi ya wafanyabiashara wakubwa wa kulitumia.

# Bandari Chato kuwa kivutio cha kiutalii

**Na Elizabeth Zaya,** CHATO

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imekamilisha ukarabati wa Bandari ya Nyamirembe wilayani Chato kwa awamu ya kwanza, ikieleza kuwa imepanga kuitumia kama sehemu ya kivutio cha utalii.

Akizungumza na waandishi wa habari bandarini hapo, Meneja wa Bandari za Ziwa Victoria, Morris Mchindiuza, alisema wamepanga bandari hiyo itumike kama kivutio cha utalii kutokana na kuzungukwa na hifadhi za taifa.

Alizitaja baadhi ya hifadhi zinazozunguka bandari hiyo kuwa ni pamoja na Hifadhi ya Lubondo na Burigi-Chato.

"Haya maeneo ya utalii yaliyopo na bandari hii ni ya Tanapa (Shirika la Hifadhi za Taifa) na tayari wanayatangaza, kwa hiyo kwa ukaribu uliopo, lazima watalii watafika mpaka huku, na ndiyo maana tukaamua kujipanga kabisa.

"Lakini pia utalii wa maji nao unapendwa na watu wengi na kwa sababu ya jiografia ya bandari hii, tunaamini utakuwa na watalii wengi," alisema.

Mchindiuza alisema Bandari ya Nyamirembe ilikuwa ikitumika kwa kiwango kikubwa tangu miaka ya 1960, lakini kutokana na matatizo mbalimbali, iliharibika na kusitisha shughuli zake.

Alisema tayari uhuishaji wa bandari hiyo awamu ya kwanza umekamilika kwa gharama ya Sh. bilioni 1.128, ukihusisha ujenzi wa gati lenye urefu wa mita 128, jengo la abiria, jengo la mizigo, uzio, mnara wa maji na miundombinu ya kusambaza maji sehemu.

"Wakati tunaanza kuhuisha bandari hii, tulitazama mahitaji ya huduma zilizokuwa zikitolewa miaka ya nyuma, tukafanya maboresho kulingana na tathmini hiyo.

"Baada ya kuanza kwa ujenzi wa meli kubwa mpya ya kisasa, tumeamua tuboreshe zaidi bandari hii kufikia kina kinachoendana na meli hiyo kwa sababu hapa itakuwa inafika," alisema.

Aliongeza kuwa awamu ya pili ya ujenzi huo inatarajiwa kuanza baada ya kupitisha bajeti na kwamba itagharimu Sh. milioni 800 kwa kuwa haitakuwa na kazi kubwa kama iliyokuwa awamu ya kwanza.

Mchindiuza alisema wanatarajia kufikia Machi mwakani, meli zitakuwa zimeanza kufika katika bandari hiyo.

Akieleza vikwazo vilivyowakabili katika ujenzi wa gati la bandari hiyo, Mhandisi wa mradi huo kutoka Kampuni ya V.J. Ministry, Anderson Ndogoe, alisema mradi huo ulikamilika Novemba 29, mwaka huu na kilichowachelewesha ni mamba waliokuwa wanaibuka mara kwa mara eneo la mradi.

"Ujenzi wa mradi huu ungekamilika hata kabla ya kipindi tulichokuwa tumekubaliana, lakini tulicheleweshwa na mamba, wakati mwingine walikuwa wanaibuka kila siku ndani ya wiki nzima, kwa hiyo inatulazimu tusitishe kazi," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**KAZI /AJIRA**

**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**au piga simu: 0782253676**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI YA TARAKA NAMBA: 104.2019**

**Mdai:** SISTY FIDELIS MATERU
DHIDI YA
**Mdaiwa:** HAPPY AZAHERI MACKY
**Kwa:** HAPPY A. MACKY WA MODEKO
**Ombi la Mdai:** SISTY FIDELIS MATERU

**Madai ya:** TALAKA NA UANGAZI WA MTOTO.

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 18 mwezi 12 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 10 mwezi 12 mwaka 2019.

115553902

## VYETI VIMEPOTEA



**PETER MGANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0670/0139** kilichotolewa na NYANG'HWALE SEKONDARI mwaka 2009. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0132/0932** kilichotolewa na MILAMBO SEKONDARI mwaka 2012. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **GE/TR/RB/7987/2016.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya wilaya ya Dodoma Mjini**
**Madai na. 68/2019**
**Mdai: Hamisi Anna Kimwala**
**MDAIWA: Costantine Mayala**
**Kwa: Costantine Mayala Mwanza**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**

**MADAI YA TALAKA**

Hivyo unahitajiwa /mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya Tarehe 23/12/2019 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama itadhibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshundwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakamahii leo tarehe 10/12/2019

115553502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**
**Wilaya ya DODOMA**
**MADAI NAMBARI 284/2019**
**MDAI............................................MARIA SHABAN**
**MDAIWA.........................................YUSTER DANIEL**

**Kwa: YUSTER DANIEL**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba **NAMDAI MDAIWA TSH. 517,500/=**
**NILIMDHAMINI BRACK AKATOROKA BILA KULIPA.**

Kwahiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya JUMATATU tarehe 16/12 /2019 saa 02:00 asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashaidi wako na hati zote zilizohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama itadhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshidwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 27/11/2019.

HAKIMU WA MAHAKAMA YA MWANZO

115553002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**

**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU**
**WILAYA YA GEITA**

**SHAURI LA MADAI NA: 54/2019**

**MADAI: JANETH JONATHAN MOBE**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: JOHN WAMBURA WANGWE**
**WA IGUNGA – TABORA**

**AMRI:**
Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 19/12/2019 saa 2:30 asubuhi bila kukosa. Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo, na kutolewa uamuzi. Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama leo JUMATATU tarehe 02 mwezi 12, 2019.

HAKIMU

115553102


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ancelotti ageukiwa na Everton, Arsenal



**MILAN,** Italia

EVERTON itaanza mazungumzo ya mkataba mpya na Carlo Ancelotti baada ya kufukuzwa kama kocha wa Napoli juzi Jumanne usiku.

Kocha wa zamani wa Everton, David Moyes bado anaweza kurudi pale kwenye dimba la Goodison Park kama kocha wa muda, huku kocha atakayepewa mkataba wa kudumu akiwa anaandaliwa, Sky Sports News imethibitisha.

Arsenal pia inamfikiria Ancelotti, ambaye aliinoa Napoli kwa miezi 19, kuchukua nafasi ya Unai Emery, kwa mujibu wa Sky in Italia.

Napoli ilitangaza maamuzi ya kumfuta kazi Ancelotti baada ya kuiongoza klabu hiyo kutinga kwenye hatua ya mtoano wa timu 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ikishinda 4-0 dhidi ya Genk na kumaliza mechi tisa bila kupata ushindi kwenye mashindano yote.

Taarifa ya Napoli ilisomeka: "SSC Napoli imeamua kuvunja mkataba na kocha wa kikosi cha kwanza, Carlo Ancelotti.

"Mahusiano ya urafiki, heshima kati ya klabu, Rais wake (Aurelio De Laurentiis) na Carlo Ancelotti yatabakia kuwa mazuri."

Vitor Pereira, ambaye alionekana kuwa kama ndiye mtu mwenye nafasi kubwa zaidi ya kuchukua nafasi ya kuwa kocha wa Everton, alikataa kuwa mrithi wa Marco Silva mapema Jumanne.

Duncan Ferguson kwa sasa ndiye kocha wa muda wa Everton na alishinda mchezo wake wa kwanza kwa kuifunga Chelsea 3-1 pale kwenye Dimba la Goodison Park.

Sky Sport Italia imeripoti kwamba, kocha wa zamani wa AC Milan, Gennaro Gattuso ndiye anayepewa nafasi kubwa ya kuchukua mikoba ya kuinoa Napoli.

# Klopp: Kweli sikujua Salah alivyofunga



**VIENNA,** Austria

JURGEN Klopp amekubali kuwa "hakuwa na wazo" namna Mohamed Salah alivyoweza kufunga bao la pili kwa Liverpool wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Salzburg kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi.

Mabingwa hao watetezi walijihakikishia nafasi ya kutinga hatua ya mtoano ya 16-bora na kuwa vinara wa Kundi E kwenye mchezo huo uliopigwa nchini Austria, kwa mabao ya Naby Keita na Salah.

Salah alifunga bao kwa shuti la mguu wa kulia baada ya jitihada za kumzunguka golikipa, Cican Stankovic.

Alipoulizwa namna gani Salah alivyoweza kufunga bao hilo, Klopp aliiambia BT Sport: "Sikuwa na wazo, wala sikufikiri.

"Kuwa mkweli kwa kuangalia ubora wake na namna gani anavyofanya uwanjani na bila kujali yupo kwenye hali gani, sikujua ni jinsi gani anaweza kufunga.

"Kwa usiku ule wa kuvutia kila mmoja alikuwa na uwezo wa kufunga bao hasa kutokana na ubora wa wachezaji wangu.

"Lakini ukiangalia namna ilivyo, kwa uhakika walikuwa kwenye nafasi nzuri na kikosi kizima kilicheza kwa staili ya kuvutia kabisa."



# Lampard: Sokoni Januari hakutawaathiri makinda

**LONDON,** England

FRANK Lampard amesisitiza mara zote alikuwa anaangalia namna ya kuiimarisha Chelsea na kwa kuwa sasa wamepata ruhusa ya kufanya usajili, anaamini wachezaji wapya hawatawaathiri vijana.

Chelsea adhabu yao ya kutofanya usajili ilifutwa wiki iliyopita na sasa watafanya usajili wa kipindi cha Januari.

Hadi sasa ameweza kuonyesha kiwango cha kuvutia licha ya kutofanya usajili – kwani Chelsea wapo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu na wameshafuzu hatua ya mtoano wa timu 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Lille, Jumanne.

Na Lampard amebainisha kwamba, mara zote alikuwa na hamasa ya kuona kikosi chake kinaimarika kwa staili ya uchezaji.

"Nitaangalia maeneo yote ya timu," alisema Lampard.

"Kipindi cha majira ya joto tulimpoteza Eden Hazard, ambaye alikuwa sehemu kubwa ya kufunga na kutengeneza mabao.

"Nafikiri tumegundua sehemu ya timu ambazo bado zitakuwa na ushindani kwa timu.

"Tumeonyesha hivyo kwenye ligi na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Lakini tunaangalia mbele, na tunaweza kuwa bora zaidi.

"Tunaweza kuwa bora kwa kupata wachezaji wengine wa kusaidia timu na kwa uhakika tunaweza kupiga hatua nzuri zaidi."

## HABARI MICHEZO



# Liverpool imethibitisha ubora wake – Van Dijk

**VIENNA, Austria**

VIRGIL van Dijk anaamini Liverpool imethibitisha tena ubora wao kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Salzburg kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne.

Vinara hao wa Ligi Kuu ya England walirudisha matumaini yao ya kutetea taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, shukrani kwa mabao mawili ya Naby Keita na Mohamed Salah, na hivyo kujivuta kileleni mwa msimamo wa Kundi E na kutinga hatua ya mtoano wa timu 16 bora.

Kikosi hicho cha Jurgen Klopp kilionyesha ubora wake kwenye mchezo huo.

"Nafikiri inajielezea yenyewe ubora tulionao," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nafikiri ni ngumu kuja hapa. Ni nafasi yao kwa maisha yao ya soka kutinga hatua ya mtoano.

"Tulijua nini tutarajie, hasa mwanzoni, ilikuwa ngumu. Ni timu nzuri. Wana wachezaji wazuri, walikuwa na presha kubwa, walionekana kuwa bora zaidi.

"Tulitakiwa kuhimili hilo na kwa uhakika tulikuwa kwenye wakati mzuri na tulitulia na nafikiri tulifanya vizuri."



# England, Italia sasa kujipima Euro 2020

**LONDON, England**

TIMU ya Taifa ya England itacheza mchezo wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya Italia Machi 27, mwakani kwenye Uwanja wa Wembley jijini London.

Chama cha Soka England (FA), kimethibitisha taarifa za kuchezwa kwa mchezo huo, ambao utakuwa sehemu ya maandalizi ya kuelekea fainali za Mataifa ya Ulaya, Euro 2020.

Mataifa ya England na Italia yamefuzu kucheza fainali hizo, ambazo kwa mara ya kwanza mwaka 2020, zitachezwa kwa mfumo mpya wa kuzunguka viwanja mbalimbali barani Ulaya.

Kwa mara ya mwisho timu za England na Italia zilikutana miaka miwili iliyopita na zilitoka sare ya bao 1-1.

Katika fainali za Euro 2020, England imepangwa Kundi D lenye timu za Croatia, Jamuhuri ya Czech na mshindi atakayepatikana katika michezo ya mchujo ya kufuzu wakati Italia wamepangwa Kundi A na Uturuki, Wales na Uswisi.

Fainali za Euro 2020 zimepangwa kuanza Juni 12, mwakani, katika viwanja mbalimbali barani Ulaya.

# Guardiola ampa nafasi Foden kumrithi Silva

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola anashawishika kwamba, Phil Foden ana uwezo wa kuwa mchezaji muhimu zaidi wa Manchester City baada ya David Silva kuondoka klabuni hapo.

Silva mwenye umri wa miaka 33, tayari amethibitisha nia ya kuondoka hapo City mwishoni mwa msimu huu wakati mkataba wake utakapokuwa umemalizika na kumaliza kipindi chake cha misimu 10 ya kukaa na klabu hiyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania alikuwa nembo ya City, huku wengi wakimtaja kwamba ni mmoja wa wachezaji bora wa kigeni kwenye Ligi Kuu ya England.


Mara nyingi amekuwa akikaa nje kwenye Ligi Kuu msimu huu, akicheza mechi mbili tu kwenye Ligi ya Mabingwa pia aliukosa mchezo wa jana dhidi ya Dinamo Zagreb, pamoja na Sergio Aguero na John Stones.

"Wachezaji wote watatu ni majeruhi," Guardiola alithibitisha Jumanne."David aliumia zaidi na ni hatari kumchezesha haraka.

"John atakuwa nje wiki chache zijazo, Sergio ni bora na hayupo tayari."

Kutokuwapo kwa Silva maana yake kinda huyo wa timu ya Taifa ya England chini ya umri wa miaka 21, Foden ndiye atachukua nafasi yake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, msimu huu amecheza dakika 83 kwenye Ligi Kuu ya England.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FATI AWEKA REKODI UEFA BARCA IKIIANGAMIZA INTER

●●● Amekuwa mchezaji kinda zaidi kuwahi kufunga Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku pia...

**TURIN,** Italia

Ansu Fati ameweka rekodi kwa kuwa mchezaji kinda zaidi kuweza kufunga bao katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Barcelona ikihitimisha matumaini ya Inter Milan kutinga hatua ya 16-bora juzi.

Fati ambaye juzi alikuwa na umri wa miaka 17 na siku 40, sasa ameipiku rekodi hiyo iliyokuwa ikishikiliwa na Samir Handanovic.

Tayari alikuwa kinda mdogo zaidi kuwahi kuifungia Barca kwenye LaLiga na mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kuichezea Barcelona kwenye Ligi ya Mabingwa.

**Mapema mwezi huu, Barca ilimtunuku Fati mkataba mpya ambao utamalizika Juni 2022, na kuongeza kipengele kinachomruhusu kuuvunja kutoka euro milioni 100 hadi euro milioni 170.**

Katika mechi hiyo ya juzi, Fati alitokea benchi dakika ya 85 na dakika moja baadaye akaitendea haki pasi ya Luis Suarez kuifungia Barcelona bao la pili wakati ikishinda 2-1 dhidi ya vinara hao wa Serie A.

Barcelona, ilikuwa tayari imeshafuzu hatua ya 16-bora, na ilipata bao la kuongoza kupitia kwa Carles Perez ambaye huo ulikuwa mchezo wake wa kwanza kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa.

Romelu Lukaku aliisawazishia Inter kwa mkwaju wa maguu 25 ya mtu mzima, lakini bao la dakika ya mwisho kupitia kwa Fati liliitoa Inter ambayo sasa itahamia kwenye michuano ya Europa League.

"Nilicheza kwa kutoa na kwenda na Luis na wakati nilipofunga uwanja ulikuwa kimya. Nimefurahi sana," alisema Fati, ambaye alikichezea kikosi cha Hispania U-21.

"Ni ndoto. Kila kitu kinaonekana kwenda kwa kasi kubwa. Nitaitumia tu kila fursa ninayopewa. Lakini hapa, unaangalia pande zote na fikiria: 'Nimefanya nini'?"

Kocha wa Barcelona, Ernesto Valverde alisifu uwezo wa umaliziaji wa straika huyo na kusema: "Ansu amezaliwa kufunga na ingawa alikuwa na maumivu tulimtaka apate dakika chache.

"Kwamba ni kijana wa Barca ambaye ndiye mdogo zaidi aliyefunga katika mashindano haya, anatufurahisha."

Miamba hiyo ya Italia ilianza mechi hiyo ya Kundi F na ikihitaji kufikia matokeo ya Borussia Dortmund ili kusonga mbele kwenye michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2011-12.

Hata hivyo, Dortmund ilishinda 2-1 ikiwa nyumbani dhidi ya Slavia Prague hivyo kumaliza nafasi ya pili, na Inter ikimaliza ya tatu.

## KWA UFUPI

### NEYMAR, MBAPPE WAIKUNA LIVER

Liverpool, Manchester City na Chelsea ni miongoni mwa timu sita zinazovutiwa na washambuliaji wa Paris St-Germain, Mbrazil Neymar, 27, na Kylian Mbappe, 20. (Le Parisien, via Mirror)

### UNITED YAJIPANGA BILA POGBA

Manchester United inajiandaa kwa Paul Pogba, 26, kuondoka kwa kusajili kiungo wa kati mbadala kabla ya msimu ujao. Kiungo wa Ajax, Donny van de Beek na wa Atletico Madrid, Saul Niguez ni miongoni wanaweza kusajiliwa. (Daily Mail)

### ANCELOTTI AWINDWA EVERTON

KOCHA Mtaliano Carlo Ancelotti, aliyetimuliwa na Napoli Jumanne usiku, ni chaguo la kwanza kwa Everton katika mpango wao wa kutafuta mrithi wa Marco Silva. (Telegraph)

### UMTITI KATIKA RADA ZA UNITED

Manchester City inahitaji beki mpya na ipo mbioni kumsajili nyota wa Ufaransa Samuel Umtiti, 26, kutoka Barcelona. (L'Equipe, via TEAMtalk)

### JUVE HAITANII KWA WILLIAN

Juventus imeweka mezani ofa ya wazi kwa mshambuliaji wa Chelsea, Willian, 31, ambaye mkataba wake unamalizika majira ya joto. (Daily Mirror)

### IBRAHIMOVIC ANUKIA EVERTON

Zlatan Ibrahimovic anaweza kushtukiza kwa kurejea Ligi Kuu England baada ya Everton kumpa ofa ya pauni milioni nne kwa msimu mshambuliaji huyo wa zamani wa Sweden mwenye umri wa miaka 38. (Express)

### ARSENAL NAYO KWA ANCELOTTI

Arsenal nayo itaingia sokoni kuutafuta ufundi wa Carlo Ancelotti wakati huu ikitafuta mrithi wa Unai Emery, ambaye alitimuliwa mwezi uliopita. (Daily Mail)

### ABRAMOVICH AKATAA KUIUZA CHELSEA

Roman Abramovich ameikataa ofa kutoka kwa mmiliki wa LA Dodgers, Todd Boehly ya kuinunua Chelsea. (Telegraph)

### CONTE AWATAKA ALONSO, PEDRO

KOCHA wa Inter, Antonio Conte anamtaka beki wa kushoto asiyekubalika Chelsea, Marcos Alonso, 28, kujiunga naye hapo Italia sambamba na winga Pedro, 32, na straika Mfaransa Olivier Giroud, 33, pia kunauwezekano wa kuondoka hapo Stamford Bridge. (Goal.com)

### SOUTHGATE AMPA NENO VARDY

KOCHA wa England, Gareth Southgate amemwambia mshambuliaji wa Leicester, Jamie Vardy kuwa "mlango upo wazi" kwake kufikiria tena uamuzi wake wa kustaafu soka la kimataifa. (BeinSports via the Sun)

### BARCA YAJITOA KWA MARTINEZ

Barcelona imekimbizwa na dau la pauni milioni 84.6 zinazohitajika ili kumpata mshambuliaji wa Inter Milan na Argentina, Lautaro Martinez, 22. (ESPN)

### TOMORI KUJIFUNGA UPYA CHELSEA

BEKI wa England, Fikayo Tomori, 21, anakaribia kuongeza mkataba wake Chelsea. (Goal)

HABARI MICHEZO

# TANZANIA BARA, KENYA ZASHIKWA CECAFA U-17

**Na Mwandishi Wetu,** JINJA

HAKUNA mbabe! Ndiyo unavyoweza kusema baada ya timu ya soka ya wasichana wa umri chini ya miaka 17 ya Tanzania Bara, ambayo ilianza kwa kishindo mashindano ya Kombe la Chalenji, jana kulazimishwa sare ya mabao 3-3 dhidi ya wenzao kutoka Burundi.

Kwa matokeo hayo, Tanzania Bara imefikisha pointi nne sawa na Kenya ambayo nayo mapema jana asubuhi ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Eritrea iliyoonyesha kiwango kizuri katika vipindi vyote viwili.

Katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Njeru, Tanzania Bara ilienda mapumziko ikiwa mbele kwa mabao 2-1.

Mabao ya Tanzania Bara katika mchezo wa jana yalifungwa na Joyce Meshack aliyefikisha mabao manne katika michuano hii, Aisha Masaka na Christer Behela wakati Lydia Karenzo, Neema Nzohabonayo na Bora Ineza walifunga kwa upande wa Burundi.

Katika mechi ya mapema jana asubuhi, Eritrea ndio walikuwa wa kwanza kupata bao kupitia kwa Misgana Mehari na Kenya ilisawazisha kupitia kwa mshambuliaji wake Sylvia Makungu na kufanya wagawane pointi.

Leo ni mapumziko na mashindano hayo yanayoandaliwa na Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa) yataendelea tena kesho kwa Tanzania Bara kucheza dhidi ya Kenya, Burundi itawavaa Djibouti na Uganda watawakaribisha Eritrea.




Wachezaji wa Simba, winga Deo Kanda (kushoto) akipata upinzani mkali kutoka kwa beki wa pembeni Shomari Kapombe, huku kiungo Mbrazil Gerson Fraga Vieira (kulia) akienda kumpa msaada wakati wa mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika katika Uwanja wa Simba Mo Arena, Bunju jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Mgunda akiri Z'bar Heroes kuwahenyesha

**Na Somoe Ng'itu, JINJA**

ILIKUWA ni zaidi ya vita! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa timu soka ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), Juma Mgunda, baada ya timu yake kupata ushindi dhidi ya ndugu zao Zanzibar (Zanzibar Heroes), katika mechi ya Kombe la Chalenji iliyochezwa juzi nchini hapa.

Ili ijihakikishie kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo ya Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, wawakilishi hao wa Tanzania Bara watalazimika kushinda mechi yao ya mwisho dhidi ya Sudan itakayochezwa Jumamosi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda, alisema mchezo huo ulikuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa kuliko mechi nyingine walizowahi kucheza "wana ndugu hao".

Mgunda alisema wachezaji wake walipambana "kufa kupona", kwa sababu walijua hiyo ndio ilikuwa sawa na fainali yao katika mashindano hayo ambayo mwaka huu yanashirikisha nchi tisa.

"Kwanza ninawapongeza sana Zanzibar kwa kiwango walichokionyesha katika mchezo wa jana (juzi), mechi ilikuwa na ushindani na ngumu haswa, ila mchezo wa mpira pia unategemea bahati, kwa jana (juzi) ilikuwa kwetu, walifanya kosa moja na sisi tukawaadhibu," alisema Mgunda.

Kocha huyo aliongeza kuwa watajipanga zaidi kwa ajili ya mchezo unaofuata na kamwe hawatawadharau Sudan, kwa kutoangalia matokeo waliyopata katika mechi zao zilizotangulia.

"Huwezi kumdharau mpinzani wako, tutaingia uwanjani kupambana zaidi ya ilivyokuwa dhidi ya Zanzibar Heroes kwa sababu tunataka kusonga mbele, najua hakuna mechi rahisi, tunahitaji kushinda na kuweka heshima katika mashindano haya," Mgunda alisema.

Naye mfungaji wa bao pekee katika mchezo huo dhidi ya Zanzibar Heroes, Ditram Nchimbi, alisema anafurahi kufunga bao hilo muhimu na anapenda kuwaambia Watanzania kwamba bado wataendelea kupambana katika mechi inayofuata.

Nchimbi alisema kuwa wanafahamu Sudan ni timu ngumu, hivyo wanahitaji kuongeza bidii zaidi ili wapate ushindi na kusonga mbele katika mashindano hayo.

Mabingwa watetezi Kenya (Harambee Stars), ambao wana pointi sita, tayari wameshafuzu hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo ambayo fainali zake zitachezwa Desemba 19, mwaka huu.

## Kitambi: Nimepata ujuzi mwingi Simba

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kufikia makubaliano ya pamoja na Bodi ya Wakurugenzi ya Klabu ya Simba ya kuhitimisha mkataba wake kama kocha msaidizi, Dennisi Kitambi aliyekuwa akimsaidia Kocha Mkuu Mbelgiji Patrick Aussems, amekiri kupata ujuzi wa kutosha kutoka kwa benchi la ufundi na uongozi mzima wa klabu hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kitambi alisema amejifunza mambo mengi wakati alipopewa jukumu zito la kuinoa timu hiyo, baada ya Aussems kutupiwa virago vyake.

"Nimepata uzoefu na nimejifunza mambo mengi nilipokuwa Simba, naamini nitayafanyia kazi popote niendapo," alisema Kitambi.

Aidha, alisema ameachana na klabu hiyo kwa amani kwani makubaliano yao yalikuwa yamemalizika.

"Nimeondoka kwa amani makubaliano yetu yameisha vizuri hakuna kitu chochote ninachodai," alisema.

Kadhalika, Kitambi aliwashukuru viongozi pamoja na wachezaji wa klabu hiyo kwa ushirikiano mzuri waliompa katika kipindi chote na kuwataka wachezaji hao wazidishe juhudi pamoja na nidhamu.

Kitambi aliachana na Klabu hiyo juzi kwa amani, huku Bodi hiyo ya Wakurugenzi ikimtambulisha aliyekuwa Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Selemani Matola kuwa kocha msaidizi.

## Machomane: Uzoefu unatugharimu Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Machomane inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, imesema matokeo mabaya wanayoyapata katika ligi hiyo kunatokana na wachezaji wake kutokuwa na uzoefu wa kutosha kwenye kinyang'anyiro hicho.

Machomane ambayo imepanda daraja msimu huu, imeshashuka dimbani mara 10 huku ikipoteza michezo sita, sare mbili na kushinda mechi mbili, matokeo ambayo yanaifanya kushika nafasi ya tatu kutoka mkiani mwa ligi hiyo yenye timu 16.

Akizungumza na gazeti mwishoni mwa wiki, Katibu wa timu hiyo, Mohmed Kombo, alisema kuanza vibaya kwa timu hiyo kumetokana na wachezaji kutokuwa wa uzoefu na Ligi Kuu, huku wakikutana na timu ambazo wachezaji wake wamecheza ligi hiyo kwa miaka mingi.

Alisema kupitia michezo hiyo waliyocheza imesaidia kuwapa uzoefu na kujiamini kwa wachezaji kutokana na kutofungwa mabao mengi kama ilivyokuwa mwanzoni mwa ligi hiyo.

Alisema licha ya kutokuwa wazoefu katika ligi hiyo, lakini bado kuna changamoto ya washambuliaji hali inayowasababishia kushindwa kupachika mabao pale wanapopata nafasi, hivyo ni moja ya idara ambayo watakwenda kuiimarisha katika usajili wa dirisha dogo.

# Michezo

Alhamisi Desemba 12, 2019

Nipashe


## Fati aweka rekodi Uefa Barca ikiiua Inter



HABARI UK. 30

## Samatta aondoka na Ancelotti Uefa

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta usiku wa kuamkia jana amehitimisha safari ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu kwa kipigo cha mabao 4-0 ugenini dhidi ya Napoli huku akimaliza na mabao matatu kwenye michuano hiyo.

Hata hivyo, safari ya Samatta na timu yake ya KRC Genk ya kuaga michuano hiyo, ilienda sambamba na kutimuliwa kwa Kocha Mkuu wa Napoli, Mtaliano Carlo Ancelotti (pichani) , ambaye licha ya ushindi huo uliowawezesha kufuzu hatua ya 16-bora, uongozi wa klabu hiyo haukuona sababu ya kuendelea na huduma yake.

Napoli ilitangaza maamuzi ya kumfuta kazi Ancelotti muda mfupi baada ya kuiongoza klabu hiyo kutinga hatua ya mtoano wa timu 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ikishinda 4-0 dhidi ya Genk na kumaliza gundu lake la mechi tisa bila kupata ushindi katika mashindano yote.

Taarifa ya Napoli ilisomeka: "SSC Napoli imeamua kuvunja mkataba na kocha wa kikosi cha kwanza, Carlo Ancelotti.

"Mahusiano ya urafiki, heshima kati ya klabu, Rais wake (Aurelio De Laurentiis) na Carlo Ancelotti yatabakia kuwa mazuri."

Katika mechi hiyo ya Kundi E, iliyopigwa Uwanja wa San Paolo mjini Napoli, nahodha huyo wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Samatta, alicheza kwa dakika 63 tu kabla ya kumpisha winga Theo Bongonda, ambaye hata hivyo hakuweza kusaidia kubadili matokeo.

Kwa matokeo hayo, Genk imemaliza mechi zake za hatua ya makundi bila ushindi hata mmoja kufuatia kufungwa michezo mitano na kutoa sare moja, hivyo kuburuza mkia katika kundi lake lililokuwa likizijumuisha Salzburg iliyomaliza nafasi ya tatu kwa kuvuna pointi saba nyuma ya Napoli (pointi 12) na mabingwa watetezi, Liverpool waliomaliza kileleni na pointi 13.



PAMBANA...



Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, anayeichezea KRC Genk ya Ubelgiji, Mbwana Samatta (jezi ya bluu) akipambana kuwania mpira na beki wa kati wa Napoli, Msenegal Kalidou Koulibaly katika mechi ya Kundi E ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa Uwanja wa San Paolo, Italia na wenyeji hao kushinda 4-0 juzi. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAPUKUTISHA MAPRO, BALINYA NJE

### ●●● Wengine zaidi kutemwa, mishahara mikubwa yadaiwa chanzo, yatakiwa kugeukia wazawa wa bei poa ambao...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya juzi uongozi wa Klabu ya Yanga kutangaza kuvunja mkataba na mshambuliaji Mnamibia Sadney Urikhob, huku pia ikikiri kuelemewa na madeni, hatimaye jana 'kituo kinachofuta' kimeangukia kwa straika Mganda Juma Balinya kufuatia kuachana naye.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Klabu Yanga: "Klabu ya Yanga inapenda kuujulisha umma kwamba tumefikia makubaliano ya kuvunja mkataba na aliyekuwa mchezaji wetu Juma Balinya kutoka Uganda.

"Yanga tunamshukuru Balinya kwa huduma yake alipokuwa akiitumikia klabu hii na tunamtakia kila la kheri katika maisha yake ya soka huko aendako."

Juzi Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla alitangaza klabu hiyo kuelemewa na madeni hatua iliyosababisha wachezaji kudai mishahara yao ya miezi miwili hadi baadhi kufikia uamuzi wa kuomba kuvunja mikataba yao.

Miongoni mwa wachezaji walioelezwa kuandika barua ya kuomba kuvunja mikataba yao na klabu hiyo ni beki Mghana Lamine Moro na Mkongomani David Molinga, ambao uongozi hautaki kabisa kuona wakiondoka kutokana na kuvutiwa na viwango vyao.

Wengine ni Sadney na Balinya ambao tayari wametangazwa kuachana na klabu hiyo, Mnyarwanda Issa Bigirimana na Mzambia Maybin Kalengo, ambao miongoni mwao inadaiwa wanaweza kukutana na panga kabla ya dirisha dogo la usajili kufunguliwa Jumatatu.

Hata hivyo, jana asubuhi katika kipindi cha michezo kilichorushwa na redio moja jijini Dar es Salaam kabla ya mchana Yanga kutangaza kufikia uamuzi huo wa kuachana na Sadney, wanachama na mashabiki wengi wa klabu hiyo walipiga simu wakipendekeza uongozi kugeukia wachezaji wazama ili kuweza kumudu gharama za kuwalipa mishahara.

Walisema nyota wengi wa nje ni gharama kubwa kuwalipa hususan wakati huu klabu hiyo ikipita katika kipindi kigumu kiuendeshaji.

Kwa upande wake aliyewahi kuwa Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Omary Kaaya alisema ili klabu hiyo iweze kuendelea lazima ibadilishe mfumo uliopo kwa sasa na kwamba suala la uongozi wao kuacha madeni ni kweli, lakini cha muhimu ni kutazama kilicho muhimu kutekeleza ili wasonge mbele.

"Sasa hivi ni wakati wa Klabu ya Yanga kubadilika na kugeukia mfumo wa uwekezaji na hisa hapo tutafikia malengo yetu," alisema Kaaya.

"Tuliacha madeni kwa sababu tulikuwa na hali mbaya sana kila mtu aliona hali halisi ilivyokuwa, lakini uongozi wa sasa unapaswa kutoa kipaumbele kwa yale mambo ya muhimu kwa sasa ili kusonga mbele," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >